# Masomo ya Kiswahili Sanifu

## Kidato cha

## 2

## Kitabu cha Mwanafunzi

Ahmed E. Ndalu

moran
PUBLISHERS

Moran (E.A.) Publishers Limited,
Judda Complex, Forest Road,
P.O. Box 30797-00100, Nairobi, Kenya

With offices and representatives in: Uganda, Rwanda, Tanzania, Malawi and Zambia

www.moranpublishers.com

© Ahmed E. Ndalu, 2016 – mswada
© Moran (E. A.) Publishers Ltd., 2016 – michoro

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna ruhusa ya kuiga, kunakili, kutafsiri au kuchapisha aya yoyote ya kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile, isipokuwa iwe imeidhinishwa kwa barua na wachapishaji; au kuambatana na masharti ya sheria za kunakili, kusanii na kuiga (Copyright, Design and Patents Act) ya 1988. Mtu yeyote anayefanya kitendo kilicho kinyume cha sheria kuhusu kitabu hiki anaweza kushtakiwa.

Kimepigwa chapa na

ISBN: 978 9966 34 992 7

2020 2019 2018 2017 2016
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

# Yaliyomo


**Utangulizi ..................................................................................... vi**

**Sura 1:Mazungumzo na majadiliano........................................................ 1**

Msamiati wa msingi kuhusu mazao na shughuli za kilimo na ufugaji nchini Rwanda.......................................................................................... 1

Msamiati wa mazao nchini Rwanda .................................................. 1

Msamiati kuhusu shughuli za kilimo nchini Rwanda ............................ 5

Msamiati kuhusu shughuli za ufugaji nchini Rwanda............................ 9

Majira ya mwaka nchini Rwanda.......................................................... 12

Msamiati wa msingi kuhusu wanyama wa porini na umuhimu wake......... 15

Msamiati wa wanyama wa porini nchini Rwanda.................................... 15

Umuhimu wa wanyama wa porini nchini Rwanda.................................. 18

Matini ya Kiswahili kuhusu kilimo na ufugaji pamoja na vipengele vya kisarufi.......................................................................................... 20

Nomino ........................................................................................ 20

Vivumishi...................................................................................... 23

Viwakilishi .................................................................................... 34

Vielezi .......................................................................................... 37

Matumizi ya wakati uliopo na uliopita na vitenzi vya silabi moja................ 39

Matumizi ya wakati uliopo -na- na vitenzi vya silabi moja........................ 39

Matumizi ya wakati uliopita -li- na vitenzi vya silabi moja ........................ 40

Maswali ya marudio ........................................................................ 41

**Sura 2: Utungaji ............................................................................ 43**

Barua............................................................................................ 43

Barua za kirafiki ............................................................................ 43

Barua rasmi .................................................................................. 49

Matangazo mbalimbali .................................................................... 55

Ilani ............................................................................................. 61

Mialiko.......................................................................................... 63

Aina za alama za uandishi na matumizi yake ........................................ 67

Aina za viakifishi ........................................ 67
Maswali ya marudio ........................................ 70
**Sura 3: Matumizi ya lugha katika mazingira mbalimbali ........................................ 72**
Rejesta mbalimbali nchini Rwanda ........................................ 72
Rejesta ya mpira wa miguu ........................................ 72
Rejesta ya burudani ........................................ 76
Umuhimu wa michezo na burudani ........................................ 78
Umuhimu wa michezo ........................................ 78
Umuhimu wa burudani ........................................ 80
Rejesta ya hotelini ........................................ 81
Rejesta ya mahakamani ........................................ 83
Rejesta ya bungeni ........................................ 87
Rejesta ya sokoni ........................................ 89
Rejesta ya kanisani ........................................ 90
Rejesta ya sarufi ya Kiswahili ........................................ 92
Matumizi ya majina ya ngeli ya KI-VI katika umoja na wingi ........................................ 97
Matumizi ya majina ya ngeli ya KI-VI ........................................ 100
Matumizi ya majina ya ngeli ya KI-VI pamoja na vivumishi ........................................ 101
Maswali ya marudio ........................................ 105
**Sura 4: Mazungumzo na mawasiliano katika shughuli mbalimbali za kijamii ........................................ 107**
Shughuli mbalimbali za jumuiya ........................................ 107
Mkutano wa kijiji chetu ........................................ 107
Sherehe ya harusi ya rafiki yangu ........................................ 109
Mazishi ........................................ 111
Kazi ya *umuganda* ........................................ 113
Namna sahihi ya kuuliza maswali ........................................ 114
Aina saba za maneno ........................................ 116
Nomino ........................................ 117
Vitenzi ........................................ 119
Vielezi ........................................ 120

Vivumishi ........................................................................................................ 122
Viwakilishi ..................................................................................................... 124
Viunganishi ..................................................................................................... 126
Vihisishi .......................................................................................................... 127
Matumizi ya wakati uliopita -li- hali yakinishi na hali kanushi ................... 129
Matumizi ya wakati ujao -ta- katika hali yakinishi na hali kanushi ............ 130
Maswali ya marudio ....................................................................................... 131
Faharasa .......................................................................................................... 133
Vitabu vya rejea .............................................................................................. 137

# Utangulizi

Mwanafunzi, pokea hongera za dhati kwa kuingia katika Kidato cha Pili. Kuingia kwako katika kidato hiki kuna maana kwamba umefanya kazi kwa bidii na umewaridhisha walimu wako kuwa unaweza kupiga hatua nyingine katika kuendeleza masomo yako.

Kiswahili ni somo muhimu katika maisha yako. Kitakuwezesha kuwasiliana na watu mbalimbali ndani na nje ya Rwanda. Kiswahili kinazungumzwa katika nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki kama vile Kenya, Tanzania, Uganda na kadhalika.

Kiswahili kinahitajika katika baadhi ya taaluma au ajira ambazo unaweza kuingia. Taaluma au ajira hizi ni pamoja na uandishi wa habari, biashara, huduma kwa wateja, uongozaji watalii, ukalimani na tafsiri. Hivyo, somo la Kiswahili linakuwezesha kumudu ipasavyo stadi zote nne za mawasiliano ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika kwa ufasaha. Pia, utapata nafasi ya kupata stadi za kushiriki kwa ufasaha katika mawasiliano rasmi na yasiyo rasmi. Hii inakusaidia kwa sasa na baadaye. Utaweza kushiriki kwa ukamilifu katika shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi, na kisiasa ambazo zinahitaji matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Kitabu hiki cha Masomo ya Kiswahili Sanifu kimeandikwa kwa nia ya kukuongoza wewe mwanafunzi wa Kidato cha Pili kujua jinsi ya kuwasiliana na kutumia Kiswahili katika mazingira mbalimbali. Masomo yaliyomo kitabuni humu yamepangwa kwa njia ambayo itakuwezesha kuendelea katika masomo yako hatua kwa hatua. Katika kufanikisha jambo hilo, mada nne zilizopendekezwa katika silabasi zimeshughulikiwa kikamilifu. Mada hizo ni:

1. Mazungumzo na majadiliano
2. Utungaji
3. Matumizi ya lugha katika mazingira mbalimbali
4. Mazungumzo na mawasiliano katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Utagundua kwamba msisitizo mkubwa katika mada hizi ni kukuwezesha kutumia lugha ya Kiswahili katika mawanda mapana. Nafasi kubwa imepewa stadi za kusikiliza na kuzungumza. Hii ndiyo sababu kitabu kina shughuli nyingi za kufanywa na wanafunzi wawili wawili na katika vikundi. Shughuli hizo zinalenga kukupa fursa nyingi za kuwasiliana na wanafunzi wenzako kwa lugha ya Kiswahili. Hili halimaanishi kwamba stadi za kusoma na kuandika hazijapewa nafasi ya kutosha. La! Stadi hizi pia zimeshughulikiwa lakini kwa kutambua kuwa ili uweze kusoma na kuandika ni lazima kwanza uwe na uwezo wa kuwasiliana kimazungumzo.

Kitabu hiki kinakuonesha jinsi ya kupanga vilivyo yale ambayo umeyasikia na kuyasoma. Kwa kufanya hivi, utaweza kuwasiliana vilivyo na yeyote yule awe ametoka wapi bora tu naye huyo anakifahamu Kiswahili.

Isitoshe, kwa kutumia kitabu hiki utaweza kusoma kwa wepesi na kuelewa unachosoma. Pia, utajifikiria mwenyewe katika lugha hii na kujitegemea katika mawazo yako bila kuogopa kwamba utakosea katika usemi wako. Isitoshe, masomo haya ni msingi imara wa masomo ya vidato vinavyofuata.

Mpangilio uliotumiwa kitabuni humu ni mwepesi sana wa kutambulika. Kwanza kuna sura, halafu kuna mada kuu ya sura hiyo ikifuatwa na mada ndogo kama ilivyopendekezwa katika silabasi. Msisitizo mkubwa umewekwa katika mbinu za wewe mwenyewe kujifanyia mambo. Katika hili, utapata kuwa utahitajika kujiunga na mwenzako au wenzako ama utashiriki kama darasa zima kutekeleza shughuli mbalimbali.

Kitabu hiki pia kina kazi ya kutosha ya kufanywa na wewe binafsi baada ya kila funzo. Vilevile, kitabu hiki kina mazoezi ya marudio baada ya kila mada kuu ili kupima uelewa wako wa mambo yaliyoshughulikiwa katika mada kuu hiyo.

Iwapo kitabu hiki kitakuwa dafina kwako, basi azma yangu kuu ya kukiandika itakuwa imekamilika.

Karibu!

Ahmed E. Ndalu

(Mwandishi)

# 1 Mada kuu: Mazungumzo na majadiliano



## Mada ndogo: Msamiati na mawasiliano katika shughuli za kilimo na ufugaji

### A Msamiati wa msingi kuhusu mazao na shughuli za kilimo na ufugaji nchini Rwanda.

***i) Msamiati wa mazao nchini Rwanda***

*Tazama mazao yafuatayo na usome maneno chini yake.*



**1 Matunda**

| | | | |
|---|---|---|---|
|  papai |  parachichi |  embe |  pera |
|  tufaha |  nanasi |  chungwa |  ndizi |


**2 Mboga na viazi**

| | | | |
|---|---|---|---|
|  sukumawiki |  boga |  mbatata |  kiazi kitamu |

**3. Nafaka**

| | | | |
|---|---|---|---|
|  mahindi |  maharagwe |  mchele |  mtama |

## 4. Viungo

| | | | |
|---|---|---|---|
|  |  |  |  |
| kitunguu | karoti | nyanya | pilipili hoho |

Bidhaa zilizopo kwenye michoro zinaitwa mazao. Mazao ni vitu tunavyovuna baada ya kupanda mbegu zake. Ni vitu vinavyozaliwa na mimea iliyopandwa. Hapa nchini Rwanda, udongo wetu ungali na rutuba ya kutoa mazao mema. Tunapanda mimea mbalimbali inayotupatia mazao.

***Tazama mifano zaidi ya mazao yanayopatikana hapa nchini Rwanda na usome vifungu kando yake.***




Kahawa ni zao la mkahawa au mbuni. Kahawa hukaushwa na kusagwa ili kutoa ungaunga. Ungaunga huo hutumiwa kwa kutengenezea kinywaji cha kahawa. Kinywaji cha kahawa kina ladha nzuri. Kahawa pia huuzwa katika nchi za nje na kuletea nchi yetu pesa za kigeni.



Haya ni majani ya mchai. Majani ya mchai hukaushwa na kusagwa. Majani haya hutumiwa kutengenezea kinywaji cha chai. Nchi yetu huuza majani ya mchai katika nchi za kigeni. Majani ya mchai pia huletea nchi yetu pesa za kigeni.



Hizi ni ndizi. Ndizi ni zao la mgomba. Ndizi humea kwenye mkungu. Ndizi inaweza kuivishwa na kuliwa moja kwa moja. Baadhi ya ndizi hupikwa na kuliwa. Ndizi pia huuzwa na kutuletea mapato.



Haya ni maharagwe. Maharagwe ni zao la mharagwe. Nafaka hii ni muhimu sana kwa chakula chetu. Hii ni kwa kuwa virutubishi vyake vya protini huhitajika sana miilini mwetu. Wale ambao hawali nyama mara kwa mara huweza kupanda miharagwe na kupata protini zao kutoka kwayo.




Huu ni mtama. Mtama huzaa punje ndogo ndogo. Punje za mtama hukaushwa na kuchanganywa na mihogo au mahindi. Baadaye husagwa ili kupata unga. Unga huu hutengenezewa uji au sima (ugali).



Haya ni mahindi. Mahindi ni mazao ya mhindi. Mahindi hukaushwa na kusagwa ili kutoa unga wa dona. Unga wa mahindi hutengenezewa sima au ugali. Mahindi pia yanaweza kupikwa pamoja na maharagwe kutengenezea pure au kande. Pure ni chakula kitamu kinachoshibisha vilivyo. Ama hindi linaweza kuchomwa au kuchemshwa na likawa chakula kwetu. Mafuta ya mahindi hutumiwa kutengenezea mafuta ya kupikia. Mbali na mahindi, njugu pia hutengenezewa mafuta ya kupaka kwenye mkate. Njugu ni zao la karanga. Njugu hukaangwa na kuliwa. Baadhi ya watu hutwanga njugu na kutengeneza borohoa ya kuungia kitoweo.


Haya ni mananasi. Nanasi ni zao la mnanasi. Nanasi huivishwa na kuliwa. Nanasi hutoa maji matamu yanayomaliza kiu. Maji hayo hutumiwa kutengenezea sharubati au soda.






Hii ni mihogo. Muhogo ni mzizi wa muhogo. Muhogo huweza kuchemshwa au kukaangwa na kuliwa. Muhogo pia huweza kukaushwa, ukasagwa na kutengenezewa sima.

Hizi ni mbatata. Mbatata ni viazi vya mviringo. Viazi hivi havina sukari. Mbatata huweza kupikwa kama kiungo. Pia, huchemshwa na kuliwa na vinywaji au vyakula vinginevyo. Mbatata pia hukatwakatwa kwa vipande vyembamba na kutiwa ndani ya mafuta ili kutengenezea vibanzi au chipsi.









Hivi ni viazi vitamu. Viazi hivi hupandwa katika matuta au sesa. Viazi vitamu huchemshwa na kunywewa kwa chai au kahawa. Viazi vitamu huwa na sukari kiasi cha haja.

## Zoezi

1. Angalia maana ya maneno yaliyokolezwa kwa wino katika kamusi. Tunga sentensi sahihi kwa kila neno.
2. Taja mazao zaidi yanayopatikana nchini Rwanda lakini hayajatajwa katika kifungu. Je, mazao hayo yana faida gani?
3. Tunga sentensi sahihi ukitumia maneno yafuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| a) ndizi | b) mahindi | c) kahawa |
| d) mbatata | e) maharagwe | f) chai |

4. Taja majina ya mazao haya na faida zake.

| | | |
|---|---|---|
| a)  | b)  | c)  |
| d)  | e)  | f)  |

## *Kazi ya wanafunzi wawili wawili*

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Jadilianeni kuhusu majina na faida ya mazao mbalimbali katika maeneo mnakoishi


## *Kazi ya kikundi*


Katika vikundi, kila mwanafunzi ataje mazao yasiyopatikana katika eneo anamoishi. Jadilianeni kuhusu faida za mazao mliyoyataja.

## ii) Msamiati kuhusu shughuli za kilimo nchini Rwanda

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Jadilianeni kuhusu shughuli mbalimbali za kilimo kwenye michoro.

*Mfano*




| | | |
|---|---|---|
| 1.  | 2.  | 3.  |
| 4.  | 5.  | 6.  |
| 7.  | 8.  | 9.  |

***Soma kifungu kilichopo hapa chini na ujibu maswali chini yake.***

HABIMANA: Habari za asubuhi wenzangu?

KAREKEZI na ITUZE: Nzuri sana Habimana.

HABIMANA: Wenzangu, naomba mnieleze maana ya kilimo.

KAREKEZI: Kilimo au zaraa ni kazi ya kulima shamba na kukuza mimea hadi kufikia kiwango cha kuvunwa.

HABIMANA: Wenzangu, naomba mnitajie shughuli hizi za kilimo.

KAREKEZI: Kwanza, kuna kufyeka. Sisi hufyeka shamba letu kwa kutumia upanga na fyekeo. Baadaye, kuna kulima shamba ili kuandaa konde. Katika kijiji chetu, tunatumia jembe la mkono kuandalia konde.

HABIMANA: Kwa nini mnatumia jembe la mkono?

KAREKEZI: Kwa sababu mashamba katika kijiji chetu ni madogomadogo. Vilevile, wakulima katika kijiji chetu hawawezi kumudu mbinu nyinginezo za kulima. Je, Ituze, wakulima katika eneo lenu hutumia mbinu zipi kuandaa mashamba yao?

ITUZE: Wakulima katika eneo letu hutumia plau inayovutwa na ng'ombe au punda. Wakulima katika eneo jirani nao hutumia plau inayovutwa na trekta. Wakulima hao wanamiliki mashamba makubwa. Pia wanaweza kulipia gharama za trekta.
Karekezi, hebu tueleze namna nyingine ya ukulima katika eneo lenu.

KAREKEZI: Sisi hulima sesa. Tunapojiandaa kupanda mbegu, huchanganya mbolea ya samadi na udongo. Udongo wetu hauna rutuba ya kutosha. Baada ya kuweka mbolea, tunapanda mbegu za mahindi na maharagwe ndani ya udongo na kuzifukia. Mbegu zinapoota, tunapalilia miche ili kuondoa magugu au kwekwe. Baadhi ya wakulima huweza kupiga dawa za kuwaua wadudu waharibifu. Wakati wa kiangazi, kuna kunyunyizia mimea maji. Baada ya mimea kukua na kukomaa, tunavuna. Viazi na mihogo yetu ndiyo hutuletea pesa za matumizi nyumbani kwetu. Tunakula baadhi ya mazao hayo na kuyauza mengine.

HABIMANA: Kumbe kazi hii ya kilimo ni nzuri mno! Nilisoma juzi kuwa nchi yetu hupata pesa za kigeni kwa kuuza chai na kahawa katika nchi za kigeni.

ITUZE: Kweli kabisa. Uchumi wa Rwanda umeimarika kwa sababu ya kilimo. Maisha ya wakulima wengi yameimarika pia. Watu wengi wameajiriwa kutokana na kilimo.

HABIMANA: Hata mimi nitaanza kufanya shughuli hizi za kilimo. Tuna shamba dogo lakini lina rutuba nyingi. Nitapanda mboga na njugu. Asanteni kwa kunifunza kuhusu kilimo. Kushauriana katika kazi ya kilimo ni jambo lililo muhimu mno.

KAREKEZI: Pia, tusome kwa bidii hadi chuo kikuu ndipo tuwe wakulima bora zaidi. Tukisoma kwa bidii, tutajifunza na kutumia mbinu za kisasa za kilimo. Mbinu hizi zitatusaidia na kusaidia jamii. Kilimo kitaimarika.

ITUZE: Taibu! Pia tukisoma, tutabuni mbinu mpya za kurahisisha kilimo na kujiongezea mazao. Ni lazima tufanye juu chini kupata elimu na kufanya utafiti zaidi. Asanteni wenzangu.

## Maelezo ya msamiati

kufyeka – kusafisha shamba kwa kukata miti au majani
kulima – kutayarisha shamba kwa kutifua ardhi
konde – sehemu ya shamba iliyolimwa
sesa – ukulima usiokuwa wa matuta katika ardhi tambarare
kuzifukia – kuzificha mbegu ardhini
zinaota – zinachipuka kutoka ardhini
kupalilia – kulima kwa kuondoa magugu katikati ya mimea au miche
kunyunyizia – kumwagilia maji au dawa ya maji
kukua – kuongezeka ukubwa au kimo
kukomaa – kuwa tayari kuvunwa/kutolewa shambani
kuvuna – kutoa mazao shambani

## Maswali

1. Angalia maana ya maneno haya katika kamusi na uyatungie sentensi sahihi.
   a) upanga b) fyekeo c) plau d) trekta e) mbolea
   f) samadi g) udongo h) rutuba i) kwekwe j) mbegu
   k) mche l) pampu
2. Andika manufaa ya kilimo yaliyotajwa kwenye kifungu. Ongezea manufaa matano zaidi.
3. Karekezi na Ndoli hawapendi kilimo. Je, kauli hii ni kweli? Toa sababu zako.
4. Je, masomo ya kilimo yana umuhimu gani?
5. Tumia maneno uliyopewa kutaja shughuli kwenye michoro.
   (kufyeka, kulima, kupanda mbegu, kupalilia, kupiga dawa, kunyunyizia maji, kuvuna)

| 1. | 2. | 3. | 4. |
|---|---|---|---|
|  |  |  |  |

5.



6.




7.



6. a) Taja majina na matumizi ya vifaa vilivyopo hapa chini.

i)



ii)



iii)



iv)



v)



vi)



b) Tunga sentensi sahihi kuhusu kilimo ukitumia jina la kila kifaa hapo juu.

7. Andika maneno kumi ya shughuli na zana za kilimo kutoka kwenye mraba huu. Tunga sentensi sahihi ukitumia kila neno.

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| E | K | U | F | Y | E | K | A |
| D | G | H | Y | D | O | U | G |
| A | T | K | E | R | T | V | N |
| M | K | M | K | A | A | U | A |
| I | O | O | E | F | L | N | P |
| L | B | L | O | P | L | A | U |
| U | O | J | E | M | B | E | K |
| K | A | I | L | I | L | A | P |

## Kazi ya wanafunzi wawili wawili

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Jadilianeni kuhusu shughuli za kilimo katika nchi ya Rwanda na manufaa ya shughuli hizo.

### iii) Msamiati kuhusu shughuli za ufugaji nchini Rwanda

Ufugaji hasa ni kazi ya kutunza wanyama, ndege na hata wadudu. Kazi hii ina faida kubwa sana kama kilivyo kilimo cha mimea. Mfugaji anaweza kufuga wanyama ama wadudu.

## Kazi ya wanafunzi wawili wawili

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Kumbushaneni majina ya mifugo mbalimbali mliyosoma katika kidato cha kwanza na umuhimu wake.


***Tazama michoro iliyopo hapa chini na usome kifungu cha maneno kando yake.***



Huyu ni Ikirezi. Ikirezi ni mfugaji wa nyuki. Ikirezi anarina asali. Baada ya kurina, yeye husafisha asali yake na kuiuza. Asali hiyo hutumiwa kama chakula au hutengenezewa dawa.


Huyu ni Gabiro. Gabiro anakata sufu. Sufu ya kondoo hutumiwa kutengenezea nyuzi za kufumia nguo.





Huyu ni Ituze. Ituze anakama ng'ombe. Kabla ya kukama, aliosha chuchu kwa maji vuguvugu na kuzikausha kwa kitambaa safi. Anatumia mkebe safi kuwekea maziwa. Ituze huwapandisha mitamba kwa dume au mpira.

Hili ni josho. Ng'ombe hawa wanaogeshwa kwa dawa ndani ya josho. Wafugaji huosha mifugo katika josho ili kuikinga dhidi ya kupe. Dawa huua viroboto wanaoishi kwenye ngozi za mifugo.





Hawa ni Mudenge na Gatera. Mudenge anawalisha kuku kwa mahindi. Pia, huwapa kuku mtama, ugali, wadudu na vyakula vinavyopatikana kwa urahisi. Wakati mwingine, yeye huwapa kuku chakula maalumu kilichotengenezwa katika viwanda. Mudenge anawafuga kuku wa mayai na nyama. Yeye huuza baadhi ya mayai ili kujipatia riziki. Mudenge pia huwaatamisha baadhi ya kuku wake ili apate vifaranga wa kuuza na kufuga. Gatera naye anawalisha ng'ombe kwa nyasi. Gatera anawafuga ng'ombe wake ndani kwa ndani. Anawapa lishe, maji na dawa humohumo zizini. Gatera hukata pembe za ng'ombe wake. Ng'ombe hukatwa pembe ili kumzuia kumdhuru mtu au kuharibu vitu.

Huyu ni Kaliza. Kaliza anapenda kuchunga punda. Anawachunga punda penye maji safi na nyasi nyingi. Kulisha mifugo ni shughuli muhimu ya ufugaji. Mifugo wanapolishwa vizuri hukua kwa haraka, huwa na afya nzuri na hutupatia mapato mazuri.





Kaliza anafagia zizi la ng'ombe. Mkulima bora husafisha makao ya mifugo na vyombo vyao vya kulia na kulalia. Mifugo wanaolala katika mahali safi na kula katika vyombo safi huwa na afya njema.

Daktari wa mifugo anamtibu kuku kwa kumdunga sindano. Kutibu mifugo ni muhimu kwa mkulima. Ni vizuri kutambua dalili ya ugonjwa ili watibiwe mapema.



## Msamiati

kurina – kufukuza nyuki kutoka kwenye mzinga na kukata masega ili kupakua asali.

kukata sufu – kunyoa manyoya ya kondoo kutoka kwenye ngozi yake

kukama – kuminya chuchu za mnyama kama vile ng'ombe ili maziwa yatoke

kupandisha mtamba – kumpa ng'ombe wa kike mbegu za kiume ili kuzalisha ndama

kufuga ng'ombe ndani kwa ndani – kufuga ng'ombe ndani ya eneo au jengo fulani na kuwapa mahitaji yote humo bila kuwatoa nje

kuwapeleka ng'ombe katika josho – kuwapelekea ng'ombe katika dimbwi maalumu lililotiwa dawa ya kuulia kupe

kuatamisha kuku – kumfanya kuku kulalia mayai



kuchunga – kuwapeleka wanyama malishoni na kuwalinda wasiibwe

kukata pembe – kutoa pembe kwa kutumia kisu au chuma moto

kulisha – kupea chakula na maji

## Maswali

1. Andika majina yote ya mifugo waliotajwa katika ufahamu hapo juu. Taja umuhimu wao.
2. Eleza faida za shughuli za ufugaji ulizosoma katika kifungu.
3. Jaza mapengo haya kwa shughuli sahihi ya ufugaji.

| | | |
|---|---|---|
| a)  Ikirezi ana ____asali. | b)  Gabiro ana__________. | c)  Ituze ana _______. |
| d)  Ng'ombe__________ katika josho. | e)  Mudenge ana ______. | f)  Kaliza ana _________ punda. |

| g) | h) |
|---|---|
|  Kaliza ___________. |  Daktari_________. |

4. Tunga sentensi sahihi ukitumia maneno hapo chini.
   a) rina asali
   b) chunga
   c) kata pembe
   d) kama
   e) lisha
   f) fagia zizi
   g) tibu ng'ombe
   h) pandisha mtamba
   i) atamisha

## *Kazi ya wanafunzi wawili wawili*


Jiunge na mwanafunzi mwenzako na mfanyeni zoezi hili:
1) Kwa pamoja, andikeni shughuli mbalimbali za ufugaji na mifugo nchini Rwanda katika karatasi.
2) Kunjeni karatasi hizo na kuziweka pamoja.
3) Kila mwanafunzi achukue karatasi moja kwa zamu, asome shughuli ya ufugaji au mifugo katika karatasi aliyochukua na atunge sentensi sahihi kwa kutumia neno katika karatasi yake. Atakayekosea asahihishwe.

## *Kazi ya kikundi*

Kama darasa zima, fanyeni mjadala kuhusu: Njia za kisasa za ufugaji zinaleta mapato makubwa zaidi kuliko njia za kienyeji.

## B Majira ya mwaka nchini Rwanda

***Tazama michoro iliyopo hapa chini. Je, nini kinafanyika?***

| 1. | 2. | 3. |
|---|---|---|
|  |  |  |

***Soma kifungu hiki na ujibu maswali yaliyoulizwa chini yake.***

Majira ni kipindi maalumu cha hali ya hewa. Majira haya ndiyo huelekeza upanzi wa mimea na uvunaji wa mazao hapa kwetu.

Tupo na majira mbalimbali. Yapo majira ya mvua nyingi. Majira ya mvua nyingi ya mfululizo huitwa masika. Majira haya hutokea kuanzia mwezi wa Machi hadi Mei kila mwaka. Shughuli za kupanda mimea kama vile maharage, mtama, mbatata, mahindi, na kadhalika hutokea mwanzoni mwa majira ya masika. Mimea hiyo huota na kupaliliwa katika majira haya ya masika.

Vilevile, mimea mbalimbali kama vile mikahawa, mipareto, migomba, minanasi na kadhalika hustawishwa mnamo majira haya.

Msimu huu wa masika hufuatwa na majira ya kiangazi au ukame. Huu ni wakati ambapo jua kali huwaka, mvua hukosa kunyesha na ardhi hukauka. Yapo majira mafupi ya kiangazi ambayo hutokea kuanzia Juni hadi Septemba. Mifugo na mimea hukosa chakula na maji ya kutosha na huanza kuwa na afya mbaya mnamo majira haya. Baadhi ya wakulima huanza kuvuna mazao yao katika majira ya kiangazi. Wengine hulima na kuandaa makonde yao mnamo majira haya kabla ya mvua kuanza kunyesha.

Mbali na majira haya, yapo majira ya vuli. Huu ni wakati ambapo huwepo mvua ndogo ndogo tu. Majira haya hutokea kati ya mwezi wa Novemba na Februari. Wakati wa vuli, wakulima hupanda vyakula vinavyochukua muda mfupi kukua na kukomaa. Hata hivyo, shughuli nyingi za upanzi hazifanyiki kwa kuwa mvua inyeshayo huwa haitoshi kukuza baadhi ya mimea.

Hali kadhalika, yapo majira ya kipupwe. Kipupwe ni majira ya baridi ambayo hutokea katika miezi ya Septemba na Novemba nchini Rwanda. Wakati huu wa mwaka huwepo baridi kali na hubidi watu kuvaa sweta, makoti na hata makabuti.

Kwa ufupi, wakulima wengi nchini Rwanda huzingatia majira mbalimbali wanapofanya shughuli zao za kilimo. Wao hutegemea mvua na jua katika kukuza mimea.

## Msamiati

masika – majira ya mvua nyingi ya mfululizo
kiangazi/ukame – majira ya jua kali
vuli – majira ya mvua ndogo ndogo
kipupwe – majira ya baridi kali

## Maswali

1. Taja miezi na majira ambapo shughuli hizi za kilimo hufanywa hapa kwetu Rwanda.
    a) kulima shamba kavu
    b) kuandaa konde lenye unyevunyevu
    c) kupanda mimea mingi

d) kupalilia
e) kustawisha mimea
f) kuvuna
g) kupanda mimea michache inayokua na kukomaa haraka

2. Ipo tofauti gani kati ya vuli na kipupwe?
3. Tazama mraba ufuatao na uandike maneno manne ya majira.

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| W | E | K | V | D | D | F | E |
| D | M | I | R | T | P | W | W |
| J | M | A | S | I | K | A | P |
| O | O | N | M | L | F | K | U |
| L | A | G | B | U | H | J | P |
| E | D | A | E | V | R | L | I |
| S | Y | Z | U | M | T | A | K |
| Z | N | I | I | N | P | E | P |

## *Kazi ya wanafunzi wawili wawili*

Jiunge na mwenzako. Chunguzeni michoro ifuatayo na mjaze mapengo kando yake.

| Majira | Miezi ya majira | Shughuli za kilimo katika majira hayo |
|---|---|---|
| a  | | |
| b  | | |
| c  | | |

| | | |
|---|---|---|
| d  | | |
| e  | | |

## C Msamiati wa msingi kuhusu wanyama wa porini na umuhimu wake

### i) Msamiati wa wanyama wa porini nchini Rwanda

***Tazama wanyama hawa. Je, hawa ni wanyama gani? Wanyama hawa wanapatikani katika mbuga na sehemu ipi ya Rwanda?***

*Kisome kifungu kifuatacho ili kujifunza msamiati wa wanyama wa porini.*

Mnyama wa porini ni mnyama anayeishi katika pori. Pori ni mahali penye miti na nyasi nyingi. Mnyama wa porini hafugwi na binadamu. Wanyama wengi wa porini hupatikana katika mbuga za wanyama. Mbuga za wanyama ni sehemu zilizotengwa na serikali kuwa ndio makazi ya wanyama hao wa porini. Je, unafahamu mbuga gani za wanyama nchini Rwanda?



Nchi ya Rwanda ina wanyama wengi wa porini. Nchi yetu ya Rwanda inasifika sana kutokana na masokwe. Sokwe ni mnyama mkubwa zaidi katika jamii ya nyani. Mnyama huyu hana mkia. Sokwe ana akili nzuri inayokaribiana na ile ya binadamu. Wana uwezo wa kumwiga binadamu. Nchi yetu inajulikana sana kutokana na masokwe. Masokwe hawa wanapatikana katika mbuga zetu za wanyama. Masokwe wengi wanapatikana katika Mbuga ya Wanyama ya Volcanoes (Volkano).



Nyani ni mnyama wa jamii ya sokwe na tumbiri. Nyani ni mdogo kuliko sokwe lakini ana akili nyingi zaidi. Ana masikio makubwa nao mwili wake una rangi ya kaki ya kijivu na ngoko nyekundu makalioni. Nyani huishi katika vikundi vya majike na madume. Wana uwezo wa kuishi kwa miaka zaidi ya arubaini.

Pia kuna tumbiri porini. Tumbiri ni mnyama mdogo zaidi katika jamii ya nyani. Tumbiri hupenda sana kukaa mitini. Hula vyakula mbalimbali kama vile matunda, mazao ya mimea mbalimbali na kadhalika.





Simba ni mnyama mkubwa wa jamii ya paka. Simba hula nyama. Anaitwa mfalme wa wanyama au nyika. Simba huishi kwenye vikundi. Vikundi hivyo huongozwa na simba dume.

Ndovu ndiye mnyama mkubwa zaidi wa porini. Ndovu ana mkonga pamoja na pembe mbili kubwa zenye thamani. Ndovu wana masikio makubwa na miguu mifupi minene. Ndovu hula nyasi, mizizi, matunda na mashina ya miti. Pia, huishi katika vikundi. Kila kikundi huongozwa na ndovu jike ambaye ana umri mkubwa zaidi kuliko wote. Uwindaji wa ndovu na kuuza pembe zake ni hatia. Sisi sote tunafaa kuwatunza ndovu na wanyama wote wa porini.





Chui pia hupatikana katika mbuga zetu. Chui ni mnyama wa jamii ya paka lakini aliye mkubwa na mkali na mwenye madoadoa ya manjano na meusi. Chui hula wanyama wadogo wadogo wanaoishi porini. Baada ya kuwinda, wao huficha nyama kwenye matawi ya mti. Wao hupenda sana kutembea na kuwinda wakati wa usiku na kupumzika wakati wa mchana.



Pundamilia pia ni mnyama wa porini wa jamii ya farasi. Ana milia myeusi na myeupe katika mwili mzima. Inaaminika kuwa milia hiyo huwawezesha kujificha nyikani ili wasionekana na wanyama wanaowawinda. Pundamilia hutembea na kula nyasi katika vikundi vikubwa.

Twiga naye ana shingo ndefu, rangi ya kahawia na madoadoa meusi. Twiga ndiye mnyama mrefu zaidi. Yeye hula majani ya miti.





Kifaru pia hupatikana katika mbuga zetu. Ni mnyama mkubwa afananaye na kiboko na mwenye kipusa usoni.

Nyati pia ni mnyama mkubwa sana. Hufanana na ng'ombe. Pembe zake zimepinda kwa mbele. Nyati hula nyasi. Wao pia huishi katika vikundi kutegemea jinsia. Nyati pia huitwa mbogo.





Swara ni mnyama mdogo anayefanana na mbuzi. Swara anaweza kukimbia haraka. Yeye hula nyasi.

Wanyama hawa wa porini hupatikana katika mbuga zetu kama vile Akagera, Nyungwe na Volcanoes. Wanyama hawa ni vivutio vikubwa vya watalii wanaotoka ndani na nje ya nchi yetu.

## Maswali


1. Andika orodha ya majina ya wanyama wa porini wanaokula:
   a) nyama
   b) nyasi
2. Eleza tofauti zilizopo kati ya sokwe na nyani.
3. Jaza kila pengo kwa jina sahihi la mnyama wa porini.
   a) Mwenye tamaa kama_______________.
   b) __________ ana mkonga na pembe mbili.
   c) ________ haoni kundule.
   d) Ndovu pia huitwa______________.
   e) Nimemwona mnyama mwenye milia myeusi na myeupe mwilini.
   Nimemwona___________.


4. Tunga sentensi sahihi ukitumia majina haya ya wanyama wa porini.
   a) pundamilia  b) simba  c) tumbiri
   d) swara  e) nyati  f) ndovu
5. Taja majina ya wanyama hawa:

a 

b 

c 

d 

e 

6. Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Fanyeni utafiti kuhusu majina na sifa za wanyama wa porini wanaopatikana ndani na nje ya Rwanda na ambao hawajatajwa katika ufahamu.

## ii) Umuhimu wa wanyama wa porini nchini Rwanda

Kufikia sasa, umesoma mengi kuhusu wanyama wa porini. Wanyama hao wana umuhimu mbalimbali.

***Tazama mchoro huu na usome kifungu chini yake*.**



KANYANA: Karibuni katika mbuga yetu ya Volcanoes.

UWASE na HIRWA: Asante.

KANYANA: Hapa, mtaona wanyama wengi wa porini.

UWASE: Wanyama hao wana umuhimu gani?

NGABO: Wanyama hao wana umuhimu mkubwa sana kwa nchi hii yetu ya Rwanda. Wanyama hao kama vile masokwe ni vitega uchumi. Kila mwaka, watalii kutoka nchi za mbali huja hapa kwetu kuwaona wanyama. Wajapo hivyo, huja na pesa za kigeni ambazo huinua sana uchumi wetu.

KANYANA: Nyinyi pia ni watalii wetu hapa. Pesa mnazolipa mkiingia hujenga uchumi wetu. Pesa hizo pia hutumiwa kutulipia mshahara. Mimi na wenzangu tumeajiriwa kwa sababu ya wanyama wa porini.

HIRWA: Je, nchi yetu hunufaika na pesa za kiingilio peke yake?

NGABO: Hapana. Wageni wanapokuja, wanaleta manufaa mengi zaidi. Wao hulipia huduma mbalimbali. Kwanza kuna malazi yao. Sisi huwakaribisha katika hoteli kubwa kubwa na nzuri nzuri. Hoteli hizo zimepanuka na kuwaajiri watu wengi kwa sababu ya wageni hao wanaokuja kuangalia wanyama wa porini. Wageni hao pia hulipia usafiri wao uwe ni wa ndege au gari. Usafiri huo huwapeleka huko wanakopenda kwenda kuwaona wanyama.

KANYANA: Mbali na hayo, zipo bidhaa nyingi sana za hapa ambazo watalii hao hununua kuwa ni ushahidi kwao kwamba kweli walikuwa hapa. Kwa njia hiyo pia nchi hufaidika kiuchumi.

UWASE: Mbali na faida hizo za kifedha, zipo faida gani tena za wanyama hawa?

NGABO: Wanyama hawa hukuza elimu yetu. Wanafunzi, na hata watu wazima huzuru mbuga zetu za wanyama ili kuwaona na kujifunza mengi kuwahusu.

KANYANA: Isitoshe, wanyama wa porini ni hazina kwa vizazi vyetu vya baadaye. Sisi sote tumewaona wanyama hawa. Vivyo hivyo, litakuwa jambo zuri sana ikiwa wanetu, wajukuu, watukuu, vilembwe na hata vilembwekeza wetu kuwaona wanyama wa porini pia. Hii ndiyo sababu ya serikali yetu kuwatunza na kuwalinda wanyama wa porini.

UWASE na HIRWA: Asanteni kwa maelezo yenu.

## Maswali

1. Taja faida za wanyama wa porini.
2. Taja njia mbili ambazo serikali hutumia kuhifadhia wanyama wa porini.

**Kazi ya kikundi**

Jiunge na wanafunzi wenzako. Jadilianeni kuhusu umuhimu wa wanyama wa porini nchini Rwanda.

## D Matini ya Kiswahili kuhusu kilimo na ufugaji pamoja na vipengele vya kisarufi

### Nomino

Je, unakumbuka maana na aina za nomino ulizosoma katika kidato cha kwanza? Zitaje.

Nomino ni neno linalotaja mtu, kitu, hali au jambo. Zipo aina mbalimbali za nomino. Zifuatazo ni baadhi ya nomino hizo.

***a) Nomino za pekee***

Nomino za pekee hutaja vitu au watu wenye sifa za kipekee. Zinapoandikwa katika sentensi, lazima zianze kwa herufi kubwa hata zikiwa katikati au mwishoni mwa sentensi. Kumbuka hapa ya kuwa majina haya hayachukui hali ya wingi.

*Mifano*

i) *Majina ya watu*: Ndoli, Abatoni, Ituze.
ii) *Majina ya Mungu*: Mola, Maulana, Rabuka na kadhalika.
iii) *Majina ya mataifa/nchi*: Rwanda, Kenya, Uganda, Marekani
iv) *Majina ya masomo*: Kilimo, Hisabati
v) *Majina ya mji*: Kigali, Nairobi
vi) *Majina ya mlima*: Mlima Virunga
vii) *Majina ya mto*: Mto Akagera

***Mifano ya nomino za pekee katika sentensi.***

i) Rwanda ni nchi yenye wanyama wengi wa porini.
ii) Mukangango ananyoa sufu ya kondoo.
iii) Mwenyezi Mungu atujalie mvua nyingi ili tulime.
iv) Kigali ni jiji linalopendeza.

**Zoezi**

a) Andika sentensi sahihi ukitumia nomino hizi za pekee:
   i) Munyana  ii) Kamana  iii) Mola
   iv) Mei  v) Mto Kivu  vi) Msitu wa Nyungwe
b) Tambua makosa katika sentensi hizi na uyarekebishe.
   i) Mimi na kayitesi tunapenda somo la kilimo.
   ii) Nitavuna mihogo yangu mwezi wa februari.
   iii) Ng'ombe anaitwaje kwa kinyarwanda?

### *b) Nomino za kawaida*

Nomino za kawaida hutaja vitu vya kawaida vinavyoweza kuchukua umoja na wingi kama jina lolote lile. Nomino hizo zinapoandikwa, huchukua herufi ndogo isipokuwa pale zinapojitokeza mwanzoni mwa sentensi.

***Mifano ya nomino za kawaida:***

*i) Nomino za viumbe wenye uhai:*

| **umoja** | **wingi** |
|---|---|
| mtu | watu |
| ng'ombe | ng'ombe |
| kondoo | kondoo |
| ngamia | ngamia |
| kifaranga | vifaranga |

*ii) Nomino zinazomtambulisha mtu na kazi yake:*

| **umoja** | **wingi** |
|---|---|
| mkulima | wakulima |
| mwuuzaji | wauzaji |
| mfugaji | wafugaji |

*iii) Nomino za vitu vya kawaida*

| **umoja** | **wingi** |
|---|---|
| shamba | mashamba |
| jembe | majembe |
| mbuga | mbuga |
| pori | mapori |
| zizi | mazizi |
| sufu | sufu |
| hindi | mahindi |
| haragwe | maharagwe |

*iv) Nomino za mahali: shambani, uwanjani, mbugani, zizini, porini*

Kumbuka hapa kuwa nomino hizi za mahali huundwa kwa kuongeza 'ni' mwishoni mwa nomino husika.

*Mifano ya matumizi ya nomino za kawaida katika sentensi.*

i) Mavuno ya mwaka huu ni mazuri.
ii) Niletee jembe hilo.
iii) Sufu za kondoo hutumiwa kutengenezea sweta.
iv) Mkulima hodari hupata mazao mengi.
v) Ndovu ni mnyama mkubwa wa porini.

**Zoezi**

Tunga sentensi kumi sahihi ukitumia nomino za kawaida.

### c) Nomino za jamii

Nomino za jamii pia huitwa nomino za makundi. Hizi ni nomino ambazo hutaja jumla ya vitu vingi au vitu katika makundi.

***Mifano ya nomino za jamii:***

| umoja | wingi |
|---|---|
| tita | matita |
| tuta | matuta |
| koja | makoja |
| kole | makole |

*Mifano katika sentensi*

i) Makole ya ndizi yamevunwa.
ii) Matuta yamepigwa shambani.
iii) Matita ya kuni yatatumika kuchomea nyama.
iv) Mitumba ya aina hii haifai wakulima.
v) Bunge letu limetenga pesa nyingi kwa wizara ya kilimo.
vi) Baraza la wafuga farasi limevunjwa.
vii) Hili ni robota la pamba.

**Zoezi**

Fanya utafiti kupata nomino kumi zaidi za jamii. Tunga sentensi ukitumia kila nomino hizo katika umoja na wingi.

### d) Nomino za dhahania

Katika kikundi hiki hupatikana nomino ambazo ni za kufikirika tu na wala haziwezi kuguswa. Chukua nomino kama urafiki. Urafiki ni neno la kufikirika au kudhaniwa tu na wala haliwezi kuonekana wala kushikika. Nomino hizi haziwezi pia kuhesabika.

*Mfano*

ukulima, njaa, shibe, uvunaji, upanzi.

***Mifano katika sentensi***

i) Upanzi hufanywa mvua inapoanza kunyesha.
ii) Kilimo kinasaidia kumaliza umaskini nchini Rwanda.
iii) Ushirikiano wao katika kupalilia unawafaidi.
iv) Fikira za wafugaji hao ni za hekima.
v) Tutafanya uvunaji mwezi ujao.

**Zoezi**

Tunga sentensi zozote kumi kuhusu kilimo na ufugaji ukitumia nomino za jamii.

***e) Nomino za wingi***

Hizi nazo ni nomino za vitu ambavyo daima hupatikana kwa wingi pekee au umoja pekee. Vitu vinavyotajwa na nomino hizi haviwezi kugawika.

*Mifano ya nomino za wingi:*

maziwa, sukari, chumvi, uji, chai, manukato, mvua na kadhalika.

*Mifano katika sentensi:*

i) Sukari ni zao la miwa.
ii) Maua yale hutumiwa kutengenezea manukato.
iii) Chai hii ni tamu.
iv) Maji yanyunyiziwayo hapa ni ya mto huo.

**Zoezi**

*Soma kifungu kilichopo hapa chini. Tambua na uanishe nomino mbalimbali kifunguni.*

Hapa nchini Rwanda, Mwenyezi Mungu ametujalia mazingira mazuri yenye kufanikisha ufugaji. Ufugaji ni kazi ya kutunza wanyama, ndege na hata wadudu. Mfugaji anaweza kufuga wanyama ama wadudu. Ikiwa ni wanyama, anaweza kutunza ng'ombe, mbuzi, kondoo, farasi, nguruwe, na kadhalika. Ikiwa nia yake ni kufuga ndege, anaweza kuwatunza kuku, bata na kadhalika. Hata hivyo, akichagua wadudu huweza kuwafuga nyuki.

Ufugaji una kazi nyingi sana. Kwa mfano, mfugaji wa ng'ombe anapotaka matokeo ya kuridhisha, itambidi atumie njia za kisasa katika ufugaji wake. Kwanza kabisa, ni lazima awatafute ng'ombe bora wa maziwa. Ng'ombe hawa huleta mapato ya juu. Mbali na hayo ni sharti ahakikishe kwamba wanyama wake wana lishe ya kutosha hasa kwa ng'ombe wanaokaa ndani kwa ndani. Ng'ombe hawa, hasa ng'ombe jike, wa kukaa ndani kwa ndani hulishiwa zizini na kulala humo humo zizini. Hata hivyo, ni lazima zizi hilo liwe safi na ng'ombe huyo alale pahali safi. Kukosa kufanya hivyo ni kukaribisha magonjwa ya namna kwa namna.

Iwapo mfugaji atawalisha wanyama wake vizuri, atafaidika pakubwa. Ataweza kupata maziwa ya kutosha. Atauza maziwa hayo na kujinunulia bidhaa nyinginezo kama vile chumvi, sukari, chane za ndizi na kadhalika. Umaskini pia utaisha.

## Vivumishi

Je, unakumbuka vivumishi mbalimbali mlivyosoma katika kidato cha kwanza? Kwa kawaida, kivumishi ni neno linaloongezea nomino maana. Zipo aina mbalimbali za vivumishi. Baadhi ya vivumishi hivyo ni:

#### a) *Vivumishi vya sifa*

Haya ni maneno yatajayo tabia au sifa za kitu, mtu ama jambo.
Zipo aina mbili za vivumishi vya sifa: vivumishi vya sifa vinavyochukua viambishi na vivumishi vya sifa visivyochukua viambishi.

*Mifano ya vivumishi vya sifa vinavyochukua viambishi:*

| | |
|---|---|
| -aminifu | -zuri |
| -pana | -kubwa |
| -pya | -dogo |
| -bovu | -fupi |

Kumbuka kuwa kiambishi au viambishi vinavyochukuliwa na vivumishi hivi hutegemea ngeli.

*Mifano katika sentensi:*

| umoja | wingi |
|---|---|
| i) Twiga ni mnyama mrefu. | Twiga ni wanyama warefu. |
| ii) Mkulima mvumilivu hufanikiwa. | Wakulima wavumilivu hufanikiwa. |
| iii) Shamba zuri hutoa mavuno mengi. | Mashamba mazuri hutoa mavuno mengi. |
| iv) Ndizi ile mbivu ni tamu. | Ndizi zile mbivu ni tamu |
| v) Kupalilia kubaya hakuondoi gugu. | Kupalilia kubaya hakuondoi magugu. |

#### ii) *Vivumishi vya sifa visivyochukua viambishi*

Hivi ni vivumishi ambavyo havibadiliki katika umoja na wingi au kutoka ngeli moja hadi nyingine; hubakia jinsi vilivyo.
Mifano: bora, safi, hodari, bandia, haba, duni, laini na kadhalika.

*Mfano katika sentensi.*

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| i) Mfugaji hodari ana kuku wengi. | Wafugaji hodari wana kuku wengi. |
| ii) Jembe safi halizeeki haraka. | Majembe safi hayazeeki haraka. |
| iii) Usiniuzie unga wa ngano kwa bei ghali. | Msituuzie unga wa ngano kwa bei ghali. |

**Zoezi**

a) Tunga sentensi sahihi kuhusu kilimo na ufugaji katika umoja na wingi ukitumia vivumishi hivi vya sifa.
   i) -baya   ii) -fupi   iii) -dogo
   iv) -ingi   v) -chache

b) Tunga sentensi sahihi ukitumia vivumishi hivi katika umoja na wingi.
   i) bora ii) dhalimu iii) duni
   iv) tele v) laini

c) Andika sentensi hizi katika umoja au wingi.
   i) Nipe ndizi chache.
   ii) Mhindi mrefu unafaa.
   iii) Farasi wakubwa watatubeba.
   iv) Zizi safi halileti magonjwa.
   v) Upanzi bora ni huu.
   vi) Mkulima nadhifu anapita.

d) Tunga sentensi zozote kumi kuhusu wanyama wa porini na kilimo zenye vivumishi vya sifa katika umoja na wingi.

### b) Vivumishi vya pekee

Vivumishi vya pekee hutoa habari kuhusu nomino au kiwakilishi chake kwa njia ya kipekee. Vivumishi vya peke ni sita katika Kiswahili kama ifuatavyo:

#### i) -enye

Huonyesha hali ya 'kuwa na' au 'kumiliki.' Ni sharti kivumishi hiki kifuatwe na nomino wala si kitenzi.

**Mifano**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| i) Mkulima mwenye panga anafyeka. | Wakulima wenye mapanga wanafyeka. |
| ii) Mgomba wenye ndizi utakatwa. | Migomba yenye ndizi itakatwa. |
| iii) Shamba lenye rutuba linalimwa. | Mashamba yenye rutuba yanalimwa. |

#### ii) -enyewe

a) Hutumika mwanzoni mwa sentensi kuonyesha jambo au kitu kinachotarajiwa.

**Mifano**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| i) Kondoo mwenyewe atachinjwa. | Kondoo wenyewe watachinjwa. |
| ii) Nanasi lenyewe ni tamu. | Mananasi yenyewe ni matamu. |
| iii) Ngozi yenyewe ni ya ng'ombe. | Ngozi zenyewe ni za ng'ombe. |

b) Hutumika mwishoni mwa sentensi kuonyesha kuwa jambo limetokea bila kusababishwa na yeyote au chochote.

***Mifano***

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| i) | Ng'ombe amejifungua mwenyewe. | Ng'ombe wamejifungua wenyewe. |
| ii) | Mkulima amelima mwenyewe. | Wakulima wamelima wenyewe. |
| iii) | Mbegu imemea yenyewe. | Mbegu zimemea zenyewe. |

***iii) -ote***

Huleta maana mbili:

a) Kuonyesha kila sehemu ya kitu hasa katika umoja.

***Mfano***

Shamba **lote** limelimwa. Maana yake ni kila sehemu ya shamba imelimwa.

b) Kuonyesha kila kitu; bila kubakisha lolote hasa katika wingi.

***Mfano***

Mashamba yote yamelimwa. Maana yake ni kila shamba limelimwa.

**Zoezi**

Eleza maana ya sentensi ikiwa ni 'kila sehemu' au 'kila kitu'.

i) Zizi lote limefagiliwa.
ii) Mazao yote yamevunwa.
iii) Paka amekunywa maziwa yote.
iv) Ndizi yote imeiva.
v) Simba wote wamepita.

***iv) -o-ote***

Huonyesha mojawapo ya vitu au baadhi ya vitu bila kubagua.

***Mifano***

1. Mihogo yoyote itakayokomaa itavunwa.
2. Nipe embe lolote.
3. Mkulima yeyote atapewa zawadi.

**Zoezi**

Tumia '-ote' au '-o-ote' pamoja na viambishi sahihi vya ngeli kujazia pengo katika sentensi zifuatazo.

1. Nitatumia jembe _____ nitakalopewa.
2. Miharagwe _________ imemea.
3. Kuku ______ wamepewa chakula.
4. Sitachukua nanasi ____________.
5. Fyeka nyasi____________.

***v) -ingine***

Kivumishi hiki cha pekee huweza kuwa na maana tatu:

a) Kuonyesha kitu tofauti na kile kilichotajwa au kilichopo.

***Mifano***

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| i) | Sikuuzii farasi huyu, nitakuuzia farasi mwingine. | Hatuwauzii farasi hawa, tutawauzia farasi wengine. |
| ii) | Usinyunyizie mmea huu maji, nyunyizia mmea mwingine. | Msinyunyizie mimea hii maji, nyunyizieni mimea mingine. |
| ii) | Asile pera hili, ale pera lingine/ jingine. | Wasile mapera haya, wale mapera mengine. |

b) Kuonyesha kitu zaidi/nyongeza

***Mfano***

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| i) | Tafadhali, nionyeshe ndovu mwingine. | Tafadhali, tuonyeshe ndovu wengine. |
| ii) | Panda mbegu nyingine. | Pandeni mbegu nyingine. |
| iii) | Niletee muhogo mwingine. | Tuletee mihogo mingine. |

c) Kuonyesha ‘baadhi ya’

***Mfano***

1) Mahindi mengine yamekauka. (Baadhi ya mahindi yamekauka.)
2) Wafugaji wengine wanafuga punda. (Baadhi ya wafugaji wanafuga punda.)
3) Nyasi zingine hazijaondolewa shambani. (Baadhi ya nyasi hazijaondolewa shambani.)
4) Mauzo mengine ya masoko ya nje hutajirisha. (Baadhi ya mauzo hutajirisha.)

***vi) -ingineo***

Kivumishi hiki hutumika kuleta maana mbili:

a) 'zaidi ya'

***Mfano***

1. Nipe jembe hilo na linginelo.
2. Walishe punda hao na wengineo.
3. Panda mbegu hiyo na nyinginezo.

b) Kuonyesha hitimisho ya orodha ambayo haikukamilika.

***Mifano***

1. Tuliwaona wanyama kama vile ndovu, twiga, swara, masokwe na wengineo.
2. Mkulima amepanda mimea kama vile mihindi, miharagwe, mikahawa na mingineyo.
3. Mavuno hayo ni mahindi, mtama, ndizi na mengineyo.

**Zoezi**

a) Tumia '-ingine' au '-ingineo' pamoja na viambishi sahihi vya ngeli kujazia mapengo.
   i. Amevuna mananasi ____________.
   ii. Sitaki panga hili, nipe panga _____________.
   iii. Mama amepanda mbegu za maharagwe, mtama, mahindi na _____________.
   iv. Usiwakame ng'ombe __________. Maziwa haya yametosha.
   v. Mpe migomba hiyo na ______________.

b) Tunga sentensi tano sahihi kuhusu kilimo na ufugaji katika umoja na wingi ukitumia nomino zozote na kivumishi cha '-ingine'.

c) Tunga sentensi tano sahihi kuhusu wanyama wa porini na mifugo katika umoja na wingi ukitumia nomino zozote na kivumishi cha '-ingineo'.

### *c) Vivumishi vionyeshi*

Vivumishi vionyeshi au viashiria ni maneno ya kuonyesha alipo mtu au kitu, yaani ujirani. Kuonyesha huko kunaweza kuwa kwa ujirani wa karibu – *hapa*, ujirani wa mbali kidogo – *hapo*, na ujirani wa mbali – *pale*.

*Mifano ya vivumishi hivi ni hii ifuatayo:*

| **Nomino** | **Vivumishi viashiria** | | |
|---|---|---|---|
| | **Vya karibu** | **Vya mbali kidogo** | **Vya mbali** |
| kondoo | ***umoja***: Kondoo ***huyu***<br>***wingi***: Kondoo ***hawa*** | ***umoja***: Kondoo ***huyo***<br>***wingi***: Kondoo ***hao*** | ***umoja***: Kondoo ***yule***<br>***wingi***: Kondoo ***wale*** |
| zao | ***umoja***: Zao ***hili***<br>***wingi***: Mazao ***haya*** | ***umoja***: Zao ***hilo***<br>***wingi***: Mazao ***hayo*** | ***umoja***: Zao ***lile***<br>***wingi***: Mazao ***yale*** |
| mhogo | ***umoja***: Muhogo ***huu***<br>***wingi***: Mihogo ***hii*** | ***umoja***: Muhogo ***huo***<br>***wingi***: Mihogo ***hiyo*** | ***umoja***: Muhogo ***ule***<br>***wingi***: Mihogo ***ile*** |

*Mfano katika sentensi:*

i) Kijijini humu mna mfugaji hodari.
ii) Hizi juhudi zenu za kulima zitamaliza umaskini.
iii) Ng'ombe wale wanakunywa maji.
iv) Fyekeo hilo halikati majani.
v) Shambani pale pamepaliliwa.

### *i) Vivumishi vionyeshi radidi*

Vivumishi hivi hutokana na kurudia vivumishi vionyeshi. Huleta maana ya kutilia mkazo.

*Mifano*

| umoja | wingi |
|---|---|
| 1. Ng'ombe huyu huyu atakamuliwa. | Ng'ombe hawa hawa watakamuliwa. |
| 2. Embe lile lile halifai. | Maembe yale yale hayafai. |
| 3. Mkahawa huo huo utang'olewa. | Mikahawa hiyo hiyo itang'olewa. |

### *ii) Vivumishi vionyeshi visisitizi*

Hutumiwa kusisitiza jambo.

*Mifano*

| umoja | wingi |
|---|---|
| 1. Shamba lili hili ni la miwa. | Mashamba yaya haya ni ya miwa. |
| 2. Swara yuyo huyo ana mbio. | Swara wao hao wana mbio. |
| 3. Mharagwe ule ule utapaliliwa. | Miharagwe ile ile itapaliliwa. |

**Zoezi**

a) Jaza kila pengo kwa vivumishi sahihi vilivyowekwa katika mabano.
   i. Mazao __________ yatajaza guni. (vionyeshi visisitizi vya karibu)
   ii. Mkulima __________ analima. (vionyeshi vya mbali)
   iii. Twiga __________ ni wengi. (vionyeshi viradidi vya mbali kidogo)
   iv. Nyama __________ ni tamu. (vionyeshi vya karibu)
   v. Wafugaji __________ wana bidii. (vionyeshi vya mbali kidogo)

b) Tunga sentensi tano tano kuhusu kilimo na ufugaji katika umoja na wingi ukitumia vivumishi vionyeshi, vivumishi vionyeshi rejeshi na vivumishi vionyeshi visisitizi.

### *d) Vivumishi vya idadi*

Vivumishi vya idadi ni maneno yanayoonyesha idadi ya watu ama vitu. Vipo vivumishi vya idadi kamili, vivumishi vya idadi ya jumla na vivumishi vya idadi ya matokeo.

### *i) Vivumishi vya idadi kamili*

Pia huitwa vivumishi vya idadi halisi au bainifu. Huonyesha hesabu halisi ya nomino husika. Baadhi ya vivumishi hivi huchukua viambishi vya ngeli kutegemea nomino inayohesabiwa.
Mfano: -moja, -wili, -tatu, -nne, -tano na -nane.

**Mifano**

1. Ukwato mmoja haupo.
2. Wafugaji watano wanawapeleka punda kunywa maji.
3. Magunia matatu ya mtama yameletwa.
4. Mihogo minane itang'olewa shambani.
5. Viti vinne vitakaliwa na wakulima.
6. Mapapai mawili ni yetu.
7. Ngamia watatu hawakuwatosha kwa safari hiyo.

Baadhi ya vivumishi vya idadi kamili havichukui viambishi vyovyote vya ngeli. Yaani hutumika jinsi vilivyo bila kubadilika.
Mfano: sita, saba, tisa na kumi, makumi, mia na kadhalika

**Mifano**

1. Matunda sita yameharibika.
2. Wakulima saba watavuna mahindi.
3. Mapanga tisa yatumiwe kukatia miti.
4. Vijiko kumi vya sukari vitawatosha.

### *ii) Vivumishi vya idadi ya jumla/isiyo kamili*

Huonyesha idadi ambayo ujumla wake haujulikani. Baadhi ya vivumishi hivi huchukua viambishi vya ngeli ya nomino.

Mfano: -chache na –ingi

*Mfano katika sentensi:*

1. Kuku hawa wametaga mayai machache.
2. Mwaka huu tumepanda mbegu nyingi.
3. Wakulima wengi wamevuna.
4. Wao huuza maziwa mengi sana.

Baadhi ya vivumishi vya idadi ya jumla havichukui viambishi vya ngeli. Yaani hubakia vivyo hivyo.
Mfano: kadhaa, tele, kiasi, kidogo na haba.

**Mifano**

1. Nimevuna mahindi tele.
2. Amewapa kuku chakula haba.
3. Niongeze mbegu kiasi nipande.
4. Tengeneza matuta kadhaa.
5. Usiwape punda maji kidogo.

#### *iii) Vivumishi vya idadi ya matokeo*

Pia huitwa vivumishi vya nafasi katika orodha. Vivumishi hivi huonyesha nafasi ya nomino katika orodha.

***Mifano***

1. Mfugaji wa kwanza amepewa zawadi.
2. Tingatinga ya pili inalima shamba.
3. Simba wa mwisho ni jike.
4. Upanzi wa mwanzo utakuwa mnamo Februari.

**Zoezi**

a) Jaza kila pengo kwa kivumishi sahihi katika mabano.
   i. Sungura ________ wanakimbia. (chache)
   ii. Masokwe __________ wanacheza. (sita)
   iii. Mkulima __________ atapewa mbolea. (moja)
   iv. Amenunua maembe_________. (ingi)
   v. Tumelima mashamba__________. (nane)

b) Tunga sentensi kumi sahihi kuhusu kilimo na ufugaji ukitumia vivumishi vya idadi jumla na isiyo jumla.

#### *e) Vivumishi viulizi*

Hili ni kundi la vivumishi ambalo lina maneno yatumiwayo kuulizia maswali. Baadhi ya mifano ya vivumishi viulizi ni:

#### *i) Kiulizi -pi?*

***Mifano***

| | **umoja** | **wingi** |
|---|---|---|
| 1. | Mkulima yupi anavuna maharagwe? | Wakulima wapi wanavuna maharagwe? |
| 2. | Muhogo upi ni wangu? | Mihogo ipi ni yetu? |
| 3. | Ndizi ipi inatakikana? | Ndizi zipi zinatakikana? |
| 4. | Nikupe jembe lipi? | Tuwape majembe yapi? |

#### *ii) Kiulizi -ngapi?*

***Mifano***

1. Wafugaji wangapi wanakuja?
2. Mihindi mingapi imezaa mahindi?
3. Mbuga ngapi zina masokwe?
4. Mananasi mangapi yameiva?

### *iii) Kiulizi gani?*

Kiulizi hiki hakichukui kiambishi chochote cha ngeli.

*Mifano*

1. Unataka fyekeo gani?
2. Mkulima gani anakuja?

## Tanbihi

Kivumishi kiulizi kinastahili kuandamana na nomino au kiwakilishi cha nomino. Viulizi ambavyo havitumiwi pamoja na nomino au viwakilishi vya nomino haviwezi kuitwa vivumishi bali ni viulizi.
Mfano: lini, nani, nini, vipi. Hivi si vivumishi viulizi kwa sababu havitumiwi pamoja na nomino au kiwakilishi cha nomino.

**Zoezi**

a) Tumia kiulizi '-pi' kwa usahihi kujazia kila pengo.
   i. Mashirika __________ yanasaidia wakulima?
   ii. Mkahawa __________ unakatwa?
   iii. Dawa __________ zinanyunyiziwa mimea?
   iv. Niwaite wafugaji __________?
   v. Kufyeka __________ kunafaa?

b) Tumia kivumishi kiulizi '-ngapi' kwa usahihi kujazia kila pengo.
   i. Tukupe magunia __________?
   ii. Pembe __________ zimekatwa?
   iii. Mbwa __________ wamechanjwa?
   iv. Mipera __________ inapandwa?
   v. Vibuyu __________ vina maziwa?

### *f) Vivumishi vimilikishi*

Maneno katika kundi hili la vivumishi hujibu swali mtu, kitu au jambo ni la nani au lina nini? Vivumishi hivi huwa sita pekee katika Kiswahili.

| | |
|---|---|
| -angu | -etu |
| -ako | -enu |
| -ake | -ao |

Kutokana na haya, unapata maneno kama vile:

| | |
|---|---|
| wangu | wetu |
| chako | chenu |
| kwake | kwao |

Unaweza kutunga sentensi hizi ukitumia vivumishi vimilikishi:

1. Jibini hii ni yangu.
2. Mawele yako yameliwa na fukusi.
3. Mbatata zenu zinauzwa Zambia.
4. Njugu za kwao ni tamu mno.

5. Huwezi kusema kuwa huu ni mchicha wako!

## Zoezi

Jaza kila pengo kwa kivumishi kiwakilishi sahihi.

1. Nyinyi mna mihogo. Mihogo ni ___________.
2. Sisi tuna maembe. Maembe ni _____________.
3. Wao wana sufu. Sufu ni _____________.
4. Mimi nina sukari. Sukari ni ____________.
5. Yeye ana kole la ndizi. Kole ni __________.
6. Wewe una muhogo. Muhogo ni _____________.

## Kazi ya wanafunzi wawili wawili

*Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Someni kifungu kifuatacho huku mkitambua jinsi vivumishi vilivyotumiwa.*

Mimi ni mwanafunzi mwenye bidii. Nia yangu kuu maishani mwangu ni kuridhika na shughuli za kilimo cha kisasa kama mojawapo ya njia nzuri za kupigana dhidi ya umaskini. Lengo langu kuu la kwenda shuleni hasa ni kupata maarifa mema ya kuniwezesha kuishi maisha ya kitajiri. Maarifa hayo yataniwezesha kuwa mkulima bora.

Nitaendelea na masomo hadi chuo kikuu. Nitafanya somo la Kilimo katika chuo kikuu. Hata hivyo, hilo pekee halitatosha. Nitafanya kazi ndogo ndogo kwa muda ili kutafuta pesa za kuanzisha kilimo. Kufikia hapo, nitakuwa nimepiga hatua lakini bado sitakuwa nimefikia lengo langu.

Kuanzisha kilimo cha kisasa kutakuwa ni hatua kubwa lakini bado kutakuwa na kazi kubwa ya kufanywa. Ni sharti niupige vita vikali umaskini kupitia kilimo hicho. Umaskini ni adui mbaya ambaye lazima niangamize. Njia moja ya kumaliza umaskini ni kuweka uvivu kando.

Mbali na kulima, nitafuga mifugo wengi. Nitahakikisha ya kuwa nina vifaa vyote vinavyohitajika kwa kufanyia kazi hizo mbili. Kutakuwa na trekta kubwa kubwa na mashine za kukamua. Nitanunua magari mazuri ya kusafirisha mazao mengi nitakayovuna. Nitawapa vijana wenzangu kazi ili nao wawe na kipato kizuri. Kwa jumla, nitahakikisha kuwa vitu vyote anavyohitaji mkulima wa kisasa vipo.

Mwisho, nitatafuta masoko mazuri na ya kuaminika. Nia yangu hapa ni kuuza bidhaa zangu katika masoko yaya haya ya hapa kwetu. Baadaye nitaziuza katika masoko, nje ya nchi yetu. Hizi zote zitakuwa ni juhudi za kuendeleza vita vikali dhidi ya umaskini au uchochole.

## Zoezi

1. Orodhesheni vivumishi vyote vilivyomo kifunguni humu kwa kuzingatia aina ya kila kivumishi husika.
2. Tunga sentensi fupi fupi na sahihi ukitumia vivumishi mlivyoorodhesha hapo juu.

## Viwakilishi

Viwakilishi ama vibadala ni maneno ama viambata (sehemu za maneno) vinavyosimama badala ya majina. Kundi hili la maneno huweza kugawika katika sehemu mbalimbali ifuatavyo.

### *a) Viwakilishi nafsi*

Husimamia nafsi za nomino inayozungumziwa katika umoja au wingi. Kuna aina mbili kuu za viwakilishi vya nafsi:

*i) Viwakilishi nafsi huru*

Huwakilisha nafsi iliyo huru, yaani isiyounganishwa na kitenzi katika umoja na wingi kwenye sentensi.
Mfano: nafsi ya kwanza (mimi, sisi), nafsi ya pili (wewe, nyinyi), nafsi ya tatu (yeye, wao).

**Zoezi**

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Mimi ninalima. | Sisi tunalima. |
| 2. Wewe unavuna. | Nyinyi mnavuna. |
| 3. Yeye anafyeka. | Wao wanafyeka. |

*ii) Viwakilishi nafsi viambata*

Viwakilishi hivi huambatanishwa na vitenzi.
Mfano: nafsi ya kwanza (ni-, tu-), nafsi ya pili (u-, m-) nafsi ya tatu (a-, wa-)

***Mifano***

| Umoja | Wingi |
|---|---|
| 1. Nitapanda viazi kesho. | Tutapanda viazi kesho. |
| 2. Utachanja mbwa wako. | Mtachanja mbwa wenu. |
| 3. Atalima shamba lote. | Watalima mashamba yote. |

*iii) Pia, vipo viwakilishi ambata vya ngeli. Navyo ni:*

***Mifano***

| umoja | wingi | |
|---|---|---|
| 1. Umepandwa. | Imepandwa. | (u-, i-) |
| 2. Yamemwagika. | Yamemwagika. | (ya-, ya-) |
| 3. Limepandwa. | Yamepandwa. | (li-, ya-) |
| 4. Kimepotea. | Vimepotea. | (ki-, vi-) |
| 5. Imevunwa. | Zimevunwa. | (i-, zi-) |

### *b) Viwakilishi vitokanavyo na vivumishi*

Je, unakumbuka vivumishi ulivyosoma hapo juu? Endapo kivumishi husika kimetumika badala ya nomino, kivumishi hicho kinakuwa kiwakilishi. Nacho kiwakilishi hicho huchukua jina la kivumishi hicho. Mfano:

*i) Viwakilishi vionyeshi*

Hutokana na vivumishi vionyeshi. Tazama vivumishi vionyeshi. Unapoondoa nomino katika vivumishi hivyo, unapata viwakilisihi vionyeshi.

***Mifano***

| Vivumishi vionyeshi | Viwakilishi vionyeshi |
|---|---|
| 1. Mkulima huyo huyo ni hodari. | Huyo huyo ni hodari. |
| 2. Ndovu yule ni mkubwa. | Yule ni mkubwa. |
| 3. Mazao yale ni yetu. | Yale ni yetu. |
| 4. Viazi vile ni vingi. | Vile ni vingi. |
| 5. Miwa ii hii itavunwa. | Ii hii itavunwa. |

Kumbuka kwamba hufai kutumia nomino na kiwakilishi katika sentensi moja.

*ii) Viwakilishi viulizi*

Viwakilishi hivi vinatokana na vivumishi viulizi.

***Mifano***

| Vivumishi viulizi | Viwakilishi viulizi |
|---|---|
| 1. Wakulima wangapi wamefika? | Wangapi wamefika? |
| 2. Chai ipi haina sukari? | Ipi haina sukari? |
| 3. Jembe gani ni lako? | Gani ni lako? |

*iii) Viwakilishi vimilikishi*

Viwakilishi hivi hutokana na vivumishi vimilikishi. Tazama mifano hapa chini.

***Mifano***

| Vivumishi vimilikishi | Viwakilishi vimilikishi |
|---|---|
| 4. Shambani mwangu mna magugu. | Mwangu mna magugu. |
| 5. Chai yangu haina sukari. | Yangu haina sukari. |
| 6. Jembe lako ni gani? | Lako ni gani? |

**Zoezi A**

Tunga sentensi ukitumia viwakilishi mbalimbali.

**Zoezi A**

Soma kifungu kifungu kifuatacho huku ukitambua jinsi viwakilishi vilivyotumiwa.

Zama hizo, fisi alikuwa jirani ya binadamu aliyependa kulima. Binadamu alimiliki shamba kubwa la mihogo. Naye Fisi alikuwa mvivu aliyependa kumtembelea binadamu kwake. Alidhani kuwa huyo binadamu naye alimpendana sana. Hata

hivyo, binadamu hakumpenda sana fisi. Fisi hakupenda kulima bali alipenda sana kula.



Siku moja jioni, fisi alimuaga binadamu na kusema, “Kesho nitaamkia huku kwako ili uniandalie kiamshakinywa!”

Kwa roho ya ndani, mwanadamu alijisemea, ‘Huyu hapendi kufanya kazi, anapenda tu kula. Kwa nini haoni kuwa simpendi?’

Akamwambia fisi, “Labda utanipata, labda utanikosa.”

Fisi kuona kuwa anaweza kukosa mlo alisema, “Basi nitajaribu nije hata mapema zaidi. Kwa namna hiyo tunaweza kula halafu wewe uende shambani. Napenda sana namna unavyopika nyama.” Bila kungoja jawabu, alitoka na kujiendea zake.

Keshoye, mwendo wa saa kumi na moja asubuhi, fisi alibisha hodi kwa mwanadamu. Naye mwanadamu hakusita kumfungulia mlango. Mwanadamu aliazimia kumfunza fisi adabu.

“Karibu, karibu kwangu rafiki yangu,” mwanadamu alijibu.

Naye fisi kwa kusukumwa na njaa yake ya asubuhi pamoja na ulafi wake, alimpita tu na kuingia ndani. Harufu ya nyama mle ndani ilimfanya fisi ameze mafunda ya mate.

“Karibu, karibu kaa,” mwanadamu alimlaki fisi. “Nipe dakika chache tu na chakula kitamu na kingi kitakuwa mezani hapa.”

“Basi fanya haraka. Ninakufa kwa njaa,” fisi alisema.

Baada ya muda usiokuwa mrefu vile, mwanadamu alikuwa ameandika meza kwa kila namna ya nyama ya mifupa. Ohoo! Fisi kuona hivyo, nusura kuirukia lakini mwanadamu akamzuia kwa kusema, “Bwana fisi, ili leo ushibe vya kutosha, tumbukiza kila sahani mdomoni mwako na umeze tu bila kutafuna.”

Hata kabla ya mwanadamu kumaliza usemi wake, fisi alikuwa ametumbukiza sahani mbili kinywani mwake!

“Mbona hiki cha leo ni kikali jinsi hii? Lo! Kinawasha sana! Looooooooo!” Fisi alilalamika.

Kumbe mwanadamu alijaza pilipili kwenye nyama. Tangu siku hiyo, fisi hakurudi tena kwa mwanadamu.

## Maswali

1. Je, fisi alikuwa mnyama wa aina gani?
2. Ni kwa nini mwanadamu hakumpenda fisi?
3. Mwanadamu aliikomeshaje tabia mbaya ya fisi?

4. Unadhani ni yapi yaliyompata fisi?
5. Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Bainisheni viwakilishi vyote vilivyomo katika kifungu mlichosoma hapo juu. Tungeni sentensi sahihi mkitumia vivumishi hivyo.

## Vielezi

Vielezi pia huitwa viarifa. Ni maneno yafafanuayo vitenzi, vivumishi au vielezi vingine. Mathalan, ukisema *Anatembea haraka,* neno 'haraka' linaeleza jinsi anavyotembea mhusika. Kwa hivyo, neno hilo linalokuarifu mengi kuhusu kutembea ni kielezi.

Maneno haya hujigawa katika vikundi mbalimbali kama ifuatavyo:

### a) Vielezi vya namna au jinsi

Haya ni maneno ambayo huarifu jinsi ya kutendeka mambo.

Mfano: sana, bure, kitoto, vizuri, upesi, kwa miguu, kwa bidii, bwe!

*Mifano*

1. Majibwa hubweka bwe! shambani humo.
2. Ulisumbuka bure kulima kwani mvua haikunyesha.
3. Je, ni kweli kuwa shamba hilo limelimwa upya?
4. Sisi hulima kwa jembe la mkono.
5. Usipofanya kazi ya kilimo kwa bidii, utapata mazao duni.

### b) Vielezi vya wakati

Nayo haya ni maneno yanayofafanua ama kueleza wakati wa kutokea tendo. Mathalan, ukisema *Mgeni alifika jioni* neno *jioni* ni kielezi cha wakati.

Vipo vielezi vya wakati vya aina mbili:

*i) Vielezi vya wakati maalumu.*

Mfano: Januari, Disemba, Jumamosi, saa tatu, kesho, leo, mtondo na kadhalika.

*Mifano*

1. Je, msimu wa kupalilia huwa mwezi wa Machi?
2. Nitaanza kufyeka mnano Oktoba.
3. Njoo kesho uchukue maziwa.
4. Tutalima asubuhi.

*ii) Vielezi vinavyotaja wakati kwa jumla*

Mfano: baadaye, zamani, daima, milele, awali, punde, karibuni, zama hizo.

*Mifano*

1. Watapanda kunde baadaye.
2. Mchunga mbuzi huyo alizaliwa zamani.
3. Bei ya njugu itashuka hivi karibuni.
4. Walikuza mawele hapo awali.

### c) Vielezi vya kiasi/idadi

Vielezi vya kiasi ni namna ya maneno ambayo hufafanua vitenzi kwa kujulisha limetokea mara ngapi tendo linalotajwa.

***Mifano***

kila mara, kwa nadra, mara nyingi, tena na tena, mno
mara kumi, mara moja, mara nne, mara sita, mara kumi na mbili,
mara ya kumi, mara ya kwanza, mara ya mwisho, mara ya ishirini

*Mifano katika sentensi*

1. Chuo kikuu hiki cha Kilimo sasa kinafanya mahafali mara ya thelathini.
2. Nimekuita mara kumi ili uone ndovu lakini husikii.
3. Magonjwa hutokea kwa nadra katika chuo hicho cha ufugaji.
4. Wanakijiji wa hapa huvuna mara mbili kwa mwaka.

### d) Vielezi vya mahali

Haya nayo ni maneno ama mafungu ya maneno yanayofafanua panapotokea kitendo. Mara nyingi, maneno haya huwa ni majina ya mahali.

***Mifano***

ndani, nje, karibu, juu, chini, kando, nyuma, pembeni

*Mifano katika sentensi:*

1. Mwizi wa kahawa alikuwa amejificha pembeni mwa chumba.
2. Usiporudi nyuma, huwezi kuiona michungwa hiyo.
3. Mliamrishwa kuingia ndani ya ghala hilo.
4. Usitembee juu ya nafaka!
5. Ni hatari kusimama kando ya mto uliofurika.

**Zoezi**

*Jiunge na wenzako watatu na mworodheshe vielezi vyote vilivyomo kifunguni humu huku mkivitungia sentensi fupi na sahihi.*

Gakwerere alikuwa mfugaji mwenye bidii nyingi sana tangu zamani. Mwanzoni, Gakwerere alikuwa akifuga ng'ombe wa kienyeji. Aliwalisha ng'ombe hao uwanjani na pembeni mwa mashamba. Hata hivyo, ng'ombe hao hawakuwa wakimpa kiasi cha maziwa alichotarajia. Angewakamua mara moja tu kwa siku. Alikata shauri kuanzisha ufugaji wa ng'ombe bora wa maziwa.

Mfugaji huyu aliwapeleka ng'ombe wake wa kienyeji sokoni na kuwauza mnamo Novemba. Baada ya kuwauza, aliamka alfajiri na kufunga safari ya kuzuru shamba la kisasa la Nyinawumuntu. Bi. Nyinawumuntu alikuwa mfugaji na mkulima mashuhuri sana katika eneo hilo alilokaa Gakwerere. Alipofika huko, alimpata bibiye yupo na wakaanza kupiga bei. Baada ya kukubaliana bei, alinunua mitamba wawili kwa bei nafuu. Alilipa papo hapo kwa sababu hakutaka kuwa na deni.

Kumaliza hivi tu, yule bibi alimpa Gakwerere gari lake ili alitumie kuwasafirisha ng'ombe wake. Gakwere alimshukuru kwa wema wake na akawasafirisha hao mitamba wake hadi kwake.

Alipofika nyumbani kwake, mfugaji huyo alianza kuwalisha ng'ombe wake kwa njia za kisasa. Kwa kuwa walikuwa wakilishwa kwa lishe bora ya ng'ombe, haukuchukua muda mrefu kuwapandisha. Muda ulipowadia, walizaa ndama wawili wenye afya nzuri.

Baada ya muda usio mrefu, Gakwerere alianza kuvuna matokeo ya jasho lake la kila siku. Hakuamini kiasi cha maziwa alichokuwa akikama kila asubuhi na jioni.

Aliweka akiba kwa muda. Hatimaye, mfugaji huyu alinunua gari. Alitumia gari hilo kuwatafutia na kuwabebea chakula ng'ombe hao wake wa gredi.

## E Matumizi ya wakati uliopo na uliopita na vitenzi vya silabi moja

### i) Matumizi ya wakati uliopo (-na-) na vitenzi vya silabi moja

Wakati uliopo -na-unaweza kuwa katika hali mbili: Hali hizo ni hali yakinishi na hali kanushi. Hali yakinishi ni ya ukubali na hali kanushi ni ya ukatavu.
**Soma sentensi hizi.**

| | Kitenzi | Hali yakinishi | Hali kanushi |
|---|---|---|---|
| i) | fa | Mkahawa unakufa. | Mkahawa haufi. |
| ii) | la | Ng'ombe anakula nyasi. | Ng'ombe hali nyasi. |
| iii) | nywa | Kifaranga anakunywa maji. | Kifaranga hanywi maji. |
| iv) | ja | Mkulima anakuja. | Mkulima haji. |
| v) | pa | Mwalimu anampa ndizi. | Mwalimu hampi ndizi. |
| | nya | Mvua inanyesha. | Mvua hainyeshi. |

***Hali yakinishi***

Hali yakinishi ni hali ya kukubali. Tazama tena mifano iliyopo hapo juu. Vitenzi *unakufa, anakula, anakunywa, anakuja, anampa na inanyesha* vimo katika hali yakinishi, yaani hali ya kukubali.

***Hali kanushi***

Nayo hali kanushi ni hali ya kukataa. Itazame tena mifano hapo juu. Vitenzi *haufi, hali, hanywi, haji, hampi na hainyeshi* vipo katika hali kanushi, yaani hali ya kukataa.

**Unaweza kutunga sentensi zaidi za namna hii kama ifuatavyo**:

| Hali yakinishi | Hali kanushi |
|---|---|
| Nafa kwa njaa. | Sifi kwa njaa. |
| Nala muhogo kwa samaki. | Sili muhogo kwa samaki. |

| | |
|---|---|
| Anakunywa chai. | Hanywi chai. |
| Wanakuja hapa kufyeka. | Hawaji hapa kufyeka. |
| Tunakupa mbegu hizi. | Hatukupi mbegu hizi. |
| Unamcha Mwenyezi Mungu? | Humchi Mwenyezi Mungu? |
| Maji yanakupwa sasa. | Maji hayapwi sasa. |

***Kazi ya wanafunzi wawili wawili***

Jiunge na mwenzako. Tafuteni vitenzi zaidi vyenye silabi moja katika kamusi huku mkijadiliana mabadilko ambayo hutokea vitenzi hivyo vinapotumiwa katika hali kanushi na yakinishi.

### ii) Matumizi ya wakati uliopita -li- na vitenzi vya silabi moja

Wakati uliopita huonyesha kuwa kitendo kilifanyika muda mrefu uliopita. Wakati huu huwakilishwa na -li-. Vitendo husika vinaweza kuwa katika hali yakinishi au kanushi. Kama ujuavyo, hali yakinishi ni ya kukubali na hali kanushi ni kukataa.

*Tazama mifano ifuatayo:*

| | Kitenzi | Hali yakinishi | Hali kanushi |
|---|---|---|---|
| i) | fa | Mharagwe unakufa. | Mharagwe haufi. |
| ii) | la | Mbuzi anakula majani. | Mbuzi hali majani. |
| iii) | nywa | Paka anakunywa maziwa. | Paka hanywi maziwa. |
| iv) | ja | Mfugaji anakuja. | Mfugaji haji. |
| v) | pa | Mwanafunzi ananipa ndizi. | Mwanafunzi hanipi ndizi. |
| vi) | nya | Asifuye mvua inamnyeshea. | Asiyesifu mvua haimnyeshei. |

Vitenzi hivyo vipo katika wakati uliopo. Tunaweza kuvigeuza viwe katika wakati uliopita kwa kuweka '-li-' mahali pa '-na-'. Tunapofanya hivyo, tunamaanisha kuwa vitendo hivyo vilifanyika muda au wakati uliopita. Tazama jedwali hili.

*Tazama mifano ifuatayo:*

| | Kitenzi | Hali yakinishi | Hali kanushi |
|---|---|---|---|
| i) | fa | Mharagwe ulikufa. | Miharagwe haikufa |
| ii) | la | Mbuzi alikula majani. | Mbuzi hakula majani. |
| iii) | nywa | Paka alikunywa maziwa. | Paka hakunywa maziwa. |
| iv) | ja | Mfugaji alikuja. | Mfugaji hakuja. |
| v) | pa | Mwanafunzi alinipa ndizi. | Mwanafunzi hakunipa ndizi. |
| vi) | nya | Asifuye mvua ilimnyeshea. | Asiyesifu mvua haikumnyeshea. |

Katika jedwali lililopo hapo juu, vitenzi *ulikufa, alikula, alikunywa, alikuja, alimpa, na ilimnyeshea* vimo katika hali yakinishi au kukubali kwa wakati uliopita. Navyo vitenzi *haukufa, hakula, hakunywa, hakumpa, haikumnyeshea* vimo katika hali ya kukataa yaani hali kanushi.

## Mazoezi ya ziada

### Zoezi A

Jiunge na mwanafunzi mwenzako na mworodheshe vitenzi vinane vya silabi moja huku mkivitungia sentensi sahihi katika wakati uliopita. Sentensi zenu zihusiane na kilimo na ufugaji. Someaneni vitenzi na sentensi huku mkisahihishiana.


### Zoezi B

Jiunge na wanafunzi wenzako katika kikundi. Msomeane tungo au hadithi mbalimbali zilizopo katika kitabu hiki na vitabu vingine. Mbainishe na kuainisha aina za maneno katika tungo hizo (vivumishi, viwakilishi na vielezi) kama vinavyotokea katika umoja na wingi pamoja na matumizi ya wakati uliopo na wakati uliopita.

## Maswali ya marudio



Ili kujikumbusha mengi ya yale uliyojifunza katika sehemu hii, yajibu vilivyo maswali haya yafuatayo yote.

1. Bila ya kuangalia popote, taja maneno kumi yanayohusu mazao na kumi yanayohusu ufugaji huku ukiyaeleza.
2. Ipo misimu mingapi hapa Rwanda? Ieleze huku ukirejelea upanzi na uvunaji wa mimea.
3. Tazama picha zifuatazo. Eleza misimu kulingana na kila mchoro.

| | | |
|---|---|---|
| a)  | b)  | c)  |

4. Tunga sentensi sahihi ukitumia msamiati ufuatao:
   a) mahindi b) ndizi c) kahawa
   d) viazi mviringo e) maharagwe f) njugu
5. a) Jaza kila pengo kwa jina sahihi la kifaa cha kilimo.
   i) Ndoli anafyeka shamba kwa _______________.
   ii) Mkulima yule anatumia __________ la mkono kulimia shamba lake.
   iii) Shamba kubwa hulimwa kwa ________________.
   iv) ___________ hutumiwa kukata matawi ya miti shambani.
6. Tunga sentensi tano fupi ukitumia vifaa mbalimbali vya kilimo ambavyo vinatumiwa katika eneo utokako.
7. Eleza jinsi unavyopanga kupiga vita uchochole kwa kilimo cha kisasa.
8. Taja majina kumi ya mifugo nchini Rwanda na uyatungie sentensi sahihi.
9. Taja chuo cha kilimo hapa nchini ambacho ungependa kukiingia baada ya masomo yako huku ukieleza ni kwa nini unakistahi chuo hicho.
10. Eleza umuhimu wa ufugaji katika jamii unapotoka.

11. Zipo tamaduni zozote za kikwenu zihusuzo kilimo na ufugaji? Zitaje huku ukieleza huo uhusiano.
12. Taja wanyama kumi wa porini wanaopatikana nchini Rwanda.
13. Andika majina na sifa za wanyama wafuatao wa porini:

| a) | b) | c) | d) |
|---|---|---|---|
|  |  |  |  |

14. Eleza faida za wanyama wanaoishi porini.
15. Pendekeza njia zinazoweza kutumiwa kuwavutia watalii wanaozuru mbuga zetu za wanyama wa porini.
16. Eleza maana ya:
    a) nomino
    b) vivumishi
    c) vielezi
    d) viwakilishi
17. Huku ukitoa mifano, eleza aina nne nne za:
    a) nomino    b) vivumishi    c) vielezi
18. a) Je, vitenzi vya silabi moja ni maneno ya aina gani?
    b) Andika mifano minne ya maneno yenye silabi moja na uyatungie sentensi sahihi.
19. a) Huku ukitoa mifano, eleza tofauti zilizopo kati ya:
        i) wakati uliopo na wakati uliopita
        ii) hali kanushi na yakinishi
    b) Andika sentensi zifuatazo katika hali yakinishi au kanushi.
        i) Baba anakula mahindi.
        ii) Mahindi hayafi wakati wa kiangazi.
        iii) Ng’ombe hakunywa maji jana.
        iv) Mkulima alimpa ndizi nyingi.
    c) Andika sentensi zifuatazo katika wakati uliopo au uliopita.
        i) Ndoli anakula mihogo.
        ii) Mimi sinywi maziwa.
        iii) Mama alinipa jembe.
        iv) Kuku hao hawakufa.
20. Kwa ufupi, elezea mambo muhimu uliyojifunza katika sura hii na useme jinsi yatakavyokufaidi na jamii.

# 2 Mada kuu: Utungaji

## Mada ndogo: Barua kuhusu matembezi, Barua za kirafiki, Barua za mwaliko, Simu,Tangazo/Ilani.

## A Barua

Barua ama waraka ni maandishi yaliyopangwa kwa utaratibu na mtiririko maalumu kwa minajili ya kuwasilisha ujumbe fulani. Zipo aina mbili kuu za barua: Ipo barua ya kirafiki ambayo pia huitwa barua ya kindugu na ipo barua rasmi.

### a) Barua za kirafiki

Barua ya kirafiki ni barua ambayo huandikiwa mtu ama watu mbalimbali walio na uhusiano wa karibu na anayeandika; kama vile rafiki, mzazi, dada na kadhalika.

**_Kazi ya wanafunzi wawili wawili_**

Jiunge na mwenzako na mjadili barua zenu mlizoandika. Je, waandikiwa walikuwa kina nani? Ujumbe ulikuwa upi na ni lugha gani uliyotumia?

*Mifano ya barua za kirafiki*

***i) Barua ya mwana kwa mzazi***



Ukimwandikia mama barua, barua hiyo ni ya kirafiki.

***Mfano***

Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Jitegemee,

S.L.P. 1300,

KICUKIRO.

4/5/2016.

Kwa Mama Mpendwa,

Pokea salamu zangu za dhati. Shuleni nipo salama. Ninashukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na afya njema. Je, hali ya huko nyumbani iko vipi?
Mama, nina hamu kubwa sana ya kukuona. Hata nikijaribu kumakinika katika masomo napata kuwa mawazo yangu yako kwako tu. Juzi, mwalimu ameniadhibu kwa kushikwa na ndoto za mchana akifundisha.

Tafadhali, niombee ruhusa kwa mwalimu wa zamu nipate kuja kukuona angaa katika saa moja tu. Kama sivyo, basi mama njoo huku shuleni tuonane.
Jambo jingine ni kwamba pesa za masurufu alizonipa baba kutumia muhula mzima zilikwisha. Sasa ninahangaika tu. Naomba kwamba pindi utakapokuja uniletee angalau pesa kidogo za kumalizia muhula huu.

Nisalimie sana baba na mdogo wangu.

Ni mimi mwanao,

Ineza.

**Zoezi**

Mwandikie ndugu yako barua ukimweleza maendeleo yako katika masomo.

### *ii) Barua ya mapenzi*



Barua ya kindugu inaweza kuwa ya mapenzi pia.

***Mifano***

Bazimanga,

S.L.P. 1300,

HUYE.

4/7/2016.

Kwa Kipenzi Changu cha Roho,

Pokea salamu nyingi kutoka kwangu. Kwanza mpenzi, nieleze hali yako. Uko salama? Je, nyumbani hawajambo?

Huku sina neno. Ninakuwaza tu ewe ua la moyo wangu. Hata kula ni shida. Siku hizi siwezi kutulia kwa kukuwaza. Jana jioni niliondoka hapa kwangu kuja kukuona lakini nikashindwa kufika. Kwenu ni mbali sana. Giza liliingia ningali njiani.

Je, utafika lini hapa kwetu nipate kukuona na kukujulisha kwa baba na mama? Ningependa wakuone jinsi ulivyoumbwa ukaumbika. Nataka waone jinsi ulivyo na miondoko ya njiwa. Nataka waone ulivyo na roho safi. Ninataka waone mke wangu wa kesho. Mpenzi, fanya hima ufike.

Ninaweza kuendelea kukupa habari zangu zinazokuhusu wewe kwa mwaka mzima lakini wacha nikomee hapa kwa mabusu teletele.

Kwaheri ya kuonana kipenzi.

Ni mimi wako wa milele,

Bazimanga.

**Zoezi**

Jifanye kuwa una zaidi ya miaka kumi na minane. Mwandikie mchumba wako barua ukimweleza sababu ya kumpenda na kutaka kumwoa.

### *iii) Barua ya kutoa ushauri*

Isitoshe, barua ya kirafiki inaweza kuwa ni ya mzazi anayetoa ushauri kwa mwanawe.

***Mifano***

S.L.P. 2217,

Kigali, Rwanda.

10/11/2016.

Kwa Ganza,

Habari za siku nyingi mwanangu? Hali ya huko ikoje? Sisi huku tu salama tunamshukuru Mwenyezi Mungu.

Nimepokea kwa furaha kuu habari kuwa umepata mchumba. Hakuna habari imfurahishayo mzazi zaidi ya habari hii.

Kwanza, namwomba Mwenyezi Mungu awabariki sana kwa kila namna.

Pili, nakushaurini kuwa ndoa ni kuvumiliana na kumweka Mwenyezi Mungu mbele. Mkiwa na imani katika Mungu, hakuna litakalotishia ndoa yenu.

Tatu, mwepukane na ugomvi. Mwenzio akikukosea, shaurianeni na muombeane neema kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Nne, fanyeni kazi kwa bidii ya mchwa ili mpate chenu. Mweze kujianzishia biashara ama mradi wenu wowote wa kuleta mapato. Si lazima uajiriwe ndipo ufaulu maishani.

Mtakapojaaliwa watoto, watunze kwa dhati na maombi. Hakikisheni kuwa wanakua vilivyo na msisahau kuniletea wajukuu zangu nikae nao mwenyewe wakati wa likizo.

Basi, nakuombeeni baraka iliyo na msingi wa imani katika Mungu wa kweli.

Ni mimi babako,

Bwana Paul Ndoli.

**Zoezi**

Wewe ni mzazi ambaye mwanao amepotoka. Mwandikie barua ya kumwelekeza kuepukana na upotovu huo na arudie wema wake wa awali. Someni barua zenu mbele ya darasa.

## Sehemu kuu za barua za kirafiki

Barua za kirafiki huwa na sehemu au muundo fulani maalumu.

***Kazi ya kikundi***

Jiunge na wanafunzi wenzako katika kikundi. Tazameni mifano ya barua za kirafiki iliyotolewa na mingineyo. Jadilianeni kuhusu sifa zinazofanana katika barua zote.

***Tazama mfano wa muundo wa barua ya kirafiki. Kuna uhusiano gani kati ya yaliyomo na barua za kirafiki ulizosoma?***

Anwani

Tarehe

Kutaja mwandikiwa

Utangulizi/salamu

Mwili wa barua

Hitimisho

Jina la mwandishi.

**Barua ya kirafiki huwa na sehemu kuu zifuatazo:**

i) Anwani moja ya mwandishi: Huandikwa juu, pembeni.
ii) Tarehe: Huandikwa chini ya anwani kwa kuacha nafasi ya mstari mmoja.
iii) Kutaja mwandikiwa: Huja chini ya tarehe kwa kuacha nafasi ya mstari mmoja.
iv) Utangulizi: Hujitokeza katika aya ya kwanza. Mwandishi humjulia hali mtu anayeandikiwa na wenzake. Pia, husema hali yake.
v) Mwili wa barua: Mwandishi hupitisha ujumbe wa barua/kuelezea kiini cha kuandikwa kwa barua husika.
vi) Hitimisho/Kufunga barua: Mwandishi huhitimisha barua yake kwa kumtakia heri aliyeandikiwa. Jina la mwandishi wa barua huja chini ya hitimisho.

**Zoezi**

*Tazama barua iliyopo hapa chini. Je, barua hii ina makosa gani? Andika upya barua hii kwa kusahihisha makosa yaliyopo na kuongezea sehemu zinazokosekana.*

Kwa Shangazi Mpendwa,
S.L.P, 45
Kigali
Rwanda

Wako Mpendwa,

Ninajua wewe unapenda sana kilimo cha ndizi. Juzi tulisoma kuhusu kilimo bora cha ndizi. Mwalimu wetu alitufunza mbinu mpya za kupanda ndizi. Tukifunga, nitakutembelea ili nikufunze mbinu hii mpya itakayokupa mavuno mengi zaidi.

Unisalimie wote waliopo nyumbani. Waambie nitawatembelea wakati wa likizo.

Kwanza, ningependa kukueleza kuwa ninazidi kutia bidii katika masomo. Juzi tulifanya majaribio na niliibuka nafasi ya tatu katika darasa letu. Ninatia bidii zaidi. U hali gani? Mimi nipo salama. Nia yangu kuu ya kukuandikia barua hii ni kukujulisha kuhusu mambo mawili makuu.

## Kanuni za kuzingatiwa katika uandishi wa barua za kirafiki

Zipo kanuni mbalimbali za kuzingatiwa wakati wa kuandika barua ya kirafiki. Soma kifungu kifuatacho ili kubainisha baadhi ya kanuni hizo.



USANASE: Hujambo, Gabiro?
GABIRO: Sijambo Usanase.
USANASE: Unaonekana mwingi wa huzuni. Pana jambo linalokutatiza?
GABIRO: Ni kweli. Ninataka kuandika barua kwa mjomba. Sijui endapo pana kanuni zozote ninazofaa kuzingatia.
USANASE: Ahaa! Zipo kanuni za kufuatwa wakati wa kuandika barua ya kirafiki.
GABIRO: Kanuni hizo ni gani?
USANASE: Kwanza, hufai kuandika kichwa.
GABIRO: Niandike tu moja kwa moja?
USANASE: Naam. Kabla ya kuandika kiini au mwili wa barua, hakikisha kuwa umeandika anwani yako kama mwandishi.
GABIRO: Anwani moja inatosha?
USANASE: Naam. Chini ya anwani, andika tarehe kisha umtambulishe unayemwandikia.
GABIRO: Ninaweza kumtambulisha vipi?
USANASE: Mtambulishe kwa kudhihirisha uhusiano uliopo baina yenu. Kwa mfano, *Kwa Mjomba Mpendwa*.
GABIRO: Ahaa! Ninakupata vizuri sana. Je, ninafaa kujikita katika ujumbe mmoja mkuu?
USANASE: Hapana. Una uhuru wa kuzungumzia maudhui mengi. Unaweza kutaja mambo mengi yasiyohusiana. Mfano, unaweza kumwambia kuhusu hali ya anga na masomo shuleni. Baadaye, unaweza kumwuliza kuhusu mazao yake yalivyo shambani na mambo mengi. Uhakikishe kuwa kila maudhui au ujumbe upo katika aya yake.
GABIRO: Ninafaa nitumie kiwango gani cha lugha?

USANASE: Hujafungwa katika kiwango fulani cha lugha. Lugha utakayotumia inategemea uhusiano uliopo kati yako na mjomba au yeyote unayemwandikia.

GABIRO: Kwa hivyo si lazima lugha yangu iwe rasmi?

USANASE: Naam. Si lazima uzingatie kiwango cha juu cha adabu kama ilivyo katika barua rasmi. Hilo halimaanishi kuwa unaruhusiwa kutumia lugha chafu au lugha isiyokuwa na tasfida.

GABIRO: Kwa hivyo ninaweza kutumia lugha yenye utani, vichekesho na yenye kuibua hisia ya huzuni, furaha au huruma.

USANASE: Naam.

GABIRO: Je, ninafaa kuzingatia urefu kiasi gani?

USANASE: Kama nilivyosema hapo mbeleni, una uhuru wa kuzungumzia mambo mengi utakavyo katika barua ya kirafiki. Urefu utategemea jumla ya mambo hayo. Una uhuru wa kuandika barua ndefu au fupi utakavyo. Hakuna urefu maalumu.

GABIRO: Nikimaliza, ninafaa kutia sahihi?

USANASE: La hasha! Barua ya kirafiki si lazima itiwe sahihi.

GABIRO: Asante sana rafiki yangu kwa maelezo hayo. Sasa ninaweza kuandika barua yangu.

USANASE: Karibu. Ukiwa na swali lingine, utaniuliza.

**Zoezi**

Jiunge na mwenzako na muigize mazungumzo yaliyopo hapo juu. Andikeni kanuni za kuzingatiwa katika uandishi wa barua za kirafiki zilizopo kwenye ufahamu.

***Kazi ya kikundi***

Jiunge na wanafunzi wenzako katika kikundi. Andikianeni barua za kirafiki kuhusu mada yoyote mpendayo. Someni barua zenu huku mkisahihishiana.

### b) Barua rasmi

Tazama michoro hii. Je, mwalimu na wanafunzi hawa wanajadiliana kuhusu nini? Je, unajua jinsi ya kuandika barua rasmi?



Barua rasmi ni barua zinazoandikiwa mtu au watu wenye nyadhifa kwa lengo maalumu la kuwasilisha ujumbe rasmi.

*Mifano ya barua rasmi*

***i) Barua ya kuomba kazi***

Hii ni aina ya barua ambayo mtu huandika wakati anapotaka kuajiriwa mahali. Kuna aina mbalimbali za barua za kuomba kazi.

***Kazi ya wanafunzi wawili wawili***

Jiunge na mwenzako. Jadilianeni kuhusu jinsi ya kuandika barua ya kuomba kazi. Andikeni barua hiyo kwa msingi wa majadiliano hayo.

*Mfano*

PAUL GATETE,
S.L.P. 2345-0022,
SIMU +2507345621876,
KIGALI.

7/8/2016.

KWA MKURUGENZI MKUU,
SHAMBA LA MIKAHAWA LA USANASE,
S.L.P. 3000,
RUHANGO.

Kwa Bi. Ituze,

MINT: KUOMBA NAFASI YA MENEJA WA UZALISHAJI

Narejelea tangazo katika Gazeti la Mkulima Bora, toleo la siku ya Ijumaa tarehe 8, Aprili, 2016, kuhusu kuwepo kwa nafasi niliyotaja hapo juu nikiomba nizingatiwe. Mimi ni Mnyarwanda na ninapenda sana kilimo hasa cha mikahawa. Kwa miaka zaidi ya kumi, nimekuwa nikijihusisha katika kuwahamasisha wanakijiji kuhusu mbinu bora za kuimarisha kilimo cha mikahawa. Kwa sasa, kijiji chetu kinaongoza katika uzalishaji wa mikahawa mingi yenye thamani ya juu zaidi.

Nimefanya utafiti kuhusu mbinu za kisasa za kuimarisha uzalishaji wa mikahawa na ninatumai kuwa maarifa niliyonayo yatakufaidi katika kukuza uzalishaji wa kahawa.

Natazamia mawasiliano kutoka kwako wakati wowote.

Wako mwaminifu,



Paul Gatete.

**Zoezi**

Andika barua ya kuomba kazi yoyote upendayo. Angazia mambo yafuatayo katika barua yako:

i) jinsi ulivyopata kuwepo kwa nafasi ya kazi hiyo,

ii) tajiriba yako, wasifu wako mfupi,

iii) sababu ya kutaka kazi hiyo,

iv) mambo mapya ambayo utafanya ukipewa nafasi hiyo na kadhalika.

### *ii) Barua ya kuomba ruhusa*

Hii ni aina ya barua ambayo mwandishi huomba kupewa fursa ya kutoshiriki katika shughuli fulani muhimu. Unaweza kusema kwa nini hutakuwepo au usiseme.

*Mfano*

JANE USANASE,
SHULE YA UPILI YA UFANISI,
S.L.P. 2345,
NYAMATA.

5/7/2016.

MWALIMU MKUU,
SHULE YA UPILI YA UFANISI,
S.L.P. 2345,
NYAMATA.
Kwa Bwana Umuliza,

MINT: KUOMBA RUHUSA

Ninaandika barua hii kukuomba ruhusa ya kutokuja shuleni siku ya Ijumaa. Hii ni kwa kuwa nitasafiri kwenda kumwona mama mzazi aliyelazwa hospitalini.
Ni mimi wako mwanafunzi,



Jane Usanase.

**Zoezi**

Mwandikie mwalimu wako barua ukiomba ruhusa yoyote. Mweleze sababu za kuomba ruhusa hiyo.

### *iii) Barua ya huduma*

Barua ya huduma ni aina ya barua ambayo humhitaji mtu, kundi la watu, shirika lisilo la kiserikali au idara ya serikali au kampuni kutoa huduma fulani katika jamii. Wakati mwingine huandikwa kutoa maoni kuhusu hatua ambazo jamii ingependa kuchukuliwa, kwa mfano, idara ya polisi ama hospitali kuweka visanduku vya

kupokea maoni kutoka kwa wananchi kuhusu namna wangependa kuhudumiwa kwa ubora zaidi.

***Mfano***

KUNDI LA VIJANA TUKUZE JAMII,
S.L.P. 3457,
MUKARANGE.
12/05/2016.

MKURUGENZI MKUU,
SHIRIKA LA MAISHA YA KESHO,
S.L.P. 8901,
KIGALI.
Kwa Bw/Bi,


<u>MINT: OMBI LA UFADHILI WA HUDUMA</u>

Vijana Tukuze Jamii ni muungano wa vijana wenye wanachama 40 wanaojihusisha na utafiti kuhusu changamoto zinazowakabili wakazi wa vijiji mbalimbali katika wilaya hii ya Mukarange na kupendekeza namna ya kuzikabili. Ni kutokana na tafiti hizi ndipo tunaomba ufadhili wa shirika lenu katika utoaji wa elimu kwa watu wazima ili waweze kusoma na kuandika.

Tungependa pia kutolewa kwa mafunzo ya kilimo kwa vijana ili kuwaepusha na uhalifu, matumizi ya dawa za kulevya na ufasiki ili wawe wenye manufaa katika jamii.

Ni matumaini yetu kwamba mtazingatia maombi yetu.

Wako mwaminifu,



Salome Abera,
Katibu Mkuu, Vijana Tukuze Jamii.

## *Kazi ya kikundi*

Jiunge na wanafunzi wenzako katika kikundi. Nyinyi ni vijana wanaojihusisha katika kufanya utafiti wa mbinu bora za kilimo katika wilaya yenu. Kipeni kikundi chenu jina na mchague katibu mkuu. Andikeni barua kwa shirika lolote linalojihusisha na kilimo katika eneo lenu. Elezeni shirika hilo kuhusu utafiti mliofanya wa kukuza kilimo katika wilaya yenu na msaada mnaohitaji kutoka kwao.

## Aina zaidi za barua rasmi

Mbali na mifano iliyotolewa, zipo aina zaidi ya barua rasmi. Barua hizo ni kama vile:

i) Barua ya kuomba nafasi katika shule fulani
ii) Barua ya kuomba msamaha
iii) Barua ya shukrani

iv) Barua ya malalamiko
v) Barua kwa mhariri
vi) Barua ya mapendekezo
vii) Barua ya uteuzi
viii) Barua ya kusimamishwa au kufutwa kazi.

### *Kazi ya wanafunzi wawili wawili*


Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Fanyeni utafiti kuhusu jinsi barua zilizotajwa hapo juu huandikwa. Kila mwanafunzi aandike mojawapo ya barua hizo kuhusu mada yoyote kisha amsomee mwenzake. Sahihishianeni.

## Sehemu kuu na kanuni za barua rasmi

Barua rasmi huwa na sehemu au muundo fulani maalumu kama ufuatao:

Anwani ya mwandishi
Tarehe
Anwani ya mwandikiwa
Mtajo/Kutaja mwandikiwa kwa heshima
Kichwa
Utangulizi/Kutajwa kwa kiini
Mwili wa barua
Hitimisho
Wako mwaminifu/mtiifu
Sahihi
Jina la mwandishi
Cheo cha mwandishi (ikiwa mwandishi anaandika kwa niaba ya shirika fulani, kikundi au kampuni)

***Soma mazungumzo haya na ujibu maswali chini yake.***



UMUHIRE: Mwenzangu, nieleze kuhusu jinsi ya kuandika barua rasmi.

NDOLI: Lazima uandike anwani yako na ile ya mwandikiwa. Anwani yako kama mwandishi huja juu. Unapoandika anwani ya mwandikiwa, ni sharti uandike cheo chake kwanza kabla ya kuandika jina na anwani ya kampuni chini ya cheo chake kama vile, 'MKURUGENZI MKUU, MWENYEKITI, MWALIMU MKUU' na kadhalika.

UMUHIRE: Baada ya anwani, ninaandika nini?

NDOLI: Unaandika ufunguzi wa barua kama vile *Kwa Mbunge Mheshimiwa, Kwa Mheshimiwa*, *Kwa Meneja Mkuu*, *Kwa Meneja, Kwa Mgeni wa Heshima* na kadhalika. Unaweza kuandika jina lake la pili baada ya *Bw* au *Bi*.

UMUHIRE: Naam! Kwa hivyo, baada ya kutambulisha mwandikiwa, ninaandika kichwa au vipi?

NDOLI: Naam, rafiki yangu. Kichwa hudokeza kiini cha kuandika barua yako. Unapoandika kichwa, unaanza kwa kutumia kifupisho *MINT*: au *KUH*:

UMUHIRE: *MINT* na *KUH* vinasimamia nini?

NDOLI: *MINT* husimamia *Mintaarafu* au *kwa mintaarafu ya*, *KUH* husimamia *kuhusu*. Kichwa au mada yako haifai kuzidi maneno sita isipokuwa pale ambapo pana lazima.

UMUHIRE: Ninapoanza kuandika mwili, ninafaa kusema nini?

NDOLI: Ikiwa ni barua ya kuomba kazi, ni vizuri uanze kwa kurejelea tangazo la kazi hiyo au jinsi ulivyopokea kuwepo kwa nafasi hiyo. Baadaye, andika moja kwa moja kiini cha barua hiyo.

UMUHIRE: Hakuna salamu?

NDOLI: Naam. Barua rasmi haina salamu. Unaeleza moja kwa moja kiini cha kuandika barua. Unafaa kujikita katika ujumbe mmoja mkuu, yaani jambo linalokufanya uiandike barua hiyo. Ikiwa unaomba kazi, toa maelezo muhimu kukuhusu. Maelezo hayo yawe na uhusiano na kazi unayolenga kupata. Epuka maelezo mengi yasiyokuwa na manufaa.

UMUHIRE: Lugha yangu inafaa kuwa ya namna gani?

NDOLI: Lugha yako sharti izingatie adabu ya hali ya juu na kiwango cha juu cha urasmi. Lugha yako iwe sahihi. Ikiwa unaandika kwa kalamu, tumia hati nadhifu. Usitaje chochote cha kuonyesha mambo au hisia za kibinafsi au uhusiano wa kibinafsi na unayemwandikia.

UMUHIRE: Nini huandikwa katika hitimisho la barua hii rasmi?

NDOLI: Unaandika tumaini lako la majibu mazuri. Chini yake, unaandika: *Wako Mwaminifu* au *Wako Mtiifu* kisha unaweka sahihi. Chini ya sahihi yako, andika jina lako kamili. Ikiwa unaandika kwa niaba ya shirika au kampuni au kikundi, andika cheo chako chini ya jina lako.

UMUHIRE: Asante kwa maelezo haya.

## Maswali

i) Je, barua rasmi ina kanuni zipi za kuzingatiwa?
ii) Linganisheni sehemu na kanuni za kuandika barua za kirafiki na zile za kuandika barua rasmi. Jadilianeni kuhusu tofauti zilizopo kati ya barua za kirafiki na barua rasmi.

## *Kazi ya kikundi*

Jiunge na wanafunzi wenzako. Tazameni mifano ya barua rasmi iliyotolewa na mingineyo. Jadilianeni kuhusu miundo ya barua hizo. Andikianeni barua rasmi kuhusu mada yoyote.

## B Matangazo mbalimbali




Tangazo ni mpangilio wa maandishi kwa mtindo maalumu kwa lengo la kupasha ama kupokeza ujumbe fulani wa kidharura au muhimu.
Zipo aina mbalimbali za matangazo:

### *i) Matangazo ya biashara*

Matangazo ya biashara ni maandishi ambayo yanalenga kutoa maelezo fulani kuhusu kitu, bidhaa, mahali au jambo kwa ajili ya kuwashawishi wasomaji kununua na kutumia bidhaa husika au

kuzuru mahali husika. Matangazo haya yanaweza pia kuwajulisha watu kuhusu bidhaa mpya zilizoingia sokoni au kuimarishwa kwa bidhaa zilizopo kwa sasa.

### *Kazi ya kikundi*

Jiunge na wanafunzi wenzako katika kikundi. Tajeni matangazo mbalimbali yaliyomo katika redio, televisheni, magazeti na vibango mbalimbali karibu na maeneo mnapoishi. Jadilianeni kuhusu jinsi istilahi au msamiati ulivyotumika katika matangazo hayo na malengo ya matangazo hayo. Je, istilahi hizo zimefaulu katika kuafikia malengo husika?

### *Mifano*

Ni sharti kujua kuwa matangazo hulenga kuwashawishi wanunuzi. Tazama mifano hii:

1. JE, UNATAKA KUONGEZA MAVUNO YAKO MARADUFU? JE, UNATAKA KUJIFUNZA MBINU ZA KISASA ZA KILIMO? BASI, JIPATIE NAKALA YAKO YA GAZETI LA *SAUTI YA MKULIMA* KILA WIKI. MKULIMA BORA HUSOMA *SAUTI YA MKULIMA*.
2. ZURU MBUGA YA KITAIFA YA VOLCANOES LEO UFURAHIE UHONDO WA MAISHA. PATA FURSA YA KIPEKEE YA KUWAONA WANYAMA WA PORINI KATIKA MBUGA HII YA VOLCANOES.
3. 




***Maelezo zaidi kuhusu Hoteli ya Sabyinyo***

Hoteli hii imo katika mazingira ya kuvutia chini ya milima ya Virunga. Inajivunia kuwa na vyumba starehe na vyombo vya kisasa vya burudani.

Utafurahia mandhari ya kuvutia iliyopambwa na vilima vidogo vidogo na mipasuko mirefu kwenye ardhi. Mandhari haya ya kufana yatakupa fursa ya kipekee ya kujiburudisha.

Isitoshe, utapata nafasi ya kushiriki katika kutembea kwenye vilima kuwaona nyani wanaoishi vilimani.

***Jinsi ya kufika huko***

Unaweza kusafiri angani kwa ndege hadi uwanja wa ndege wa Gisenyi. Hapo, waajiri wetu watakupokea kwa tabasamu na unyenyekevu.
Ikiwa una gari, pitia barabara kuu ya Kaskazini Magharibi kutoka jijini Kigali. Itakuchukua saa tatu pekee.

Tembelea hoteli ya Sabyinyo leo upate uhondo wa burudani.

### *Kazi ya wanafunzi wawili wawili*

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Someni tena matangazo yaliyopo hapo juu kwa makini huku mkitambua sifa na miundo ya matangazo hayo.

## Sifa na miundo ya matangazo ya biashara

***Soma kifungu hiki na ujibu maswali chini yake.***

Matangazo ya biashara huwa na utangulizi wenye mvuto na hitimisho lenye ushawishi. Kumbuka kuwa lengo kuu la tangazo lolote la biashara ni kuwavutia wasomaji.

Yapo matumizi ya takriri. Takriri ni kurudiarudia neno au maneno fulani. Kwa kuwa matangazo ya biashara hulenga kutambulisha bidhaa fulani au mahali fulani, bidhaa au mahali husika hurudiwarudiwa katika mwili wa tangazo ili wasomaji au wateja lengwa wazikumbuke. Pia, jina la bidhaa na kampuni hutajwa na kurudiwarudiwa.

Watu hupenda sana kusoma maneno mafupi na ni rahisi kuyakumbuka. Maneno marefu kwa upande mwingine huchosha na huchukua nafasi kubwa. Matangazo ya biashara huandikwa kwa maneno mafupi mafupi yenye mnato na ujumbe mzito. Maneno mafupi hupunguza gharama ya matangazo hayo.

Katika matangazo ya biashara kwenye redio na televisheni, matangazo hayo huambatana na sauti ya kimuziki. Sauti hiyo hulenga kuwavutia wanaosikiza matangazo hayo. Pia, huchangia katika kupitisha ujumbe uliokusudiwa.

Wakati mwingine, matangazo hufuata mtindo wa dayalojia. Hapa, watu wanaohusika katika kutangaza bidhaa fulani huulizana maswali na kupashana ujumbe. Kwa mfano

MTU I: Je, umejaribu sabuni hii?
MTU II: Bado
MTU I: Ijaribu leo. Hii ndiyo suluhisho ya kudumu kwa madoa sugu.

Matangazo ya biashara pia hutumia lugha ya kushawishi. Lugha hiyo huwa sahihi au hukosa usahihi. Lugha inayotumika hutegemea umri, jinsia ya wanunuzi wanaolengwa.

Matangazo ya biashara hueleza ubora wa bidhaa pekee na manufaa yake. Hutilia mkazo mambo haya kwa undani na wakati mwingine hutilia chumvi ubora na manufaa ya bidhaa husika.

Matangazo mengi ya biashara hayataji bei ya bidhaa. Pia, hueleza zinakopatikana bidhaa zenyewe au jinsi ya kuzipokea mahali unapoishi. Wakati mwingine, hutoa mwito wa kutembelewa kampuni husika.

**Zoezi**

1. Taja sehemu kuu za matangazo ya biashara kwa mujibu wa kifungu na matangazo ya biashara uliyosoma au kusikia.
2. Taja kanuni au sifa kuu za kuzingatiwa katika uandishi wa matangazo ya biashara.

***Kazi ya kikundi***

Jiunge na wanafunzi wenzako katika kikundi. Fanyeni mradi wa kuandika matangazo mbalimbali ya biashara kuhusu bidhaa mtakazojichagulia.

### *ii) Matangazo ya mkutano*

Katika matangazo haya, mwandishi hutaja kiini au ajenda za mkutano, mahali pa mkutano, tarehe na wakati ambapo mkutano utaandaliwa na maelezo mengine muhimu.

*Mfano*

TANGAZO!!!

MKUTANO WA WANAKIJIJI

Wanakijiji wote mnatangaziwa kwamba siku ya hotuba ya Bwana Borafya itakuwa Jumamosi tarehe 28-03-2016 saa nne za asubuhi. Wanakijiji wote mnatarajiwa kuwa mmefika wakati huo ili tuanze mkutano kwa wakati unaohitajika.

Bwana Borafya atalizungumzia suala la ugonjwa wa sokota.
Nyote mnakaribishwa.

### *iii) Matangazo kuhusu ziara ya rais*

Ziara ni tendo la kwenda mahali kwa sababu fulani kama vile kuzindua ujenzi wa barabara, kuwahutubia wananchi na kadhalika. Nalo tangazo lake linaweza kuwa kama hili lifuatalo:

*Mfano*

Tangazo! Tangazo!

ZIARA YA MTUKUFU RAIS

Wakazi wote wa mji mkuu huu wa Ikeza wanatangaziwa ya kwamba Mtukufu Rais wa nchi yetu atauzuru mji huu wetu kutoka tarehe 07-10-2016 hadi tarehe 14-10-2016. Kwa hivyo, nyote mnahimizwa kujitokeza kwa wingi kumpokea na kumkaribisha Mtukufu Rais.

Halmashauri ya Usimamizi wa Mji.

Napo hapa, unaona kuwa mara nyingi matangazo kama haya hayatoi habari kwa mjazo wake bali hualika tu nia ikiwa kwamba ufike pale ujionee mwenyewe.

**Zoezi**

Liandike tangazo kwa watu wote waliomo shuleni mwenu kuhusu ziara ya waziri wa elimu shuleni humo. Liandike tangazo hilo kwa niaba ya mwalimu mkuu.

### *iv) Matangazo ya kuwachagua watu kujiunga na kikosi cha polisi*

Huweza kutokea kwamba serikali inataka kuchagua watu kujiunga na kikosi cha polisi. Basi, huweza kulitangaza jambo kwa wananchi.

*Mfano*

IDARA YA POLISI,

2/6/2016.

KUJIUNGA NA KIKOSI CHA POLISI

Idara ya Polisi inawatangazia kuhusu majaribio ya kujiunga na kikosi cha polisi kuanzia tarehe 14/07/2016 hadi tarehe 28/07/2016 katika makao makuu yote ya tarafa. Wake kwa waume wanaopenda kushiriki katika majaribio haya sharti watimize masharti yafuatayo:

i) Awe Mnyarwanda,
ii) Awe na ari ya kuhudumia nchi yake,
iii) Awe na miaka kati ya 18 na 25,
iv) Awe na cheti cha kidato cha sita (6),
v) Awe mtu mwadilifu,
vi) Asiwe na rekodi ya kutumikia kifungo cha gereza kwa zaidi ya miezi sita,
vii) Awe na cheti cha Diploma au cheti chenye kiwango hicho,
viii) Awe mkakamavu na mwenye afya nzuri na athibitishe hili kwa cheti cha ukaguzi wa daktari aliyeidhinishwa/kusajiliwa na serikali,
ix) Asiwe na rekodi ya uhalifu,
x) Aweze kupita mtihani wa kusajiliwa watakaopewa.

Wanyarwanda wote waliotimiza masharti haya wanakaribishwa.

Idara ya Polisi.

## *Kazi ya wanafunzi wawili wawili*

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Someni tangazo lililopo hapo juu na matangazo mengineyo ya mikutano. Jadilianeni kuhusu sehemu muhimu za matangazo ya mikutano na kanuni za kuzingatiwa katika uandishi wa matangazo maalumu.

### *v) Matangazo kuhusu nafasi za kazi*

Hutolewa kwa lengo la kufahamisha watu kuhusu kuwepo kwa nafasi fulani ya/za kazi katika kampuni, shirika ama idara fulani.

*Mfano*

HALMASHAURI YA WILAYA YA NYAGATARE
Tarehe 3/07/2016.
NAFASI ZA KAZI
Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyagatare anatangaza kuwepo kwa nafasi zifuatazo za kazi:

1. MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA (Nafasi 1)

**Sifa za Mwombaji kazi**

Ni sharti awe:

i) mkazi wa muda mrefu wa Wilayani Nyagatare,
ii) na shahada ya uzamifu katika usimamizi,
iii) mwenye umri wa miaka 35 au zaidi,
iv) na tajiriba ya miaka 5 katika kusimamia watu katika shirika kubwa tajika,
v) na rekodi nzuri ya utendakazi,
vi) mwenye uwezo wa kuwatia motisha wafanyakazi ili kuinua hadhi ya bodi hii,
vii) mtu mwenye kutoshawishika katika misimamo sahihi yake na ile ya halmashauri.

**Wajibu na majukumu**

i) Kutangaza nafasi za ajira,
ii) Kupendekeza kupandishwa vyeo kwa wafanyakazi,
iii) Kutoa mafunzo au maelekezo kwa waajiriwa wapya,
iv) Kupendekeza nyongeza ya mishahara kwa wafanyakazi,
v) Kutekeleza majukumu mengineyo kama itakavyopendekezwa mara kwa mara.

**Kiwango cha mshahara**

Kitajadiliwa wakati wa mahojiano.

2. MAAFISA WA UCHUKUZI DARAJA LA II ( Nafasi 5)

**Sifa za mwombaji kazi**

Ili kufuzu katika nafasi hii, unahitajika kuwa na:

i) shahada katika masuala ya usimamizi wa kibiashara,
ii) tajiriba ya miaka 3 katika kitengo hiki,
iii) uelewa wa masuala ya uchukuzi katika forodha na kanuni za barabara,
iv) rekodi nzuri ya utendakazi,
v) ufahamu wa matumizi ya kompyuta na mtandao.

**Majukumu**

i) Kutayarisha bajeti na kuendesha uchukuzi,
ii) Kuhakikisha kuwa takwimu, stakabadhi na kumbukumbu zinazohusu vyombo vya usafiri pamoja na mitandao yake zinatunzwa vyema,

iii) Kukusanya na kuandaa takwimu kuhusu maendeleo ya sekta ya uchukuzi na kuziwasilisha kwa wadau ndani na nje ya wilaya,
iv) Kuweka faili za uchukuzi nchini,
v) Kukadiria na kushauri juu ya utendaji wa miradi mbalimbali ya sekta ya uchukuzi.

**Kiwango cha mshahara**

Kitajadiliwa wakati wa mahojiano.

Ikiwa una sifa hizi na ungependa kujiunga nasi, tuma barua ukionyesha kazi unayoomba na uambatanishe wasifukazi wako wa hivi karibuni, nambari ya/za simu na warejelewa watatu kwa mawasiliano wakati wa mchana. Tuma kwa anwani hii kabla ya usiku wa manane ya tarehe 23/08/2016.

J.M. Gatete,

Halmashauri ya Wilaya ya Nyagatare,

S.L.P. 3013,

NYAGATARE.

### Tanbihi

Halmashauri hii ni huru katika utoaji wa nafasi sawa za kazi bila kubagua yeyote.

Ombi litakataliwa moja kwa moja endapo anayeomba kazi atahonga afisa yeyote kwa ajili ya kupendelewa.

### Zoezi

Tafuta matangazo mbalimbali kuhusu nafasi za kazi katika magazeti, mabango na kadhalika. Soma matangazo hayo na ubainishe sifa zayo na kanuni zilizozingatiwa katika uandishi huo.

### *Kazi ya kikundi*

Jiunge na wanafunzi wenzako katika kikundi. Huku mkirejelea matangazo mbalimbali, jadilianeni kuhusu tofauti zilizopo katika matangazo hayo mkizingatia:

i) sifa
ii) sehemu kuu
iii) kanuni
iv) msamiati
v) malengo

## C Ilani

Ilani ni tangazo ambalo hutahadharisha au kuarifu kuhusu aina ya jambo ama tukio ambalo linastahili kuepukwa, lau sivyo madhara hutokea.

Ilani huwa na wazo moja tu maalumu. Hutolewa mahali penye shughuli nyingi ama palipo na watu wengi kama vile shuleni, chuoni, kanisani msikitini na kadhalika.




Ilani mara nyingi huwa na mtindo rasmi. Ilani nyingi huwekwa katika mabango makubwa, magazetini, kwenye majarida na kadhalika.

*Mifano*

***i) Ilani kuhusu mkurupuko wa ugonjwa***

ILANI
WIZARA YA AFYA, KUPITIA HOSPITALI KUU YA MKOA, INAWATANGAZIA KUZUKA KWA UGONJWA HATARI WA KIPINDUPINDU.
WATU WOTE WANASHAURIWA KUZINGATIA USAFI WA MWILI NA MAZINGIRA.
ILI KUJIKINGA KUTOKANA NA MAAMBUKIZI YA UGONJWA HUU HATARI, MAMBO YAFUATAYO NI SHARTI YAZINGATIWE:

i) KILA MTU AHAKIKISHE ANATUMIA CHOO.
ii) KILA MTU ANAWE MIKONO KWA MAJI SAFI NA SABUNI BAADA YA KUTOKA CHOONI.
iii) HAKIKISHA UNAKULA KATIKA MAHALI SAFI
iv) WATU WASILE KWENYE MIKAHAWA.
v) ALIYE NA DALILI ZA KUENDESHA NA KUTAPIKA AKIMBIZWE MARA MOJA HOSPITALINI KWA UCHUNGUZI NA MATIBABU.
vi) ALIYEAMBUKIZWA APEWE MAJI MENGI YA KUNYWA WAKATI ANAPOPELEKWA HOSPITALINI.
vii) KILA MTU ACHEMSHE MAJI YA KUNYWA.
viii) MTU YEYOTE ALIYEAMBUKIZWA ATENGWE NA WATU WENGINE.

ONYO:

MTU YEYOTE ATAKAYEPATIKANA AKIUZA CHAKULA KATIKA MAENEO WAZI ATASHTAKIWA.

*ii) Ilani kuhusu unywaji wa pombe*

*Mfano*

POMBE HATARI

Serikali, kupitia wizara ya afya, inawatahadharisha wananchi kuhusu kuzuka kwa pombe hatari ya SUMEDA inayonywewa sana katika sehemu mbalimbali nchini. SUMEDA ni pombe hatari kwa afya yako kwa kuwa inatengenezwa kwa kutumia dawa ya kuhifadhi maiti na kemikali nyingine hatari.

Pombe hii hatari imesababisha vifo vya watu zaidi ya 50, kuwapofusha wengine wengi pamoja na kutoa mimba.

Atakayepatikana akiuza ama kunywa aina hii ya pombe atakamatwa.
Ofisi ya mkuu wa wilaya.

*iii) Ilani ya kutokanyaga nyasi*

*Mfano*

ILANI
HAPANA RUHUSA KUKANYAGA NYASI
NA MENEJIMENTI

**Zoezi**

i) Tazama mifano ya ilani zilizotolewa hapo juu. Je, ilani hizo zina sifa gani?
ii) Andika ilani kuhusu mada yoyote upendayo.

***Kazi ya wanafunzi wawili wawili***

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Andikeni ilani kuhusu mada hizi na mziweke kwenye maeneo husika shuleni.

i) Kutokanyagwa kwa sehemu fulani zenye nyasi.
ii) Kuwepo kwa mjadala kuhusu: mbinu za kisasa za kilimo ni bora kuliko mbinu za jadi za kilimo.
iii) Kuwafahamisha wanafunzi kunawa mikono watokapo msalani.
iv) Kuzingatia usafi jikoni

## D Mialiko

Mwaliko ni mwito wa kumtaka mtu au watu kuhudhuria shughuli au hafla fulani. Wito wa namna hii huweza kufanywa kwa njia ya barua ya kirafiki au barua rasmi na hata kwa matangazo.

## Kazi ya kikundi

Jiunge na mwanafunzi mwenzako na mchunguze mchoro huo uliopo hapo chini. Jadilianeni kuhusu mambo yaliyomo ubaoni.




*Mifano ya mialiko*

### *i) Mwaliko wa harusi*

*Je, umewahi kualikwa katika harusi au kuona kadi ya mwaliko wa harusi? Je, mwaliko huo ulikuwa na mambo gani?*

Mwaliko wa harusi huwaomba jamaa na marafiki kuhudhuria sherehe ya harusi. Kadi za mialiko ya harusi huchukua miundo na sura tofautitofauti. Miundo ya kadi hizo hutegemea ubunifu wa anayeziunda au mapendekezo ya maarusi au waandalizi wa harusi.

## Kazi ya kikundi

Jiunge na wanafunzi wenzako. Tazameni mialiko ya harusi iliyotolewa hapa chini. Jadilianeni kuhusu mambo yaliyomo katika mialiko hiyo.

*Mfano*

**A.**



**B.**



*"...Nilimshika na sikumwachia aende hadi nilipomleta katika nyumba ya mama yangu..."*

*Bwana na Bi Paulo na Maria Butera*
*Wanaomba uhudhurie harusi ya binti yao*
*Gwiza*
*na*
*Habineza*
*Mwanawe*
*Bwana na Bi Yosefu na Maria Nkusi*
*Jumamosi, 5/8/2016*
*Kuanzia saa nane alasiri*
*katika*
*Kanisa la Kikatoliki la Utakatifu*
*N34 barabara ya kanisa*
*Jijini Upendo.*

## Kanuni za kuzingatiwa katika uandishi wa mwaliko wa harusi

Unapoandika mwaliko wa harusi, ni sharti utaje majina ya watu wanaofunga ndoa, tarehe ya harusi, mahali pa harusi na wakati sherehe itakapoanza.

Watu mbalimbali huandika mialiko ya harusi kwa njia tofauti tofauti. Mara nyingi, kadi hutumika. Wao hurembesha kadi za harusi ili kuwavutia wasomaji na kuonyesha mapenzi yaliyopo kati ya maharusi. Wengine hunukuu maandiko takatifu yanayotaja mapenzi na ndoa. Almuradi, kila mwaliko wa harusi huwa na umbo lake maalumu.

### *Kazi ya kikundi*

Jiunge na wanafunzi wenzako na mchukulie kuwa nyinyi ni wanachama wa kamati inayoandaa harusi. Mna nia ya kutengeneza kadi nzuri ya mwaliko wa harusi. Kila mmoja achore kadi ya mwaliko na aweke ujumbe wake. Linganisheni mialiko yenu na mchague mwaliko bora zaidi kisha muufanye urembeke zaidi. Onyesheni na mlisomee darasa zima kadi yenu.

### *ii) Mwaliko wa kutembelea mbuga ya wanyama*

Mwaliko kama huu huchukua umbo la barua rasmi.

*Mfano*

Chuo cha Walimu cha Rukara,
S. L.P. 0020,
KAYONZA.
12/7/2016.

Mwenyekiti,
Halmashauri ya Wasimamizi wa Chuo,
S. L.P. 0020,
KAYONZA.

Kwa Bi Mwenyekiti,

KUH: KUZURU MBUGA YA WANYAMA YA AKAGERA

Mwalimu mkuu, walimu, pamoja na wanafunzi wote wa chuo hiki wanakuomba uandamane nao katika safari yao ya kielimu kuzuru Mbuga ya kuhifadhia Wanyama ya Akagera.
Twakuomba pia utujulishe mapema kama hili litawezekana ama la.

Wako mwaminifu,



Johana Nziza,

Kamati ya Usimamizi.

### *iii) Mwaliko wa maonyesho ya vitabu*

***Mfano***

Chama cha Wachapishaji Vitabu,
S. L. P. 1111,

MUSANZE.

1/7/2016.

Mkurugenzi Mkuu,
Shirika la Uchapishaji Vitabu la Kigali,
S.L. P. 1001,
KIGALI.

Kwa Bwana Musoni,

MINT: MAONYESHO YA VITABU

Chama cha Wachapishaji Vitabu kinakualika kuhudhuria maonyesho yetu ya kila mwaka ya vitabu yatakayoandaliwa kuanzia tarehe 14 hadi 18 Septemba mwaka huu katika ukumbi wa Hoteli ya Banjunkara.

Unaombwa kutuma barua ya kuthibitisha kushiriki kwako pamoja na faranga 50, 000 kufikia tarehe 30/7/2016 ili utengewe nafasi yako.
Utapata fursa ya kuonyesha vitabu vyako vipya na vinginevyo ili vipate kujulikana na kununuliwa kwa wingi. Pia, utapata nafasi ya kutangamana na waandishi mbalimbali watakaohudhuria maonyesho hayo.

Ni mimi wako mwaminifu,



Cleah Klarenzi,
Mkurugenzi Mkuu,
Chama cha Wachapishaji Vitabu.

**Zoezi**

i) Soma tena barua za mialiko hapo juu. Taja mambo muhimu yaliyozingatiwa katika uandikaji wazo.
ii) Mwandikie aliyekuwa mwalimu wako barua ya kumwalika kwenu kwa sherehe ya kukuaga kwa safari ya kwenda ng’ambo kusoma.

**Zoezi la ziada**

Andika barua za mialiko kuhusu mada yoyote.

## E Aina za alama za uandishi na matumizi yake

Wenzetu wanapozungumza, tunaweza kutambua wanapomaliza usemi wao kwa kusikia sauti zao. Lakini katika uandishi, hakuna sauti. Badala ya sauti, zipo alama za uandishi ambazo hutumiwa kuwakilisha sauti katika uandishi. Kutokana na alama hizo, tunatambua kama usemi umekwisha, kuulizwa swali, kushangaa na kadhalika. Pia, tunaposoma, tunajua wapi tunafaa kupumua kidogo, kushusha au kupandisha sauti na kadhalika.

Alama hizi huitwa viakifishi. Hivyo basi, viakifishi ni alama zinazotumiwa katika maandishi ili kuleta maana ikusudiwayo katika matini mbalimbali kama vile sentensi, aya, mtungo, barua, mialiko, matangazo, ilani na kadhalika.

### Aina za viakifishi

**Nukta (.)**

a) Huwekwa mwishoni mwa sentensi. Kwa mfano:
   *i) Nimechoka.*
   *ii) Waziri mkuu wa Uchina amewasili mjini Kigali.*
b) Hutumiwa kuonyesha ufupisho wa maneno. Kwa mfano:
   *i) S.L.P. – Sanduku la Posta*
   *ii) Bi. – Bibi*
c) Hutumika kubainisha saa na dakika au tarehe. Kwa mfano:
   *i) 3.20 – saa tisa na dakika ishirini*
   *ii) 14.5.2016- tarehe kumi na nne, mwezi wa tano, mwaka wa elfu mbili na kumi na sita*
d) Hutumiwa kuonyesha vipashio vya pesa. Kwa mfano:
   *Sh. 10.50 – shilingi kumi na thumuni hamsini*
e) Zikitumiwa mara tatu mfululizo (...), huonyesha kutokamilika kwa sehemu husika. Kwa mfano:

*Nitakupa lakini ni sharti...*

**Mkato/koma ( , )**

a) Hutumiwa kuonyesha pa kutua kwa muda mfupi katika sentensi. Kwa mfano:
   *i) Nilipowasili nyumbani, nilienda kuteka maji kisimani.*
   *ii) Kwa kuwa tulijiandaa vilivyo kwa mtihani wa kitaifa, tulipita.*

b) Hutumiwa kutenga maneno yaliyo katika orodha:
   *i) Kwenda sokoni ununue mboga, nyama, mafuta, na unga.*
   *ii) Mwanafunzi huyu ni mtiifu, mwerevu, mtanashati, na mwenye bidii.*

c) Hutumiwa kubainisha sehemu mbili za sentensi zilizo kinyume:
   *i) Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.*
   *ii) Aliniambia atakuja, hakuja.*

d) Hutumiwa kabla ya alama za mtajo. Kwa mfano:
   *Mama akasema, "Niletee chumvi."*

e) Hutumiwa wakati sentensi inapoanza kwa kiunganishi. Kwa mfano:
   *Kweli, alikuwa mtu mwovu.*

f) Hutumiwa unapoita mtu ili kupata usikivu wake kabla hujamwambia chochote. Kwa mfano:
   *Nkusi, niletee kalamu.*

g) Hutumiwa unapokubali au unapokataa kitu. Mfano:
   *i) Ndio, nitakuja.*
   *ii) Hapana, sitakulipa.*

**Nukta mbili/koloni (:)**

a) Hutumiwa kutanguliza maneno yaliyo katika orodha.

*Kwa mfano:*

   *i) Nenda kaniletee: kalamu, karatasi na kifutio.*
   *ii) Amenunua: machungwa, sukari, na ndizi.*

b) Hutumiwa kuashiria maneno ya msemaji badala ya alama za mtajo hasa katika uandishi wa mazungumzo au tamthilia.
   *i) Mama: Lazima uniambie ulikokuwa tangu jana.*
   *ii) Mwalimu alisema: Ingieni darasani.*

c) Hutenganisha numerali za saa.

*Kwa mfano:*

   *4:10 – saa kumi na dakika kumi*

**Nukta na kituo (;)**

a) Hutumiwa kuunganisha vishazi vikuu bila kutumia kiunganishi. Kwa mfano:
   *Sikwenda Kayonza; nilienda Kirehe.*

b) Hutumiwa kumpumzisha msomaji katika sentensi iliyo ndefu ili apumzike zaidi kuliko pale inapotumiwa koma. Kwa mfano:
   *Alipofikiri sana, alitanabahi kuwa hakikuwepo cha kutorokwa; yeye angeweza kuondoka nyumbani au kumwacha mumewe, aende popote kufanya lolote.*

**Kistari kifupi (-)**

a) Hutumiwa kuonyesha kuwa neno linakatwa kwa vile limefika ukingoni mwa mstari husika na bado linaendelea katika mstari unaofuatia.
*Tanbihi*: Neno la silabi moja halikatwi.

b) Hutumiwa kuunga maneno yanayojenga neno moja. Mtindo huu aghalabu hujitokeza katika maneno yenye asili ya kigeni. Kwa mfano:
*i) Idd-el-Fitri*
*ii) Dar-es-Salaam*

c) Huweza kutumiwa badala ya koma. Kwa mfano:
*Nyimbo za asili-hasa rumba-zinapendwa na wengi.*

**Alama ya mshangao (!)**

Hutumiwa kuashiria mahangaiko ya moyo kama vile hasira, hofu, mshangao na kadhalika.

*i) Lo! Mwanafunzi ameangusha kitabu cha mwalimu matopeni.*
*ii) Wamefungwa mabao kumi kwa nunge!*

**Alama ya kuulizia/kiulizi (?)**

a) Hutumiwa mwishoni mwa sentensi kuonyesha kuwa sentensi hiyo ni swali.

*Mwa mfano:*

*Unaitwa nani?*

b) Hutumiwa kuonyesha ukosefu wa uhakika kuhusu jambo kama vile mwaka. Kwa mfano:
*Shule hii ya Tumaini ilianzishwa 1992 (?)*

**Mabano/parandesi ( )**

a) Hutumiwa kufunga maneno ya ziada katika sentensi. Kwa mfano:
*Nyamata (makao makuu ya Bugesera) inakua kwa kasi.*

b) Hutumiwa mwandishi anapotaka kutoa ufafanuzi kwa lugha nyingine tofauti na ile anayoitumia.
Kwa mfano: *Walowezi (settlers) walifukuzwa.*

c) Hutumiwa kufungia herufi za kuorodhesha. Kwa mfano:
*(a) huelimisha, (b) huburudisha, (c) huonya.*

**Mkato (/)**

Hutumiwa kuonyesha kuwa mojawapo ya vitu vilivyotajwa chaweza kutumiwa badala ya hivyo vingine.
Tazama: *Abera alishangaa/aliduwaa*

**Mtajo: (“ ” au ‘ ’)**

Hutumiwa kuonyesha maneno halisi ya mzungumzaji. Kwa mfano:
*“Nitafika kesho jioni,” alisema mdogo wake.*

**Herufi kubwa (H)**

a) Hutumiwa kuanzishia sentensi:
*Nilikuona jana.*

b) Hutumiwa kuanzia majina ya pekee:
*Rwanda, Mwenyezi Mungu.*

c) Hutumiwa kuandikia anwani:
*JINSI YA KUPANDA MITI*

**Herufi ndogo (h)**

Hizi ndizo alama za uandishi zinazotumiwa sana kuliko nyingine zote. Hutumiwa kila baadaya herufi kubwa.
*Mama anapika.*

### Zoezi

***Kiakifishe kifungu kifuatacho***

Ilikuwa asubuhi na mapema bw butera alipotoka kwake kwenda kazini fikirani mwake alijikumbusha pindi nikifika ofisini nitaomba ruhusa niende nimlipie binti yangu karo

aliabiri gari linaloelekea ruhango baada ya mwendo mfupi tu lo gari hilo lilipata ajali liligongana na lori japo ng'ombe waliokuwemo njiani walikufa takriban wote abiria walipata majeraha madogo madogo lakini ililazimu wapelekwe hospitalini hivyo butera hakutimiza azma yake

## Mazoezi ya ziada

### Zoezi A

Andika kifungu cha habari kuhusu mada yoyote ukitumia alama za uandishi kwa usahihi.

### Zoezi B

Jiunge na mwanafunzi mwenzako na msome vifungu mbalimbali vya habari vilivyomo katika kitabu hiki, magazeti, na vitabu vinginevyo. Bainisheni na kuainisha alama mbalimbali za kuakifisha zilizotumika na jinsi zilivyotumiwa.

## Maswali ya marudio

1. Eleza maana ya barua ya kirafiki.
2. a) Taja watu watano wanaoweza kuandikiwa barua ya kirafiki.
   b) Mwandikie mmoja wa hao uliowatajia barua ya kirafiki.
3. Zitaje sehemu zote kuu za barua ya kirafiki huku ukizieleza.
4. Eleza maana ya barua rasmi.
5. Taja aina tano za barua rasmi.
6. Mwandikie Mwalimu Mkuu wa shule ya msingi ulikosomea ukiomba nafasi ya kufunza katika shule hiyo.
7. Zitaje sehemu kuu za barua rasmi.

8. Eleza kanuni za kuzingatiwa wakati wa kuandika barua rasmi.
9. Eleza tofauti zilizopo kati ya barua rasmi na barua ya kirafiki.
10. Kwa maneno yako mwenyewe, eleza tangazo ni nini.
11. Ipo tofauti gani kati ya matangazo na barua rasmi?
12. Eleza tofauti kati ya tangazo la tanzia na tangazo la mkutano.
13. a) Ilani ni nini?
    b) Andika ilani utakayoweka msalani ili kuwatahadharisha wanafunzi wenzako kuhusu madhara ya kutonawa mikono baada ya kutoka msalani.
14. a) Eleza sifa za matangazo ya biashara.
    b) Andika tangazo la biashara kuhusu bidhaa upendayo.
15. Eleza umuhimu wa mwaliko.
16. Je, kuakifisha ni kufanya nini?
17. Eleza umuhimu wa uakifishaji.
18. Yataje kwa mifano matumizi matano ya nukta.
19. a) Eleza maana ya mtajo.
    b) Andika mifano miwili ya matumizi ya mtajo.
20. Eleza kwa ufupi mambo muhimu uliyojifunza katika sura hii. Taja jinsi mambo hayo yatakavyokusaidia na kuisaidia jamii yako.

# 3 Mada kuu: Matumizi ya lugha katika mazingira mbalimbali

## Mada ndogo: Rejesta za mpira na burudani

### A Rejesta mbalimbali nchini Rwanda

Rejesta au sajili ni lugha inayotumiwa mahali ama katika hali fulani na wala haiwezi kuhamishwa kutoka mazingira yale na kutumiwa katika mahali pengine. Lugha hizi hutofautiana kwa misingi ya msamiati, muundo wa sentensi na kadhalika. Kutokana na tofauti hizi, tunapata rejesta za aina mbalimbali. Baadhi ya rejesta hizo ni kama hizi zifuatazo.

#### i) Rejesta ya mpira wa miguu

Mpira wa miguu pia huitwa kandanda, soka au kambumbu. Huu ni mchezo maarufu sana hapa nchini Rwanda na duniani kote. Kwa mfano, mashindano ya kombe la dunia hutazamwa na watu wengi sana kote duniani. Mashindano hayo huandaliwa kila baada ya miaka minne. Pia, yapo mashindano ya Bara la Afrika, Kombe la Kagame, ligi mbalimbali na kadhalika.

Baadhi ya watu hufuatilia mechi mbalimbali kupitia redio au televisheni. Wapo wanahabari ambao hutangaza mpira kupitia vyombo hivyo. Rejesta ya mchezo hujitokeza kupitia matangazo hayo.

**Kazi ya wanafunzi wawili wawili**

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Tazameni mchoro huu. Jadilianeni kuhusu yaliyomo michoroni na myahusishe na mazingira yenu.



***Soma kifungu hiki na ujibu maswali chini yake.***

**Matangazo ya kandanda sehemu I**

Hujambo msikilizaji. Karibu katika matangazo haya ya moja kwa moja ya kabumbu. Ni mimi mtangazaji wako, Teta. Huu ni mchuano wa fainali ya kuwania kombe la Fahari ya Rwanda kati ya shule ya wasichana ya Elimu Bora na Tusonge Mbele. Timu hizi mbili ni wapinzani sugu tangu jadi. Elimu Bora inajivunia historia nzuri kwa kushinda kombe hili mara kumi. Wao ndio bingwa tetezi. Tusonge Mbele imeshinda kombe hili mara tatu. Mwaka jana walitimuliwa katika nusu fainali. Katika awamu hii, wana rekodi ya kutoshindwa katika mechi zote hadi kufikia fainali. Je, rekodi hiyo itavunjwa na Elimu Bora?

Naona timu zote mbili zikiingia uwanjani tayari kwa pambano. Kwa sababu ya muda sitataja majina ya wachezaji wote. Nitayataja kadri wanavyozidi kucheza. Kwa ufupi, kila timu ina golikipa mmoja. Elimu Bora wameweka wachezaji watatu katika safu ya ulinzi nao Tusonge wanawachezesha wachezaji wanne katika safu hiyo hiyo. Timu ya Elimu Bora wametia wachezaji watano katika kiungo cha kati nao Tusonge wanawachezesha wachezaji watatu. Elimu Bora wana washambulizi wawili nao Tusonge wana washambulizi watatu katika safu ya mashambulizi. Timu zote mbili zina wachezaji wa akiba watano. Refa mkuu anapuliza kipenga nao wasaidizi wake wawili wanakimbia pembeni mwa uwanja kuinua kijibendera. Mmoja anakimbia kushoto naye mwingine anakimbia kulia.

Manahodha wa timu zote mbili wapo pale katikati ya uwanja kurusha sarafu ili kuamua timu inayoanzisha mpira. Mashabiki wa timu zote mbili wanaimba nyimbo za kushangilia timu zao. Nao makocha wao wamekaa pembeni mwa uwanja kushuhudia wasichana wao wakimenyana.

Naam, refa anapuliza kipenga. Mpira unaanzishwa pale na Ikirezi na Uwamwiza wa timu ya Elimu Bora. Ikirezi anapiga pasi kwake Gwiza. Gwiza anapiga chenga. Anaangalia aupige wapi. Anapiga pasi safi kwake Umuliza. Umuliza na mpira. Umuliza anakwenda. Anapiga shoti ndefu kuelekea lango la Tusonge. Munyana anajibu kombora kwa kichwa. Mpira unakuwa mwingi na kutoka nje.

Hee! Hee! Elimu Bora wameanza mchuano huu kwa kasi mno. Wanatafuta bao la mapema. Kamaliza anarusha ngoma ile kwake Muteteri. Muteteri anateleza na kuanguka. Refa anasema twendelee. Mutoni anachukua mpira. Tusonge wanafanya shambulizi la kujibu. Kamiza kwake Umuhire. Umuhire…Umuhire na mpira. Umuhire anakwenda. Umuhire anavuka mstari wa katikati. Anatoa pasi safi.. go..go..ah! Kijibendera kipo juu. Tona amejenga kibanda katika ardhi ya wenyewe pasi ruhusa. Lo! Leo kuna kazi hapa.

## Msamiati

| | | |
|---|---|---|
| kabumbu | – | mchezo wa mpira wa mguu/kandanda |
| mchuano | – | mashindano baina ya timu mbili |
| fainali | – | shindano la mwisho kabisa la kutafuta mshindi |

kuwania kombe – kushindania kombe/tuzo katika mchezo
wapinzani – kikundi cha watu wanaoshindana na wengine
bingwa tetezi – timu ambayo iliibuka mshindi/kuchukua kombe katika awamu iliyopita ya shindano fulani.
nusu fainali – mchezo unaotangulia fainali ambapo washindi hucheza katika fainali
safu ya ulinzi – wachezaji ambao huzuia wapinzani kufunga bao
kiungo cha kati – wacheza ambao hucheza sana katikati ya uwanja
washambulizi – wachezaji ambao hucheza karibu na lango la wapinzani ili wafunge bao
wachezaji wa akiba – wachezaji ambao hukaa nje ya uwanja na ambao huingizwa ndani kuchukua nafasi za wenzao waliopata jeraha au kuchoka
kuinua kijibendera – kuonyesha kuwa mchezaji amekiuka kanuni za mchezo
kurusha sarufi – kuamua timu gani inaanzisha mchezo kwa kurusha sarafu juu.
anapiga pasi – mchezaji mmoja kumpigia mwenzake mpira
anapiga chenga – kumhepa au kumpita mpinzani kwa mpira
anapiga shoti – kupiga mpira kuelekea lango la mpinzani
anajibu kombora – kuzuia mpira kwa kuupiga kuelekea upande wa pili
mpira unakuwa mwingi – mpira kukosa kuthibitiwa na wachezaji
mpira umetoka nje – mpira kuenda nje ya mstari wa nje uwanjani
bao – mpira kuingia ndani ya lango
shambulizi la kujibu – wachezaji kuelekeza mpira kwa kasi kuelekea lango la wapinzani punde tu baada ya mpira kuelekezwa langoni mwao
kujenga kibanda/kuotea – kuvunja kanuni za ushambulizi kwa kushambulia ghafla nyuma ya mchezaji wa mwisho wa timu pinzani

## Zoezi

1. Tunga sentensi sahihi ukitumia msamiati uliotolewa maelezo hapo juu.
2. a) Orodhesha na utoe maana ya maneno yote katika rejesta ya kandanda kifunguni humu lakini ambayo hayakuelezwa hapo juu.
   b) Tunga sentensi ukitumia msamiati uliotaja hapo juu.

## *Kazi ya kikundi*

Wewe ni mtangazaji wa mpira wa miguu. Andika matangazo ya mchezo kati ya timu zozote mbili upendazo. Baada ya kuandika, jiunge na mwanafunzi mwenzako. Kila mmoja amsomee mwenzake matangazo yake.

## Sifa za rejesta ya mpira wa miguu

Tazama matangazo ya mpira katika kifungu ulichosoma. Je, pana sifa gani katika rejesta hiyo?

Zifuatazo ni orodha ya sifa za rejesta ya mpira wa miguu.

i) Hujaa jadhba hasa baada ya mchezo kuanza,
ii) Hujaa mazungumzo ya kuhamisha ndimi ambapo baadhi ya maneno ya Kiingereza na hata kienyeji hutumiwa,
iii) Huwa na lugha ya kuchekesha na kuburudisha wanaoisikiliza,
iv) Hujaa maoni mbalimbali kuhusu nani atashinda, nani mchezaji bora zaidi, na kadhalika,
v) Huwepo kurudiarudia maneno kama vile majina ya wachezaji, dakika zilizopita, mabao yaliyofungwa na kadhalika,
vi) Huwa na lugha ya kuibua hisia na kumfanya mtu kuingiwa na mahangaiko ya moyo,
vii) Sentensi fupi fupi huweza kutumika pamoja na taswira ya kuchora picha kamili ya yanayotendeka.

### Kazi ya wanafunzi wawili wawili

*Jiunge na mwenzako mmoja. Someni kifungu hiki ili mbainishe rejesta ya mpira wa miguu na sifa zao.*

**Matangazo ya kandanda sehemu II**

Mlinda lango wa Elimu Bora anaenda kupiga mpira wa madhambi. Anapiga kombora ndeeeefu na kutoka nje. Munyana anarusha ngozi iliyowambwa na kutengenezwa mpira. Kamiza anapiga chenga. Anatoa pasi kwake Usanase. Usanase anakwenda. Anaingia ndani ya kijisanduku. Hatari katika lango la Tusonge. Hatariiiii! Lo! Kayitesi ananawa mpira. Refa anasemaje. Naam, kipenga kinapulizwa. Refa anawapa Elimu Bora penalti. Shangwe na vifijo kutoka kwa mashabiki wa Elimu Bora. Kayitesi anaonyeshwa kadi ya manjano. Kayitesi amecheza rafu. Achunge asionyeshwe kadi nyingine ya manjano kwani atatolewa uwanjani.

Haya! Tuone jinsi mambo yatakavyokuwa hapa. Refa anahesabu miguu kumi na miwili kutoka lango la Tusonge. Anaweka mpira chini. Ikirezi amesimama nyuma ya mpira ule tayari kupiga mkwaju wa penalti. Mlinda lango wa Tusonge, Kabatesi, amesimama mbele ya wavu. Refa anapuliza kipenga. Ikirezi anapiga hatua mbili tatu nyuma. Anapiga…go…goo... Nje! Heeee! Heee! Ikirezi ameshindwa kutikisa wavu. Alipiga kombora zito. Kabatesi akaruka na kuupiga mpira ule ukapitia juu ya mtambaa panya wa goli hadi nje. Kona! Kona ile inapigwa kutoka kushoto wa goli la Tusonge.

Dakika zilizokatika hapa ni dakika kumi na tano. Bado dakika thelathini kipindi cha kwanza kikamilike. Tutakupa nafasi ya kuwasiliana nasi wakati wa mapumziko

ambao utachukua dakika kumi na tano. Baadaye tutarudi hapa kwa kipindi cha pili ambacho kitachukua dakika nyingine arubaini na tano pamoja na dakika za nyongeza kutoka kwa refa mkuu. Ikiwa timu hizi zitatoka sare baada ya kipindi cha lala salama, dakika thelathini za ziada zitaongezwa. Ikiwa bado mshindi hatapatikana, watapiga penalti ya kuamua mshindi. Mshindi na mshinde sharti wapatikane leo kwa sababu hii ni fainali.

Umuliza anapiga kona safi pale. Uwamwiza anakimbilia mpira ule. Anapiga kichwa.. go..goo…gooooooool! Mpenzi msikilizaji, hayawi hayawi huwa! Hatimaye Elimu Bora wamepata goli la kwanza. Uwamiza amecheka na wavu. Yeye ndiye mfungaji bora kufikia sasa. Mashabiki wote wa Elimu Bora na makochi wao wameacha viti vyao. Mashabiki wa Tusonge wameinamisha vichwa vyao. Wachezaji wa Tusonge wamepandwa na mori. Wamemzingira refa mkuu. Wanadai kuwa Uwamwiza alikuwa ameotea. Nahodha wao, Mutoni, ambaye ni beki wa kupanda na kushuka anammiminia refa maneno makali. Refa anatia mkono katika mfuko wa nyuma ya kaptura na kuchomoa kadi nyekundu. Salaale! Mutoni ameonyeshwa kadi nyekundu kwa kukosa adabu. Anasindikizwa nje ya uwanja. Timu ya Tusonge wamebaki na wachezaji kumi pekee. Je, itakuaje?

### ii) Rejesta ya burudani

Kama ujuavyo, burudani ni shughuli ifanywayo kwa ajili ya kuchangamsha na kufurahisha watu. Nayo mazingira ya namna hii yana msamiati wake ambao ndio lengo la sehemu hii.

***Tazama mchoro huu na ueleze mambo yanayojiri katika mchoro wenyewe.***



***Soma kifungu hiki cha habari na ujibu maswali chini yake***.

MFAWIDHI: Leo ni leo! Asemaye kesho….?

WATU: Ni mwongo!

MFAWIDHI: Hapana! Asemaye kesho hayuko hapa. (*Watu wanacheka*) Leo *show* hii itakuwa ya kukata na shoka. Kama huna shoka sijui utakata na nini.

MTU I: Tutakata na wembe.

MFAWIDHI: Wembe utavunjika. (*Watu wanacheka*) Tuna wasanii wanaotajika ambao wamefika hapa kututumbuiza. Mko tayari *kuvunjika mbavu*?

WATU: Ndiyooooo!

MFAWIDHI: Shauri yenu. Mimi sitagharamia matibabu ya mbavu zitakazovunjika. (*Watu wanacheka*) Mabibi na mabwana, sote tumkaribishe mwimbaji katika jukwaa kwa makofi na vigelegeleeeeee!
*(Watu wanapiga makofi. Mwimbaji anaingia.)*

MFAWIDHI: Kwenu mnanunua sindano kweli?

MWIMBAJI: Hapana.

MFAWIDHI: Ningeshangaa. Wewe ni sindano tayari. (*Watu wanacheka*)

MWIMBAJI: Kwetu tuko wengi sana.

MFAWIDHI: Mko wengi hadi mnapika chapati moja kisha mnapiga chapa. (*Kicheko*). Kabla hatujaanza, ebu tupe historia fupi kuhusu safari yako katika muziki.

MWIMBAJI: Nilianza kwa kucheza kayamba kanisani. Hapo ndipo bendi ya Umoja Jazz wakatambua kipawa changu. Wakanichukua kuwachezea tarumbeta. Baada ya muda mfupi, nikaanza kujisimamia. Nikatunga na kurekodi nyimbo zangu kama na kujichezea gitaa. Hivi karibuni nitaunda bendi yangu.

MFAWIDHI: Usikose kunijumuisha katika kwaya yako. Nitakuimbia *soprano*. (*Watu wanacheka*) Leo umetuandalia nini?

MWIMBAJI: Leo nitawatumbuiza kwa taarabu.

MFAWIDHI: Haya haya! Wakati wa burudani umewadia. Kila mtu atafute nafasi na mwandani wake. Muwe wawili wawili. Kama huna wako, eleka jiwe. Kuna mawe mengi hapa. (*Kicheko*) Hakuna kukanyagana mguu. (*Watu wanacheka*). Kama hujui kucheza miondoko ya taarabu, kuja hapa mbele nikufunze. (*Watu wanacheka*). Haya twende kazi.
*(Mwimbaji anaimba. Watu wanacheza.)*

## Maelezo ya msamiati

kukata na shoka – kufana
kuvunjika mbavu – kucheka
kayamba – ala ya muziki yenye umbo la kisanduku ambayo hutengenezwa kwa matete na kutiwa punje kavu au changarawe na hutikiswatikiswa wakati wa kuimba
bendi – kikundi cha waimbaji wanaoimba pamoja
tarumbeta – ala ya muziki ya kupuliza ambayo hutengenezwa kwa shaba na hutoa sauti mbalimbali
gitaa – ala ya muziki ambayo kwa kawaida huwa na nyuzi sita
kwaya – uimbaji wa pamoja katika kikundi maalamu cha kuimba
taarabu – muziki wenye mahadhi ya mwambao wa Afrika Mashariki unaotumia mchanganyiko wa ala za Kiarabu, Kihindi na Kizungu

## Zoezi

1. Tunga sentensi sahihi ukitumia msamiati uliotolewa maelezo hapo juu.
2. Toa mifano zaidi ya rejesta ya burudani. Andika msamiati wa kimsingi unaotumika katika rejesta hizo.
3. Eleza sifa ya lugha iliyotumika kifunguni.

## Sifa za rejesta ya burudani

Rejesta ya burudani huwa na sifa mbalimbali. Tazama baadhi ya sifa hizo katika orodha ifuatayo:

i) Kuwa na maneno ya raha,
ii) Huibua hali za kutuliza na kupumbaza mshiriki,
iii) Kuwepo na uwezekano wa washirika wake kukesha hadi che huku wakijifurahisha kwa namna wapendavyo,
iv) Kuwepo bendi ya muziki na wanasarakasi,
v) Hali ya kusahau shida na mahangaiko aliyonayo mshiriki angalau kwa wakati mfupi tu.

## *Kazi ya wanafunzi wawili wawili*

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Fanyeni mazoezi haya:

1. Toeni mifano zaidi ya rejesta za burudani.
2. Jadilianeni sifa za lugha inayotumika katika rejesta mlizotaja.
3. Linganisheni na mtofautishe msamiati uliotumika katika rejesta hizo mbalimbali za burudani.

## Umuhimu wa michezo na burudani

### *a) Umuhimu wa michezo*


Michezo ni shughuli za kushindana kati ya timu au watu tofauti tofauti ili kutafuta ushindi. Je,wewe unapenda kucheza mchezo gani?

## *Kazi ya wanafunzi wawili wawili*

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Tazameni michoro iliyopo hapo chini na mtaje yanayotendeka.

1



2



3



4



5



6



***Soma kifungu na ujibu maswali yaliyoulizwa chini yake.***

Michezo ina umuhimu mkubwa kwetu kutokana na sababu mbalimbali. Kwanza, mchezo huimarisha afya yetu. Wachezaji hufanya mazoezi ya viungo. Mazoezi hayo ya viungo husaidia miili yetu kuyeyusha mafuta ya ziada, kunyosha misuli, kuimarisha mapigo ya moyo na kadhalika.

Pili, michezo huleta umoja miongoni mwa jamii. Watu wanapoenda kutazama mchezo kama vile kandanda, hujumuika pamoja kushabikia timu fulani. Pale, wao hujenga urafiki. Mathalan, timu yetu ya taifa inapocheza, Wanyarwanda wote huja pamoja kuishabikia. Tunapofanya hivyo, tunajenga umoja wetu kama Wanyarwanda. Baadhi ya mashabiki pia husafiri pamoja na timu yetu ya taifa wanapocheza nje ya Rwanda. Safari kama hizo huchangia kujenga umoja na urafiki miongoni mwa mashabiki hao.

Tatu, michezo huleta fahari. Mchezaji mashuhuri, timu bora na taifa bingwa katika michezo fulani hujulikana kwingi na kusifiwa. Sifa hizi huinua hadhi ya mtu binafsi, timu na taifa kwa jumla. Nchi inayosifika kwa mchezo au michezo fulani huwa katika hali nzuri ya kuvutia watalii.

Michezo huleta pato la kuridhisha. Pato hili huwa kwa mchezaji binafsi, kwa kilabu na hata kwa taifa. Wachezaji wa vilabu mbalimbali na timu ya taifa hulipwa

mshahara na marupurupu mengi. Baadhi ya wachezaji hawa hasa wanaochezea vilabu vya kimataifa ni matajiri wa kutajika kutokana na michezo.

Vilabu mbalimbali pia hunufaika pakubwa. Wao hukusanya pesa nyingi kutokana na mauzo ya tikiti, matangazo ya biashara katika viwanja vyao, kuuzwa kwa wachezaji wao kwa vilabu vinginevyo na kadhalika.  Taifa zima pia hunufaika kutokana na ushuru mbalimbali unaolipwa na wachezaji pamoja na vilabu husika.


Michezo huburudisha na kutuliza roho. Baada ya shughuli nyingi za siku au wiki, mashabiki hujipumzisha akili kwa kutazama michezo wanayopenda. Pia, kushabikia timu na kusherehekea ushindi huleta uchangamfu.

### Maswali

1. Taja umuhimu wa michezo kulingana na kifungu hiki.
2. Michezo ni njia bora kuu ya kuimarisha afya yetu. Tetea kauli hii.
3. Eleza jinsi michezo huleta ushirikiano kati yetu.
4. Jadilianeni kuhusu jinsi mnavyoweza kutumia michezo kukuza ushirikiano, kuboresha afya na kutatua matatizo yanayokumba jamii yenu.

### *b) Umuhimu wa burudani*

***Tazama michoro iliyopo hapa chini. Je, mambo gani yanafanyika?***

1


2



3


4


***Soma kifungu kifuatacho na ujibu maswali chini yake.***

Kama ilivyo michezo, burudani ina umuhimu mkubwa kwa jamii. Kwanza, burudani hukuza umoja na utangamano miongoni mwa wanajamii. Watu wanapokuja pamoja kucheza densi, kutazama sarakasi, sinema na kadhalika, wao hujenga urafiki na uhusiano mwema miongoni mwao.

Vilevile, burudani hukuza ushirikiano. Watu wanaoshiriki katika kuwaburudisha wanajamii huja pamoja ili kuafikia malengo hayo. Mfano, bendi au kwaya hushirikisha watu mbalimbali. Ushirikiano huu hukuza umoja miongoni mwa wahusika wote.

Burudani pia hukuza afya yetu. Tunaposhiriki katika densi, viungo vya miili yetu hupata mazoezi muhimu ambayo huboresha afya yetu. Vilevile, akili zetu huchangamka kupitia burudani hasa baada ya kazi nyingi za siku au msiba. Uchangamfu huu huleta utulivu na liwazo katika akili zetu. Pia, hutuepushia huzuni ambayo ni hatari kwa afya yetu.

Burudani hudumisha utamaduni. Hapa, chukua mfano wa ngoma zetu maarufu. Unapata kuwa ngoma hizo zilichezwa enzi za kale. Kupitia nyimbo hizo, tunafahamu hali ya maisha katika enzi hizo za kale. Kwa hivyo, hii ni njia moja ya kuhakikisha kuwa utamaduni wetu haupotelei mbali.

Burudani pia ni chanzo cha ajira na pato. Watu wengi wameajiriwa kupitia burudani kama vile bendi, sarakasi, mchezo wa kuigiza na kadhalika.

Burudani pia huweza kumletea mtu sifa nzuri. Kwa mfano, wapo waimbaji, waigizaji, wanasarakasi na kadhalika ambao wanajulikana kote ulimwenguni na kupendwa na wengi.

### Maswali

1. Kwa maneno yako mwenyewe, eleza maana ya burudani.
2. Je, ni jambo lipi unaloliona kuwa ni la muhimu zaidi kuhusu burudani? Kwa nini?
3. Andika sifa ambazo zinafanya michezo na burudani kuwa sawa.
4. Taja umuhimu wa burudani ambao haukutajwa kifunguni humu.

### *Kazi ya wanafunzi wawili wawili*

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Jadilianeni kuhusu umuhimu wa burudani kiafya na kiushirikiano.

## iii) Rejesta ya hotelini

Hoteli ni nyumba ambamo vyakula na vinywaji huuzwa. Vyumba vya kulalia pia hupatikana hotelini. Rejesta ya hoteli hutumika katika mazingira haya.

***Jiunge na mwenzako na msome kifungu kifuatacho*.**



NDOLI: Karibuni katika hoteli yetu! Jina langu ni Ndoli na mimi ndiye mhudumu.
ITUZE: Asante sana kwa makaribisho yenu.
GANZA: Tunashukuru. Mna nini leo?
NDOLI: Tuna vyakula vingi kwenye ankra. Tuna *tilapia, matoke, ugali, kisamvu* na *mizuzu*. Pia tuna vinywaji vingi. Tuna uji, chai na kahawa.
GANZA: Niletee *matoke* sahani moja.
ITUZE: Mimi juisi ya baridi. Nitaitisha vingine baadaye.
(*Ndoli anaondoka na kurudi na vyakula vilivyoagizwa*)
NDOLI: Karibuni. Mjihisi nyumbani.
GANZA: Asante. Nina swali kabla hujaenda. Sisi ni wageni hapa Kigali. Jioni tutahitaji mahali pa kulala. Je, tunaweza kupata vyumba vya kukaa?
NDOLI: Bila shaka vyumba mtapata. Vyumba vyetu vyote ni vya hali ya juu kwa wageni kama nyinyi. Vyumba hivyo vina maji moto, televisheni na huduma za bure za mtandao. Pia, tunawapa wageni wetu kiamsha kinywa, chamcha na chajio.
GANZA: Mna huduma gani zaidi?
NDOLI: Tuna mabwawa ambapo wageni wetu huogelea. Pia, tuna ukumbi wa mazoezi ya viungo. Mtakaa kwa muda gani?
GANZA: Tutakaa kwa siku tatu. Tunahudhuria kongamano kuhusu mbinu mpya za kilimo. Baadaye tutazuru mbuga ya wanyama ya Akagera.
NDOLI: Karibuni tena.
GANZA na ITUZE: Asante sana.

## Maswali

1. Eleza maana ya msamiati mbalimbali wa hoteli jinsi ulivyotumika kifunguni.
2. Tunga sentensi sahihi ukitumia msamiati uliotaja hapo juu.
3. Je, pana umuhimu gani kwa mhudumu kuonyesha adabu na heshima anapozungumza na wateja katika hoteli?

## Kazi ya wanafunzi wawili wawili

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Fanyeni utafiti kuhusu lugha gani inayotumika katika mazingira ya hoteli nchini Rwanda. Wasilisheni matokeo yenu mbele ya darasa.

## Sifa za rejesta ya hotelini

Rejesta ya hotelini huwa na sifa zifuatazo:

i) Kuwepo kwa lugha ya vyakula mbalimbali,
ii) Kupatikana kwa msamiati wa vinywaji vingi,
iii) Wahudumu kuzungumza na wateja kwa unyenyekevu,
iv) Kupatikana maneno ya huduma mbalimbali,
v) Lugha ya mkato hutumika.

## Kazi ya kikundi

Jiunge na wanafunzi wenzako katika kikundi. Fanyeni maigizo ya mazungumzo ya hotelini kati ya mhudumu na wateja. Zingatieni sifa mbalimbali za rejesta ya hoteli.

## iv) Rejesta ya mahakamani

Mahakamani au kortini ni mahali pa kusikilizwa na kuamuliwa mashtaka na kesi mbalimbali. Yeyote anayefanyiwa mabaya ana ruhusa ya kumshtaki mahakamani aliyemfanyia ubaya huo.

Je, umewahi kuhudhuria vikao vya mahakama?

*Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Tazameni mchoro uliopo hapa chini. Jadilianeni kuhusu watu waliopo kwenye mchoro na shughuli zinazoendelea. Linganisheni yaliyomo humo na yale mnayofahamu kuhusu mahakama.*



***Soma kifungu kifuatacho na ujibu maswali chini yake.***

**Mahakamani sehemu I**

KARANI: Shughuli za korti hii zimeanza. Hakimu Ganza ndiye mwamuzi katika kesi hii. Ketini tafadhali. (*watu wanakaa*)

HAKIMU: Ninatangaza rasmi kusikilizwa kwa kesi ya Thierry Ngabo dhidi ya Jane Usanase. Je, pande zote mko tayari?

KIONGOZI WA MASHTAKA: Tayari kwa niaba ya upande wa mashtaka, Mheshimiwa.

WAKILI: Tayari kwa niaba ya mshtakiwa, Mheshimiwa.

HAKIMU: Thierry Ngabo?

MSHTAKIWA: Naam, mheshimiwa.

HAKIMU: Natumai unajua haki zako. Una haki ya kuwakilishwa na wakili mbele ya mahakama hii. Una haki ya kunyamaza kimya au kujibu mashtaka. Pia, una haki ya kukata rufaa ikiwa hutaridhika na uamuzi wa mahakama. Je, ni kweli kuwa unajua haki hizi?

MSHTAKIWA: Naam.

HAKIMU: Unashtakiwa kwa mashtaka mawili. Katika shtaka la kwanza, unashtakiwa kuwa mnamo usiku wa tarehe ishirini na tisa, mwezi wa kumi na moja mwaka wa elfu mbili kumi na sita ulipatikana ukiendesha gari la kibinafsi lenye nambari ya usajili ASA000R katika barabara kuu ya kutoka Ngoma kuelekea Kirehe bila idhini ya mmiliki wa gari hilo. Gari hilo liliripotiwa kupotea mnamo tarehe ishirini na nane, mwezi wa kumi na moja mwaka wa elfu mbili kumi na sita. Katika shtaka la pili, unashtakiwa kwa kukwepa vizuizi vya polisi na kutumia njia mbadala polisi walipojaribu kukusimamisha. Unakubali au unakataa shtaka la kwanza?

MSHTAKIWA: Ninakataa.

HAKIMU: Unakubali au unakataa shtaka la pili?

MSHTAKIWA: Ninakataa.

HAKIMU: Upande wa mashtaka.

KIONGOZI WA MASHTAKA: Asante Mheshimiwa. Nina ushahidi wa kutosha kuthibitisha kuwa mshukiwa ana hatia kwa mashtaka mawili yaliyopo mbele ya mahakama. Mheshimiwa, ushahidi utaonyesha kuwa gari ASA 000 R liliibwa mnano tarehe ishirini na nane, mwezi wa kumi na moja mwaka wa elfu mbili kumi na sita, usiku. Siku moja baadaye, mshukiwa alipatikana akiendesha gari hilo. Mheshimiwa, mshukiwa alishindwa kutoa idhini ya mwenye gari na stakabadhi za kumiliki gari hili. Alama za vidole vya mshukiwa pia vilipatikana katika funguo bandia zilizotumika katika wizi wa gari husika. Mheshimiwa, kwa mshukiwa kujaribu kukwepa vizuizi vya polisi ni ithibati tosha kuwa aliiba gari hili. (*Wakili anaomba nafasi ya kuchangia. Hakimu anampa nafasi.*)

WAKILI: Mheshimiwa, ni haki kwa Kiongozi wa mashtaka kudai kuwa mshukiwa ana hatia bila kuthibitisha? Mheshimiwa, kwa mujibu wa sheria kuhusu haki za mshtakiwa, mteja wangu hana hatia

hadi mahakama hii itakapoamua kesi yake hii. Wakati wa kesi hii, utajua ukweli wa mambo. Ngabo alikuwa akiendesha gari ambalo liliibwa na mtu mwingine. Ngabo alipogundua kuwa gari limeibwa, alikuwa mbioni kurejesha gari hilo. Alikuwa amempigia polisi simu katika kituo cha polisi mjini Kerehe kuwa gari analoendesha limeibwa. Hakuwa na nia ya kukwepa vizuizi vya polisi. Alikuwa na nia ya kukwepa mlolongo mrefu wa magari ili afike mjini Kerehe mapema iwezekanavyo. Mheshimiwa, mteja wangu ni mtu asiyekuwa na rekodi yoyote ya wizi. Ndio maana alipewa dhamana bila kuhitajika mdhamini. Kwa hivyo mteja wangu hana hatia.

## Msamiati

korti – mahali ambapo kesi na mashtaka mbalimbali husikilizwa na kuamuliwa. Pia huitwa mahakama.

hakimu – mtaalamu wa sheria anayeajiriwa kusikiliza mashtaka kortini na kutoa maamuzi

kesi – mashtaka yanayosikilizwa mahakamani

mshtakiwa – mtu anayefikishwa kortini kwa kudaiwa kufanya kosa

mheshimiwa – jina la heshima ambalo watu hutumia kortini kumrejelea hakimu

kukata rufaa – mshtakiwa kukataa hukumu aliyopewa kwa kuomba mahakama ya juu isikilize tena kesi yake au ipunguze adhabu aliyopewa

unashtakiwa kwa mashtaka mawili – makosa mawili yameletwa mbele ya mahakama dhidi yako.

ushahidi – thibitisho kuwa jambo fulani lilifanyika au halikufanyika

## Maswali

1. Bainisha msamiati zaidi wa kimsingi katika rejesta ya mahakama katika kifungu ulichosoma.
2. Eleza maana ya kila msamiati na utungie sentensi sahihi.

## Sifa za sajili ya mahakamani

Baadhi ya sifa zinazoweza kubainisha rejesta ya mahakamani ni:

i) Matumizi ya lugha ya adabu,
ii) Kuwepo tafsiri na fasiri ya yanayosemwa hasa ambapo mshtaki ama mshtakiwa haijui lugha rasmi ya mahakamani,
iii) Mawakili hutumia lugha iliyojaa msamiati wa sheria,
iv) Kunukuliwa kwa vifungu mbalimbali vya katiba au sheria,
v) Kukosekana kupinga uamuzi wa korti papo kwa papo bali kupinga huja baadaye,
vi) Kuwepo msamiati wa Kilatini.

***Soma mazungumzo haya ya mahakamani na ujibu maswali.***

**Mahakamani sehemu II**

HAKIMU: Upande wa mashtaka, mna mashahidi?

KIONGOZI WA MASHTAKA: Naam, Mheshimiwa.

HAKIMU: Walete kizimbani.

(*Askari analeta shahidi wa kwanza. Anasimama kwenye kizimba. Karani wa korti anaelekea alipo shahidi akiwa na Biblia na Kurani.*)

KARANI: Unaitwa nani?

SHAHIDI I: Jane Usanase.

KARANI: Uko mbele ya mahakama. Mahakama inataka kujua ukweli. Usimwogope mshukiwa wala mtu yeyote. Ujikaze ili korti ijue ukweli wa mambo. Utakula kiapo kwa Biblia au Kurani?

SHAHIDI I: Biblia.

(*Jane anainua Biblia kwa mkono kwa kulia*)

KARANI: Uyarudie maneno haya kwa sauti. Mimi Jane Usanase.

SHAHIDI I: Mimi Jane Usanase.

KARANI: Ninaapa kwamba yale ambayo nitasema mbele ya korti hii ni ukweli.

SHAHIDI I: Ninaapa kwamba yale ambayo nitasema mbele ya korti hii ni ukweli.

KARANI: Ewe Mungu nisaidie.

SHAHIDI I: Ewe Mungu nisaidie.

(*Karani anakaa. Kiongozi wa Mashtaka anaamka na kuelekea alipo shahidi.*)

KIONGOZI WA MASHTAKA: Unafanya kazi wapi?

SHAHIDI I: Katika Halmashauri ya Wilaya ya Kerehe.

KIONGOZI WA MASHTAKA: Unatumia mbinu gani za usafiri ukienda kazini?

SHAHIDI I: Gari langu la kibinafsi.

KIONGOZI WA MASHTAKA: Gari hilo lilikuwa wapi mnamo usiku wa tarehe 29/11/2016?

SHAHIDI: Nilikuwa nimeliegesha mbele ya hoteli ya Starehe mjini Kirehe.

KIONGOZI WA MASHTAKA: Nambari ya usajili wa gari hilo ni A...

WAKILI: (*Baada ya kumwomba Hakimu nafasi ya kuongea*) Mheshimiwa, ni haki kwa kiongozi wa mashtaka kumwelekeza shahidi katika kutoa ushahidi wake? Gari likiwa lake, mbona asiseme nambari yake ya usajili bila kuambiwa?

HAKIMU: Kiongozi wa mashtaka, shahidi anajua nambari ya usajili wa gari lake. Mwache aitaje.

### *Kazi ya kikundi*

Jiunge na wanafunzi wenzako na mfanye mazoezi haya:


i) Jadilianeni kuhusu sifa za rejesta ya mahakamani. Rejeleeni vifungu mlivyopewa na ikiwezekana msikilize rekodi za matukio mahakamani au kuhudhuria vikao vya mahakama.

ii) Kamilisheni kesi iliyopo mahakamani kuanzia ilipofikia katika kifungu cha pili kwa kuigiza.

### v) Rejesta ya bungeni

Bunge ni baraza la taifa linalotunga sheria na lenye wajumbe waliochaguliwa na wananchi kwa kupigiwa kura ama kwa kuteuliwa na rais.

***Soma kifungu kifuatacho na ujibu maswali chini yake.***



| | |
|---|---|
| KARERA: | Jina langu ni Karera. |
| RUSARO: | Na mimi ninaitwa Rusaro. |
| RURANGIRWA: | Nami ninaitwa Rurangirwa. |
| KARERA: | Tupo hapa mbele yenu, wanadarasa wenzetu, kukuelezeni mengi kuhusu bunge letu ama baraza letu la taifa. Mambo haya tumeyapata kupitia kwa utafiti wa kina ambao tumekuwa tukiufanya. |
| RUSARO: | Wabunge wetu huwawakilisha watu waliowachagua ama vikundi fulani fulani vya raia wa jamhuri yetu. |
| RURANGIRWA: | Namo bungeni, yamo mambo mengi unayostahili kuyajua. Mathalan, mwenye mamlaka ya kuongoza, kuamuru au kuzuia shughuli bungeni ni spika ambaye husaidiwa na naibu wa spika. |
| RUSARO: | Spika ana mamlaka ya kuamua ni mbunge gani atazungumza, atazungumzaje na kwa muda gani na kadhalika. Hapana lolote linaloweza kuendelea bungeni bila yeye kuliruhusu. |
| KARERA: | Hali kadhalika, yamo mambo mengi mengineyo yanayopatikana bungeni. Mambo hayo ni kama vile rais, makamu wa rais, sheria, kutunga sheria, hoja, upinzani, kura, uchaguzi, wakala, eneo la |

| | |
|---|---|
| | ubunge, piga kura, mjumbe mteule, mjumbe wakilishi na kadhalika. |
| RUSARO: | Tukianza na rais tunapata kuwa hakuna bunge bila kuwepo rais. Yeye huhitaji kutawala serikali na nchi nzima kwa mujibu wa sheria. |
| RURANGIRWA: | Nazo sheria hizo ni lazima zitungwe na bunge. Kwa hivyo, kila nchi huhitajika kutawaliwa na rais kwa sheria zilizotungwa na bunge. Naye makamu wa rais ni yule anayemsaidia rais kutawala nchi. Lakini, je, sheria nazo ni nini? |
| RUSARO: | Sheria ni kanuni za kutawalia nchi na ambazo, kama ilivyotajwa awali, hutungwa na bunge. Wabunge huwasilisha hoja bungeni na zikajadiliwa. Baadhi yazo hupitishwa kuwa sheria baada ya kuidhinishwa na rais. Lakini zile hoja zinazopingwa na upinzani na kukataliwa haziwi sheria. Nazo zile anazozikataa rais hurudishwa bungeni ama kurekebishwa ama kutupiliwa mbali. |
| KARERA: | Nao takriban wabunge wote hupigiwa kura ili kuingia bungeni. Wafikapo huko huwa ni mawakala wa wale waliowachagua kutoka maeneo yao ya bunge na huhitajika kufanya juu chini ili kuwainulia hali yao ya kimaisha. |
| RURANGIRWA: | Hata hivyo, huwepo wajumbe wateule ambao huteuliwa na rais ili kuwakilisha sehemu fulani fulani. Kwa mfano, panaweza kuwepo mbuge mteule anayewawakilisha masilahi ya wanawake ama vijana. |
| KARERA: | Isitoshe, ipo kura ya kutokuwa na imani na mtu ama tume fulani. Inaweza kutokea kwamba kiongozi fulani anatuhumiwa kukosea. Basi, bunge linaweza kupitisha kura ya kutokuwa na imani naye na akafutwa kazi. Katika hali kama hii, mara nyingine huteuliwa tume ya kuchunguza ukweli wa tuhuma kabla ya uamuzi kama huu kutolewa. |

**Zoezi**

Bainisha msamiati maalumu wa bungeni kutoka katika kifungu huku ukiutungia sentensi sahihi.

## Sifa za rejesta ya bungeni

Rejesta ya bungeni kama rejesta yoyote ile huwa na sifa zake. Ifuatayo ni orodha ya baadhi ya sifa hizo:

i) Kumrejelea spika kila wakati kwa heshima,
ii) Matumizi ya maneno yenye adabu,
iii) Kutokuwepo ruhusa ya kumshtaki mzungumzaji kwa maneno aliyotamka,
iv) Kuwepo kwa lugha ya kupiga kura kwa hoja fulani,
v) Kuwepo kwa mtindo fulani wa kuandika ama kuwasilisha hoja,
vi) Kuwepo kwa utaratibu wa kuzungumza,

vii) Kurejelewa kwa vifungu vya sheria mbalimbali za bunge na katiba kila wakati,
viii)Kutumika kwa lugha ya utafiti.

### Kazi ya wanafunzi wawili wawili

Jadilianeni kuhusu sifa za sajili ya bunge kwa kurejelea mjadala bungeni na makala mbalimbali ambayo yamerekodi mijadala bungeni.

### Kazi ya darasa

Kama darasa zima, igizeni mjadala bungeni. Pawepo spika, karani na maafisa mbalimbali wa bunge. Wanafunzi waliosalia wawe wabunge na wachangie katika mjadala.

## vi) Rejesta ya sokoni

Sokoni ni mahali penye mkusanyiko wa watu wanaouza na kununua bidhaa mbalimbali. Wauzaji wengi huuza bidhaa zao kwa rejareja, kwenye kibanda au katika maduka. Baadhi ya masoko hutenga siku moja au mbili kama siku maalumu za soko kila wiki. Siku kama hiyo ya soko huitwa chete. Masoko mengine huendesha shughuli zake kila siku. Bidhaa nyingi huuzwa sokoni.

***Soma kifungu hiki ili kujifunza mengi kuhusu rejesta ya sokoni.***

*(Umuhire anaingia sokoni. Sauti za wauzaji mbalimbali zinasikika.)*

SAUTI: Mia bei! Mia bei...Karibu mteja..Ni za leo...ni za leo...bei rahisi...bei ya jioni...bei ya hasara...karibu, chagua...chagua...beba nguo na hamsini...

MWUZAJI: (*Umuhire anaingia katika kioski kimoja*.) Karibu mteja wangu! Bei rahisi kwa bidhaa nzuri! Karibu katika kibanda changu! Karibu uchague bidhaa utakazo. Leo nina mboga safi safi, matunda matamu matamu na nyanya kubwa kubwa.

UMUHIRE: Ahaa! Leo sina pesa ya matunda. Nitanunua siku nyingine. Una kitunguu?



MWUZAJI: Siwezi kukosa vitunguu, bi mdogo. Ndivyo hivi hapa.

UMUHIRE: Je, kifungu kimoja ni pesa ngapi?

MWUZAJI: Hicho ni bei rahisi sana. Kila kifungu ni faranga kumi tu. Nikufungie ngapi?

UMUHIRE: Aa! Hiyo ni bei ghali mno. Tafadhali, niuzie vifungu vitano kwa faranga arubaini.

MWUZAJI: Hapo umenizamisha, bi mdogo. Sitapata faida yoyote. Bei ni hiyo tu.
UMUHIRE: Wewe nawe! Faida utapata kwa bidhaa nyingine. Hutaki nirudi tena?
MWUZAJI: Ninataka urudi kila mara. Basi ongeza faranga tano nikufungie.
UMUHIRE: Jamani! Unataka tule mboga bila chumvi? Hiyo faranga tano ni ya chumvi.
MWUZAJI: (*Anacheka*) Nami hutaki nile chamcha? Hiyo faranga tano ni ya kujinunulia chakula. Unataka babu yako afe kwa njaa?
UMUHIRE: Haya! Chukua faranga zako arubaini na tano.
MWUZAJI: Asante bi mdogo. Chukua bidhaa zako.
UMUHIRE: Asante.
MWUZAJI: Karibu tena. Mbona hununui mboga pia?
UMUHIRE: Mboga ninazo katika shamba langu nyumbani.
MWUZAJI: Pongezi sana. Una aina gani ya mboga?
UMUHIRE: Nina sukumawiki.
MWUZAJI: Unaweza kuniuzia gunia moja la sukumawiki?
UMUHIRE: Sawa. Nitakuletea siku ya Jumamosi. Nyama inauzwa wapi?
MWUZAJI: Nyama inauzwa kwenye buchari. Buchari ipo nyuma ya kibanda hiki.
UMUHIRE: Nimeshukuru.

**Zoezi**

1. Eleza maana ya maneno yaliyokolezewa wino katika kifungu.
2. Tunga sentensi ukitumia msamiati ulioorodhesha hapo juu.

### Sifa za rejesta ya sokoni

Sifa zinazobainisha rejesta ya sokoni ni:

i) Lugha ya kurudiarudia maneno hutumika huku bidhaa zikinadiwa,
ii) Lugha ya kuwavutia wateja huweza kutumiwa,
iii) Hutumika lugha isiyo rasmi na sarufi hukosa kufuatwa,
iv) Kiimbo cha wauza bidhaa hutumika kama vile kuzungumza kwa upole kwa wazee na kutumia lugha ya kusifu kwa wateja wanaonekana tajiri,
v) Lugha ya kununua na kuuza hutumiwa kama vile: panda bei, shuka bei,

***Kazi ya wanafunzi wawili wawili***

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Igizeni mazungumzo kati ya mwuzaji na mnunuzi. Zingatieni sifa za rejesta ya sokoni.

### vii) Rejesta ya kanisani

Kanisa ni jengo ama mahali panapotumiwa na Wakristo kufanyia ibada. Ama pia neno hili lina maana ya Jumuiya ya Wakristo.

***Kazi ya kikundi***

Jiunge na wenzako watano na mjadili mambo mnayoyaona katika mchoro ufuatao.



***Sasa someni kifungu kifuatacho na halafu mjibu maswali yaliyoulizwa.***

Mambo yote yanayohusu kanisa na imani ya mtu ni mambo magumu sana maishani mwetu. Amri Kumi za Mungu pamoja na amri nyingine zozote zinazohusu dini ya kweli, huhitaji mwanadamu kukaa katika mema na haki mbele ya Mwenyezi Mungu. Hayo ndiyo masharti ya Neno ama Biblia. Mitume na malaika wa Mungu waliwajia mara kwa mara waumini walioamini katika dini kuwakumbusha haya. Nayo misahafu dini mbalimbali za haki huyasisitiza yaya haya. Sasa ugumu huja katika kuyatekeleza.

Hata hivyo, kupo kutubu. Huku kutubu ni njia ya pekee ya kuondoa ugumu huo. Kila atendaye dhambi mbele ya Mola ana ruhusa ya kutubu. Makasisi, mapadri, wachungaji, maaskofu, maaskofu wakuu pamoja na viongozi wengine makanisani wana jukumu la kuhakikisha kuwa waumini wao hutubu na kumrudia Manani. Nako kutubu huko kunaweza kufanywa wakati wa ibada wanapokuwa wanamwabudu Muumba ama wakati mwingine wowote. Kunaweza pia kufanywa kupitia kwa sala. Katika haya yote, ni sharti ikumbukwe kwamba mwovu shetani hapumziki mpaka aone kuwa binadamu wengi ama wote wamo katika dhambi. Binadamu huyo akitubu, malaika mbinguni wanafurahi sana. Lakini shetani anatafuta njia nzuri nzuri za kumfanya mwanadamu yuyo huyo arudi dhambini tena. Mbinu zake nyingi huwa za msingi wa raha. Anajua kuwa binadamu ni mpenda raha. Hata hivyo, lipo Neno linalovunjavunja juhudi kama hizo.

Kanisa huhubiri habari za jahanamu, kuangamia motoni, kuingia mbinguni, njia pana, njia nyembambana, msalaba wa Yesu, Mwokozi Yesu, Utatu wa Uungu, na hata siku ya kiama. Jahanamu ama ahera ni pahali ambapo inaaminika roho za wale waliokufa huenda kungoja siku ya kiama ambayo itakuwa siku ya kutolewa

hukumu na Mungu Muumba. Swali kuu siku hiyo litakuwa, *Umefanya nini na Neno langu*? Wale ambao hawatajibu vilivyo watatupwa motoni na wale ambao watajibu vilivyo wataingia mbinguni.

Jambo jingine kanisani ni msalaba. Yesu Kristo alisulubishwa kwenye msalaba ili amfie mwanadamu apate kuokolewa na damu yake. Kwa hiyo, msalaba ni ukumbusho kwamba tayari mwanadamu ameokolewa na analohitaji kufanya ni kuungama dhambi zake.

Jambo jingine ni kwamba maeneo mbalimbali ya kuabudia huwa na maneno wanayochukulia kuwa yanawawezesha kuwasiliana vilivyo na Mungu. Maeneo hayo ni kama vile kanisani, msikitini, hekaluni na kwingineko kukiwa pamoja na barabarani.

**Zoezi**

Jiunge na mwenzako. Jadilianeni maana ya maneno yaliyokolezewa wino na msamiati zaidi unaotumiwa kanisani na msikitini.


### Sifa za rejesta ya kanisani

Baadhi ya sifa za rejesta ya kanisani ni kama vile:

i) Huwepo na pahali pa kumwabudia Mungu,
ii) Katika baadhi ya dini, hutumika msamiati wa wale walioileta dini k.v. Kiingereza,
iii) Huwezekana kuwepo mkalimani wa kutafsiri na kufasiri,
iv) Baadhi ya wahubiri huanza kuzungumza kwa kasi wanapopandwa na jadhba,
v) Sadaka hupewa majina mbalimbali na huwa ni sharti zitolewe,
vi) Waumini hawana ruhusa ya kuulizia wasilolielewa wakati mhubiri anapokuwa anahubiri,
vii) Ni sharti msamiati wa kidini utumiwe badala ya ule wa lugha ya kawaida,
viii) Huwepo kwaya ama mwimbaji,
ix) Vifungu mbalimbali vya Biblia hunukuliwa.

### viii) Rejesta ya sarufi ya Kiswahili

Sarufi ni kanuni za lugha zitumiwazo ili kupata ufasaha katika lugha. Kila lugha huwa na sarufi yake. Hivyo basi, ipo sarufi ya Kiswahili ambayo ina rejesta yake.




***Someni kifungu kifuatacho ili kujifunza maneno zaidi ya sajili hii ya lugha.***

Fikiria ingekuwaje kama hatungekuwa na lugha? Hata ishara mbalimbali zina msingi wa lugha. Ama kwa kweli, mambo mengi yangalikwama kama hapangekuwa na lugha.

Rejesta ya lugha ni muhimu kama lugha ilivyo kwa kuwa mambo hayo mawili ni jambo moja tu. Katika rejesta ya sarufi mna maneno kama vile sajili, sarufi, Kiswahili, sentensi, lafudhi, alfabeti, vitenzi, mnyambuliko, maandishi, majina, namna za majina, vivumishi, vielezi, viwakilishi, viunganishi, vihusishi, vihisishi, aya, kuakifisha na kadhalika.

Ukija kuangalia maana ya maneno haya, unapata kuwa sajili ni rejesta kama ilivyoelezwa hapo awali lakini sarufi ni sheria ziongozazo lugha fulani. Nacho Kiswahili ni lugha izungumzwayo na Waswahili lakini sentensi ni tungo ijitoshelezayo na ambayo huhusisha mtendaji na kitendo. Nayo lafudhi au lafidhi ni namna maneno yanavyotamkwa ilhali alfabeti ni herufi za lugha ambazo zimepangwa kwa utaratibu maalumu.

Navyo vitenzi ni maneno yakuambiayo cha kufanya na mnyambuliko ni namna vitenzi hivyo hujigeuzageuza ili kuleta maana ihitajikanayo. Maandishi nayo ni kuwakilisha sauti kwenye karatasi kwa kutumia kalamu ilhali majina ni neno la kumtaja mtu, kitu au jambo.

Namna za majina ni vikundi vya majina yanayochukua sifa fulani inayoyasawazisha. Vivumishi ni maneno yaongezeayo majina maana na pia kujiongezea maana. Vielezi navyo ni maneno yaongezeayo vitenzi maana ilhali viwakilishi ni maneno ama viungo vya maneno vinavyosimamia majina.

Isitoshe, kuna viunganishi, vihusishi, vihisishi, aya, na kuakifisha. Viunganishi ni maneno yanayounganisha maneno mengine lakini vihusishi huhusisha watu ama vitu na mahali. Navyo vihisishi ni maneno yanayoonyesha mahangaiko ya moyo ilhali aya ni fungu la sentensi lililo na maana kamilifu, yaani paragrafu. Nako kuakifisha ni kuwakilisha sauti kimaandishi. Ufahamu ni pale ambapo mtu husoma kifungu na halafu akapima ama akapimwa ufahamu wake kuhusu hayo aliyoyasoma. Imla nayo ni pale ambapo unasomewa maneno ama kifungu huku ukiandika.

**Zoezi**

Jiunge na wenzako watatu na mjadili maana na matumizi ya maneno haya yafuatayo:

1. mtungo au insha
2. msamiati
3. rejesta
4. vitendawili
5. methali
6. misemo
7. nahau
8. mafumbo
9. barua
10. masimulizi
11. dhahania
12. istilahi
13. kiimbo

## Sifa za rejesta ya sarufi ya Kiswahili

Nazo sifa za rejesta ya sarufi ya Kiswahili zinaweza kuwa hivi:

i) Imejaa maneno ya kitaalamu,
ii) Hufundisha jinsi ya kutunga tungo sahihi,
iii) Huwa na semi za kutia hekima,
iv) Huwa ndio msingi wa maongezi yote katika lugha husika,
viii)Huwezesha kuhifadhi mila za kabila husika,
ix) Huwa na tamathali za usemi za kuungia usemi

## Zoezi la ziada

***Kazi ya wanafunzi wawili wawili***

Jiunge na mwanafunzi mwenzako na mjibu maswali yaliyopo hapa chini.

***Jazeni jedwali hili. Sehemu ya kwanza imejazwa kama mfano.***

| | **Kifungu** | **Rejesta na watu wanaozungumza** | **Sifa za rejesta na mfano wa msamiati wake** |
|---|---|---|---|
| a) | Mtu I: Wapi menu?<br>Mtu II: Hii hapa.<br>Mtu I: Nipe chai tano, na matoke nne.<br>Mtu II: (*Kwa MTU III*) Wewe?<br>Mtu III: Mimi *isombe*. | Hotelini<br>Mtu I na III: Wateja<br>Mtu II: Mhudumu | 1. Matumizi ya lugha isiyokuwa rasmi. Mfano: chai moja, mimi *isombe*<br>2. Matumizi ya msamiati maalumu wa chakula. Mfano: matoke<br>3. Kuchanganya lugha: Mfano: wapi menu? |
| b) | Mtu I: Ulianza kuhisi maumivu ya tumbo lini?<br>Mtu II: Siku mbili zilizopita.<br>Mtu I: Ulikula nini?<br>Mtu II: Siku hiyo nilikunywa tu maji.<br>Mtu I: Maji hayo yalichemshwa?<br>Mtu II: Hapana.<br>Mtu I: Maji hayo yalitiwa dawa?<br>Mtu II: Hapana.<br>Mtu I: Umemeza dawa gani?<br>Mtu II: Asprin.<br>Mtu I: Kuna mkurupuko wa cholera. Chukua karatasi hii. Enda kwenye maabara ufanyiwe uchunguzi kisha urudi nikuandikie dawa. | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| c) | Mwandishi: Vijana wawili wavumbua dawa mpya ya kuwaulia wadudu wanaoharibu sukumawiki.<br>Jane Usanase, 15, na Paul Ngabo, 14, washangaza wakazi wa wilaya ya Karongi kwa kuvumbua dawa mpya ya kuulia wadudu wanaoharibu sukumawiki. Akionyesha furaha yake, mkuu wa wilaya hiyo Bwana Ndoli aliwapongeza vijana hao kwa kutumia maarifa waliyopata darasani kusaidia jamii zao.<br>“Hii ni changamoto kwa vijana waliopo shuleni. Usisome tu kwa ajili ya kupita mtihani. Tumia maarifa hayo kuleta mabadiliko katika jamii,” alisema Bwana Ndoli.<br>Vijana hao walipokea tuzo nyingi kutoka kwa wakulima. Walionyesha furaha zao na kuahidi kufanya tafiti zaidi.<br>“Sisi tunapenda sana masomo ya Kilimo na Sayansi. Tuliamua kutumia maarifa tuliyopata katika somo la Kemia kutafitia dawa hizi,” alisema Usanase.<br>Vijana hao wanatarajiwa kukutana na rais katika ikulu siku ya Jumamosi. | | |
| d) | Mtu I: Kiranja yu wapi?<br>Mtu II: Hajakuja leo. Aliomba ruhusa! | | |


| | | | |
|---|---|---|---|
| | Mtu I: Akija kesho, mwambie anione ofisini. Mmoja wenu afute ubao. Mwingine aniletee chaki kutoka ofisini.<br>Mtu I: Tafadhali, naomba kuenda msalani.<br>Mtu II: Haya! Harakisha, ninaanza kipindi sasa hivi.<br>Mtu I: Asante. | | |
| e) | Mzungumzaji: Sote tunafaa kumshukuru Mola kwa kutupa uhai ili kufika hapa kumwabudu. Imeandikwa katika Kitabu Kitakatifu kuwa sisi sote ni wageni hapa duniani na tunaishi ili tumwabudu Mwenyezi Mungu na kufanya mapenzi yake. Wale ambao watakiuka mapenzi yake watachomwa na moto wa jehanamu. | | |






## B Matumizi ya majina ya ngeli ya KI-VI katika umoja na wingi

Ngeli ya KI-VI hujumuisha majina mbalimbali. Majina yote katika ngeli hii huchukua upatanisho wa sarufi, ki- katika umoja na vi- katika wingi. Hii ndiyo sababu ya ngeli hii kuitwa ngeli ya KI-VI. Maumbo ya majina katika ngeli ya KI-VI hubadilika kutoka umoja hadi wingi.

Je, unakumbuka majina yanayopatikana katika ngeli hii? Yataje matano katika umoja pamoja na wingi wayo.

***Tazama jedwali hili. Je, ni mabadiliko gani yanayotokea katika majina yanapotoka umoja hadi wingi?***

| | umoja | wingi |
|---|---|---|
| 1. | <br>kiatu | <br>viatu |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | <br>kisu | <br>visu |
| 3. | <br>chungu | <br>vyungu |
| 4. | <br>choo | <br>vyoo |
| 5. | <br>kigoma | <br>vigoma |
| 6. | <br>kitoto | <br>vitoto |

Yapo makundi mbalimbali ya majina yanayopatikana katika ngeli ya KI-VI.

***i) Majina yanayoanza kwa ki- katika umoja na kuchukua vi- katika wingi***

Kundi hili la majina ndilo huwa na majina mengi ya ngeli hii ya KI-VI.

*Mifano*

| Umoja | Wingi | Umoja | Wingi |
|---|---|---|---|
| a) kiboko | viboko | b) kikapu | vikapu |
| c) kinanda | vinanda | d) kijiko | vijiko |
| e) kikombe | vikombe | f) kikoi | vikoi |

**Kumbuka**

Majina ya viumbe wenye uhai ambayo huanza kwa kiambishi ki- katika umoja na vi- katika wingi hayawekwi hapa bali huchukua viambishi ngeli vya ngeli ya A-WA.

**Zoezi**

Andika majina kumi zaidi ya ngeli ya Ki-Vi pamoja na wingi wayo.

***ii) Majina yanayoanza kwa ch- katika umoja na kuchukua vy- katika wingi***

| Umoja | Wingi | Umoja | Wingi |
|---|---|---|---|
| a) chungu | vyungu | b) choo | vyoo |
| c) chombo | vyombo | d) chuma | vyuma |

## Kumbuka

Majina ya viumbe wenye uhai ambayo huanza kwa kiambishi ch- katika umoja na vy- katika wingi hayawekwi hapa bali huchukua viambishi ngeli vya ngeli ya A-WA.

**Zoezi**

Andika majina kumi zaidi yanayopatikana chini ya orodha hii ya majina katika ngeli ya KI-VI.

***iii) Majina kutokana na vitenzi***

Yapo baadhi ya majina ambayo huundwa kutokana na vitenzi. Majina hayo pia hupatikana katika ngeli ya KI-VI.

***Mifano***

| | Kitenzi | Jina (umoja) | Majina (wingi) |
|---|---|---|---|
| a) | lia | kilio | vilio |
| b) | cheka | kicheko | vicheko |
| c) | kaa | kikao | vikao |
| d) | tenda | kitendo | vitendo |
| e) | pima | kipimo | vipimo |

**Zoezi**

Andika majina kumi zaidi yaliyomo katika kundi hili.

***iv) Majina yanayoanza kwa ki- lakini hayachukui wingi***

Yapo majina katika Kiswahili ambayo huanza kwa kiambishi ki- lakini hayana wingi. Majina haya huwa ya viumbe wasiokuwa na uhai.

***Mfano***

a) Kiswahili b) kiangazi c) Kiingereza d) kilimo e) kimya

**Zoezi**

Andika majina matano zaidi yanayopatikana katika kikundi hiki.

### v) *Majina ya vitu katika hali ya udogo*

Katika Kiswahili, majina yanaweza kuwa katika hali ya wastani, udogo au ukubwa.

*Mifano*

| Kawaida | udogo | ukubwa |
|---|---|---|
| mtu | kijitu | jitu |
| mtoto | kitoto | mtoto |
| nyumba | kijumba | jumba |

Majina yote yanapoandikwa katika hali ya udogo, huwekwa katika ngeli ya KI-VI iwe majina ya viumbe wenye uhai au vitu visivyokuwa na uhai.

Katika mfano uliotolewa hapo juu, mtu na mtoto ni viumbe wenye uhai. Majina haya hupatikana katika ngeli ya A-WA. Unaposema kijitu au kitoto, unarejelea mtu mdogo zaidi ya kawaida. Kwa hivyo, majina kitoto na kijitu yanawekwa katika ngeli ya KI-VI. Katika wingi huwa tunasema vitoto au vijitu. Vilevile, nyumba ipo katika ngeli ya I-ZI. Hata hivyo, kijumba (nyumba ndogo kupita kiasi) hupatikana katika ngeli ya KI-VI. Tazama mifano zaidi katika jedwali hapa chini.

*Mifano*

| Umoja | Wingi | Umoja | Wingi |
|---|---|---|---|
| a) kijibwa | vijibwa | b) kidege | videge |
| c) kigoma | vigoma | d) kijikaratasi | vijikaratasi |

**Zoezi**

Andika majina matano zaidi yanayopatikana katika orodha hii ya majina katika ngeli ya KI-VI.

## Matumizi ya majina ya ngeli ya KI-VI

Kama ilivyoelezwa hapo mwanzoni, vitenzi vinavyoambatana na majina katika ngeli hii ya KI-VI huchukua kiambishi ki- katika umoja na vi- katika wingi. Tazama mifano iliyotolewa katika jedwali lifuatalo:

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| a) | Kiatu *ki*meraruka. | Viatu *vi*meraruka. |
| b) | Kijiko *ki*nasafishwa. | Vijiko *vi*nasafishwa. |
| c) | Kiti *ki*taanguka. | Viti *vi*taanguka. |
| d) | Choo *ki*mechafuka. | Vyoo *vi*mechafuka. |
| e) | Cheti *ki*taandikwa. | Vyeti *vi*taandikwa. |
| f) | Chuma *ki*limwangukia. | Vyuma *vi*liwaangukia. |
| g) | Kisahani *ki*mevunjika. | Visahani *vi*mevunjika. |

| | | |
|---|---|---|
| h) | Kitoto *ki*nacheza. | Vitoto *vi*nacheza. |
| i) | Kicheko *ki*nasikika. | Vicheko *vi*nasikika. |
| j) | Kiangazi *ki*meanza. | ----- |
| k) | ------ | Vigelegele *vi*napigwa. |

## Zoezi

1. Eleza maana ya ngeli ya KI-VI.
2. Eleza mabadiliko yanayotokea katika wingi ukirejelea majina haya ya ngeli ya KI-VI.
   i) chombo ii) kioo iii) kiti iii) cheo
3. Kamilisha sentensi zifuatazo:
   i) ___akula ___livyonunuliwa ___meliwa.
   ii) ___dege ___mekamatwa.
   iii) ___beti ___mejaa faranga.
   iv) ___sima vya maji ___nachimbwa hivi sasa.
   v) Niliwaambia wanileteee ___uma ___livyokunjwa.
   vi) Nitasoma kwa bidii ili niingie katika __uo _kuu.
4. Bainisha sentensi sahihi kutoka kwa zile zisizokuwa sahihi na uzisahihishe. Nambari za kwanza mbili zimetolewa kama mfano.
   i) Kiti hiki kinapendeza. SAHIHI
   ii) Choo vimebomolewa. SI SAHIHI.
   Vyoo vimebomolewa. SAHIHI
   iii) Viswahili kinazungumzwa Afrika Mashariki.
   iv) Kioo kinanipendeza.
   v) Kitoto anaruka.
   vi) Kijiti limevunjika.
   vii) Vyuo vikuu vinatoa elimu ya juu.
   viii) Vyuma kinachomwa.
   ix) Kigelegele kinasikika.

## *Kazi ya wanafunzi wawili wawili*

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Tungeni sentensi sahihi katika umoja na wingi mkitumia majina ya ngeli hii ya KI-VI.

## Matumizi ya majina ya ngeli ya KI-VI pamoja na vivumishi

Je, unakumbuka vivumishi ulivyosoma katika sura ya kwanza? Rejelea vivumishi hivyo.

### *a) Majina ya ngeli ya KI-VI pamoja na vivumishi vya sifa*

Vivumishi vya sifa ni maneno yatajayo tabia au sifa za mtu, kitu au jambo.

*Mifano katika sentensi:*

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| i) | Kiti kirefu hakifai. | Viti virefu havifai. |
| ii) | Kijitu kivumilivu hufanikiwa maishani. | Vijitu vivumilivu hufanikiwa maishani. |
| iii) | Kishamba kizuri kinatoa mavuno mengi. | Vishamba vizuri vinatoa mavuno mengi. |
| iv) | Chombo cheupe kinapita. | Vyombo vyeupe vinapita. |

**Zoezi**

Tunga sentensi zozote kumi ukitumia majina ya ngeli ya KI-VI na vivumishi mbalimbali vya sifa.

### *b) Majina ya ngeli ya KI-VI pamoja na vivumishi vya pekee*

Vivumishi vya pekee hutoa habari kuhusu nomino au kiwakilishi chake kwa njia ya kipekee. Huwa vitano.

i) -enye ii) -enyewe iii) -ote iv) -o-ote v) -ingine

Majina katika ngeli ya KI-VI huchukua kiambishi ch- katika umoja na vy- katika wingi yanapotumika pamoja na vivumishi vya pekee vyote isipokuwa -ingine au -ingineo.

***Mifano***

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| i) | Kiti chenye mguu dhaifu kimeanguka. | Viti vyenye miguu dhaifu vimeanguka. |
| ii) | Kifarasi chenyewe kinapenda nyasi. | Vifarasi vyenyewe vinapenda nyasi. |
| iii) | Chuma chochote kitafaa. | Vyuma vyovyote vitafaa. |
| iv) | Choo chote kimeoshwa. | Vyoo vyote vimeoshwa. |

Hata hivyo, kivumishi cha pekee -ingine na -ingineo huchukua viambishi ki- katika umoja na vi- katika wingi kinapotumika na majina ya ngeli ya KI-VI.

***Mifano***

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| i) | Kitoweo kingine kiletwe. | Vitoweo vingine viletwe. |
| ii) | Fagia chumba kingine. | Fagieni vyumba vingine. |
| iii) | Kipimo kingine kinafaa. | Vipimo vingine vinafaa. |

| | | |
|---|---|---|
| iv) | Kioo kinginecho kimepasuka. | Vioo vinginevyo vimepasuka. |
| v) | Nyanya anunue chungu kinginecho. | Kina nyanya wanunue vyungu vinginevyo. |

**Zoezi**

Tunga sentensi zozote kumi ukitumia majina ya ngeli ya Ki-Vi pamoja na vivumishi mbalimbali vya pekee.

### c) *Majina ya ngeli ya KI-VI pamoja na vivumishi vionyeshi*

Vivumishi vionyeshi au viashiria ni maneno ya kuonyesha alipo mtu au kitu, yaani ujirani. Kuonyesha huko kunaweza kuwa kwa ujirani wa karibu – hapa, ujirani wa mbali kidogo – hapo, na ujirani wa mbali – pale.

Katika ngeli ya KI-VI, kivumishi kionyeshi cha karibu huwa: hiki (umoja) na hivi (wingi), kionyeshi cha mbali kidogo huwa hicho (umoja) na hivyo (wingi) na kionyeshi cha mbali huwa kile (umoja) na vile (wingi).

*Mfano katika sentensi:*

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| i) | Kijiji hiki kina mkulima hodari. | Vijiji hivi vina wakulima hodari. |
| ii) | Chombo hicho kinaweza kuzama. | Vyombo hivyo vinaweza kuzama. |
| iii) | Kiatu kile kinapendeza. | Viatu vile vinapendeza. |

**Zoezi**

Tunga sentensi zozote sita ukitumia majina ya Ki-Vi pamoja na vivumishi vionyeshi mbalimbali.

### d) *Majina ya ngeli ya KI-VI pamoja na vivumishi vya idadi*

Vivumishi vya idadi ni maneno yanayoonyesha idadi ya watu ama vitu. Vipo vivumishi vya idadi kamili, vivumishi vya idadi ya jumla na vivumishi vya idadi ya matokeo.
Majina ya ngeli ya KI-VI huchukua viambishi ki- katika umoja na vi- katika wingi yanapotumika pamoja na vivumishi vya idadi vinavyochukua viambishi.

***Mifano***

i) Kijiko kimoja kimeoshwa.
ii) Tuletee viti vitano.
iii) Vyuo vikuu vinane vimefungwa.
iv) Vijiti vichache vitatutosha.
v) Vyombo vingi vinaletwa.

### Kumbuka

Idadi sita, saba, tisa na kumi hazichukui kiambishi chochote cha ngeli.

**Zoezi**

Tunga sentensi zozote kumi ukitumia majina katika ngeli ya KI-VI na vivumishi mbalimbali vya idadi.

### e) *Majina ya ngeli ya KI-VI pamoja na vivumishi viulizi*

Hili ni kundi la vivumishi ambalo lina maneno yatumiwayo kuulizia maswali. Baadhi ya mifano ya vivumishi viulizi ni: -pi?, na -ngapi?

Majina katika ngeli ya KI-VI huchukua kiambishi ki- katika umoja na vi- katika wingi yanapotumiwa pamoja na viulizi.

***Mifano***

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| i) | Kijiko kipi ni chako? | Vijiko vipi ni vyenu? |
| ii) | ---- | Vyetezo vingapi vinatosha? |

### Kumbuka

Kiulizi -ngapi hutumika katika wingi pekee.
Kiulizi gani? hakichukui kiambishi.
Tunasema: Kijiko gani? au vijiko gani?

**Zoezi**

Tunga sentensi zozote tano ukitumia majina ya ngeli ya KI-VI na vivumishi viulizi mbalimbali.

### f) *Majina ya ngeli ya KI-VI pamoja na vivumishi vimilikishi*

Maneno katika kundi hili la vivumishi hujibu swali mtu, kitu au jambo ni la nani? Maneno haya huwa sita pekee katika Kiswahili.

| | |
|---|---|
| -angu | -etu |
| -ako | -enu |
| -ake | -ao |

Katika ngeli ya KI-VI, kiambishi ch- hutumika katika umoja na vy- katika wingi.

***Mifano***

| | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| i) | Kijiji chetu kinapendeza. | Vijiji vyetu vinapendeza. |
| ii) | Choo chako kimechimbwa. | Vyoo vyenu vimechimbwa. |
| iii) | Kibeti chake kimepotea. | Vibeti vyao vimepotea. |

### Zoezi

Tunga sentensi zozote sita ukitumia majina katika ngeli ya KI-VI na vivumishi mbalimbali vya kumiliki.

## Maswali ya marudio

1. Kwa maneno yako mwenyewe, eleza maana ya rejesta za lugha.
2. Jaza jedwali hii kwa kuandika mifano kumi ya msamiati unaotumika katika kila rejesta iliyotajwa.

| Rejesta | Mifano ya msamiati |
|---|---|
| Burudani | |
| Michezo | |
| Mahakamani | |
| Hotelini | |
| Kanisani | |
| Bungeni | |
| Hospitalini | |

3. Eleza sifa za rejesta zifuatazo:
   a) Michezo
   b) Burudani
   c) Hotelini
   d) Sokoni
4. Pana tofauti gani kati ya rejesta ya burudani na ile ya michezo?
5. Rejesta ya hotelini ni sawa kabisa na ile ya sokoni. Je, haya ni kweli? Kwa nini?
6. a) Bainisha aina mbalimbali za michezo katika jamii.
   b) Eleza umuhimu wa michezo katika afya ya binadamu.
7. a) Taja namna mbalimbali za burudani katika jamii.
   b) Eleza umuhimu wa burudani kiafya na kiushirikiano.
8. Eleza umuhimu wa kuonyesha adabu na heshima kwa watu katika mazingira mbalimbali.
9. Bainisha rejesta zifuatazo na utaje sifa zao za kimsingi:
   a) Mheshimiwa spika, sheria hii imekiuka katiba ya nchi yetu. Mheshimiwa spika, ikiwa sheria hii itapitishwa jinsi ilivyo, patatokea migogoro.
   b) Bei rahisi...bei imeshuka...njoo mteja..karibu..usitembee kwa miguu mitupu....nunua viatu kabla bei kupanda...
   c) Maandiko yanasema kuwa wenye dhambi watachomwa motoni.
10. Linganisha na utofautishe rejesta ya bungeni na mahakamani.
11. Rejesta ya hospitalini inaweza kufaa sana katika mazingira ya jikoni. Hili ni sawa? Kwa nini?
12. Taja maneno sita ya rejesta ya utamaduni.
13. Huku ukitoa mifano, eleza rejesta ya sarufi.

14. Tunga sentensi sahihi ukitumia msamiati ufuatao:
    a) mwana mpotevu
    b) baraka
    c) mpira umekuwa mwingi
    d) densi
    e) bei ghali
    f) ankra
    g) kukata rufaa
15. Andika maneno haya katika wingi:
    a) chombo
    b) kiti
    c) kioo
    d) choo
16. Eleza muundo wa nomino za ngeli ya Ki-Vi katika umoja na wingi.
17. Tunga sentensi tano tano ukitumia majina ya ngeli ya Ki-Vi na vivumishi vilivyotolewa hapa chini katika umoja na wingi.
    a) vivumishi vya sifa
    b) vivumishi vionyeshi
    c) vivumishi viulizi
    d) vivumishi vimilikishi
18. Sahihisha makosa katika sentensi hizi:
    a) Kijiko vyangu kimenunuliwa.
    b) Vioo vikumi vitaletwa kesho.
    c) Niletee kitabu hivyo.
    d) Vyumba chote vimefagiliwa.
19. Tunga sentensi sahihi ukitumia vivumishi vilivyotolewa.
    a) vyetu
    b) vinane
    c) kile
    d) kipi
    e) vyenyewe
20. Eleza jinsi utakavyotumia ujuzi uliopata katika sura hii.

# 4 Mada kuu: Mazungumzo na mawasiliano katika shughuli mbalimbali za kijamii

## Mada ndogo: Msamiati katika kazi za jumuiya

### A Shughuli mbalimbali za jumuiya

***i) Mkutano wa kijiji chetu***


Kijiji ni mgao wa chini zaidi katika migao ya utawala. Kijiji aghalabu hujumuisha watu wanaotoka koo mbalimbali na ambao wanajuana. Watu hawa huja pamoja kufanya shughuli mbalimbali. Mikutano mbalimbali ya vijijini huweza kutumiwa kuinua hali ya maisha ya jamii ya vijiji hivyo.

***Kazi ya wanafunzi wawili wawili***

Je, kijiji chenu kinaitwaje? Je, umewahi kuhudhuria mkutano wa kijiji chenu? Jiunge na mwanafunzi mwenzako na mjadilianeni shughuli mbalimbali ambazo hufanyika katika mikutano vijijini mwenu.

***Sasa tazameni michoro iliyopo hapa chini na msome kifungu cha habari.***

Mimi ni Munyana. Leo ni siku ya mkutano wa kijiji hiki chetu. Mwenyekiti wa kijiji chetu anamwomba Nziza kufungua mkutano kwa maombi. Wanakijiji wote wanasimama na kuomba kisha wanakaa.



"Asanteni sana kwa kuitikia mwaliko wa mkutano wetu. Shughuli yetu kuu siku ya leo ni kujadiliana kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Patakuwepo upimaji wa UKIMWI ndani ya hema. Upimaji utakuwa kwa hiari yako. Kwa sasa, ninamwalika mgeni wa heshima katika mkutano wetu huu wa leo atuhutubie. Mgeni huyo ni afisa wa afya kutoka Wizara ya Afya, Bi. Abigael Uwera. Tumkaribishe kwa makofi na vigelegele." Watu wote wanasimama na kupiga makofi.

"Mabibi na mabwana, UKIMWI ni ugonjwa usiojua umri, utajiri wala umaskini. Uwe tajiri au maskini unaweza kuupata. Unamshika yeyote anayeshiriki ngono hasa bila kutumia kinga. Pia, unaweza kuambukizwa ikiwa damu yenye maradhi haya imechanganyika na damu yako. Damu hizi zinaweza kuchanganyika kwa kutumia sindano au wembe mmoja au kugusa damu ya mtu aliyeambukizwa. Tukumbuke kuwa huwezi kupata UKIMWI kwa kumsalimia au kumkumbatia au kula pamoja na mtu aliyeambukizwa."

Watu wanatazamana na kunong'onezana. Ninainua mkono na kumwuliza mgeni wa heshima ikiwa ugonjwa huu una tiba.

"La hasha! Ugonjwa huu hauna tiba. Hata hivyo, zipo dawa nzuri za kupunguza makali yake. Unapougua UKIMWI, ni sharti utumie dawa hizi tena kwa wakati uliopendekezwa bila kukosa. Ni vizuri sote tujue kuwa miili yetu ina chembechembe katika damu zetu ambazo hutukinga dhidi ya magonjwa. UKIMWI hudhoofisha chembechembe hizi. Miili yetu hukosa uwezo wa kupiga vita dhidi ya magonjwa. Hivyo, waathiriwa huweza kuuliwa na magonjwa kama vile malaria, kifua kikuu na magonjwa mengineyo."

Bi. Mutesi anainua mkono. Anapewa nafasi ya kuongea.

"Mimi ni mwathiriwa wa ugonjwa huu wa UKIMWI. Bwanangu aliaga dunia kutokana na ugonjwa huu. Wanangu wawili pia wanaugua ugonjwa huu. Sote tumekubali hali zetu. Tunatumia dawa za kupunguzia makali. Tunakula vizuri na kuendelea na shughuli zetu za kila siku. Ningependa kuwaambia wenzangu ambao wanaugua ugonjwa huu wasiogope. Ninawashukuru sana wanakijiji hiki kwa kunionyesha mapenzi na kunisaidia kukubali hali yangu. Kwa wale ambao hawana UKIMWI, nawasihi mwepuke ngono nje ya ndoa. Wasichana kwa wavulana, jiepusheni na ngono hadi mfunge ndoa. Asanteni."

Tunampigia Bi. Mutesi makofi. Wengine wanasimama na kumkumbatia. Anaonekana mwenye afya nzuri. Kumbe mtu anayeugua UKIMWI huwa na afya nzuri! Huwezi kujua anayeugua ugonjwa huu kwa kumtazama. Njia ya kipekee ni kupitia upimaji. Ninasimama na kuwahutubia wanakijiji.

"Mimi nipo tayari kupimwa. Baada ya kupimwa, nitakubali hali yangu. Ikiwa sina, nitajilinda. Baada ya kumaliza masomo na kuanza kufanya kazi, nitakubali kuchumbiwa. Nitamwambia mpenzi wangu tujipime ili tuwe na uhakika wa hali zetu. Nitakuwa mwaminifu kwake. Nipo tayari kushirikiana na wanakijiji wenzangu ili tuwapende na kuwasaidia waathiriwa wa UKIMWI. Pia, nipo tayari kujiunga na wanakiji kufanya kampeni ya kuwahamasisha wenzetu wajue kuhusu UKIMWI na waepuke kuambukizwa ugonjwa huu. Asanteni."

Wanakijiji wote wanasimama. Wanasema kwa pamoja kuwa wako tayari kujua na kukubali hali zao za UKIMWI.

"Haya, twende tukajipime wenzangu," anasema Kiongozi wa kijiji. Watu wote wanapiga foleni nyuma yake.

## Maswali

1. Bainisha msamiati wa kimsingi kifunguni kuhusu shughuli katika mkutano na uutolee maana.
   Mfano: kufungua mkutano: kutangaza rasmi kuwa mkutano umeanza.
2. Ni nini kilichokuwa kiini cha mkutano uliopo kifunguni?
3. Nani alikuwa mgeni rasmi katika mkutano wa kijiji?
4. Eleza mambo muhimu yanayojitokeza katika kifungu hiki.
5. Toa muhtasari wa kifungu cha habari ulichosoma hapo juu katika aya moja.

### *Kazi ya kikundi*

Jiunge na wenzako katika kikundi. Nyinyi ni wanachama wa kijiji kimoja. Mmeandaa mkutano. Jadilianeni kuhusu mambo mbalimbali mtakayofanya ili kuangamiza umaskini katika kijiji chenu.

### *ii) Sherehe ya harusi ya rafiki yangu*


### *Kazi ya wanafunzi wawili wawili*

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Jadilianeni kuhusu mambo muhimu ambayo hufanyika katika sherehe ya harusi. Kwa mfano:


1. Watu huja pamoja kutengeneza hema la wageni.
2. Maarusi huimbiwa na kuchezewa.

Baada ya kujadiliana mambo muhimu katika harusi, simulianeni kuhusu sherehe ya harusi mliyohudhuria.

***Tazama michoro hii. Je, mambo gani yanafanyika?***





***Someni mazungumzo haya na mjibu maswali chini yake***.

SHEMA: Hujambo mwenzangu?

TONA: Sijambo, ulikuwa wapi wiki nzima?

SHEMA: Nilihudhuria harusi ya rafiki yangu.

TONA: Kumbe! Ndiyo sababu una furaha tele.

SHEMA: Mbona nisiwe na furaha? Ndoa ni jambo linalowafurahisha watu wengi. Kutajwa tu kwa neno hili hufanya roho za kila mtu kusisimka kwa furaha.

TONA: Haya! Hata mimi ipo siku nilikuwa mpambe nilipokuwa mdogo. Bibi. harusi alivaa mavazi yake maalumu ya kupendeza kweli. Sisi wapambe pia tulinunuliwa viatu na nguo za kupendeza. Sisi na bibi harusi tulipambwa tukapambika. Nieleze kuhusu harusi hiyo uliyohudhuria.

SHEMA: Sikujua kuwa Ganza angeweza kumchumbia msichana mrembo kama yule. Aliponiambia eti posa yake imekubalika nilidhani ananitania. Aliniandikia barua kunieleza eti amepeleka mahari. Bado sikuamini hadi aliponitumia kadi ya kunialika harusini.

TONA: Ehe...

SHEMA: Mimi nilifika mapema na wenzangu kumsaidia rafiki yangu. Tulitengeneza mahema na kupanga viti hemani. Wengine walirembesha mahema kwa maua, baluni, na mapambo yenye rangi mbalimbali. Mahema yale yalivutia kwelikweli. Wengine walikuwa jikoni wakiandaa vyakula nao wengine walipokea wageni ambao walianza kuwasili mapema. Tukakodisha magari ambayo yangemsafirisha bwana na bibi harusi. Tukahakikisha kuwa vyombo vya burudani vipo katika hali sawa tayari kuwatumbuiza wageni.

TONA: Ahaa! Bibi harusi alikuwa wapi wakati huu wote?

SHEMA: Ah! Kwani hujui? Bibi harusi alikuwa mahali kusikojulikana. Huko alikuwa na wapambe ambao walikuwa wakimrembesha.

TONA: Ehe...

SHEMA: Baada ya maandalizi, nikajiunga na wanaume ambao huandamana na bwana harusi. Pale, tulipewa mafunzo ya jinsi ya kutembea na kumsindikiza bwana harusi. Tukapima suti zetu nyeusi na kujaribu

kutembea kwa viatu vyetu vipya. Bwana harusi naye akajaribu kuvaa pete ili ahakikishe kuwa inamtosha. Kila kitu kikawa shwari.

TONA: Nieleze mambo yaliyojiri siku ya harusi.

SHEMA: Harusi hiyo ilianza kwa watu kukaa kanisani kwa matarajio makubwa huku wakinong'onezana. Mara mfawidhi akatangaza kuwa tusimame kwa kuwa bibi harusi sasa anaingizwa kanisani. Bibi harusi akasindikizwa kanisani na babake na kupelekwa pale mbele alipokuwa akisubiriwa na mchumba wake pamoja na mchungaji. Hapo, waliapishwa na halafu kuvishana pete na mwishowe kutangazwa bibi na bwana. Wacha sasa sherehe kamili zianze. Waliokula walikula na waliokunywa walikunywa. Nao waliocheza walicheza na waliofanya urafiki kwa matarajio ya kufanya ndoa kama hiyo walifanya.

TONA: Ama kwa kweli harusi hiyo ilifana kweli! Asante.

SHEMA: Karibu.

**Maswali**

1. Kwa nini ndoa ni jambo la kufurahisha?
2. Eleza maana ya msamiati uliowekewa wino nzito.
3. Tunga sentensi sahihi ukitumia msamiati ulioeleza hapo juu.
4. Eleza mambo muhimu yanayofanyika harusini kwa mujibu wa kifungu hiki.
5. Eleza umuhimu wa ushirikiano katika jamii kwa kurejelea matukio kifunguni.
6. Toa muhtasari wa kifungu hiki cha habari katika aya moja.

### *iii) Mazishi*

Mazishi ama maziko ni shughuli za kuzika mfu au wafu. Mfu ni mtu aliyeaga dunia. Shughuli hizi huendeshwa kutegemea utamaduni na imani za kidini za wahusika au waathiriwa.

***Kazi ya wanafunzi wawili wawili***


Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Tazameni mchoro ulio kwenye ukurasa ufuatao. Je, ni shughuli gani inayofanywa? Jadilianeni kuhusu shughuli ambazo hufanywa wakati wa mazishi katika jamii yenu.

***Soma kifungu kilichopo hapa chini na ujibu maswali chini yake.***

Sikujua kuwa sigara huua hadi nilipompoteza mjomba wangu mwaka jana. Mjomba aliaga dunia kutokana na ugonjwa wa saratani ya mapafu. Alipenda sana kuvuta sigara. Aliaga dunia katika hospitali moja jijini Kigali. Punde tu alipofariki, mwili wa mjomba ulipelekwa katika mochari. Huko, mwili wake ulisafishwa na wahudumu wa mochari na kuwekwa katika jokofu.

Jamaa na marafiki walikuja pamoja kumpa mjomba heshima zake za mwisho. Wanakijiji na watu kutoka mbali walishiriki katika shughuli mbalimbali kufanikisha mazishi ya mjomba.

Wanakijiji walichanga pesa za kulipia gharama za mochari na shughuli nyinginezo. Wengine walijitolea kutengeneza jeneza zuri la kumzikia mjomba. Wengine walinunua sanda. Wengine walichimba kaburi. Kila mtu alishiriki katika shughuli hizi kadiri ya uwezo wake.



Mwili wa mjomba uliondolewa kwenye mochari baada ya wiki moja. Mwili huo ulisafirishwa hadi kanisani. Alifanyiwa ibada ya wafu. Jamaa na marafiki walifika kanisani kushiriki katika ibada hiyo. Baada ya maombi, watu walipewa ruhusa ya kutazama mwili wa mjomba. Hali ya huzuni ilitanda kanisani.

Baada ya ibada, mwili huo ulisafirishwa nyumbani kwake. Mimi na jamaa za mjomba tulihuzunika. Wanakijiji na marafiki zetu walitufariji.

Siku ya mazishi ilipofika, ibada ya wafu iliandaliwa. Mchungaji aliendesha shughuli akishirikiana na familia ya marehemu mjomba. Mchango wa kusaidia familia ya marehemu mjomba pia ulifanywa. Wanakijiji na wageni walitoa michango yao.

Hatimaye wakati wa kuteremshwa kwa jeneza kaburini ulifika. Baada ya maombi mafupi kando ya kaburi, jeneza lilitiwa ndani ya kaburi. Mchungaji alituhutubia.

"Tunasikitika kuwa marehemu aliaga dunia kutokana na uvutaji wa sigara. Nawasihi vijana kwa wazee mwepuke uraibu wa sigara na dawa za kulevya. Tumempoteza mwenzetu aliyekuwa na bidii ya mchwa. Tuige tabia zake nzuri na kuepuka zile mbaya. Ikiwa pana mtu ambaye mfu huyu alikuwa na deni lake, aseme sasa."

Hakuna aliyeinua mkono. Mhubiri alifanya ombi la mwisho kisha shughuli za kufunika kaburi zikaanza. Familia ya mjomba ilikuwa ya kwanza kuweka mchanga kwenye kaburi. Baadaye, wanakijiji walisaidia katika kufunika kaburi.

"Asanteni kwa kushiriki katika mazishi haya. Tunamwomba Mungu amlaze mahali pema peponi," mhubiri alisema kisha watu wakaondoka.

Wageni kutoka mbali walipewa vyakula na vinywaji. Baadaye waliondoka kwenda zao.

## Maswali

1. Kwa maneno yako mwenyewe, eleza maana ya mazishi.
2. Bainisha na utoe maana ya msamiati mbalimbali kuhusu mazishi kifunguni.
3. Tunga sentensi ukitumia msamiati uliotajwa hapo juu.
4. Eleza shughuli muhimu za mazishi zilizotajwa kifunguni.
5. Kwa maneno yako mwenyewe, eleza mambo muhimu kifunguni katika aya moja.

### Kazi ya kikundi

Jiunge na wanafunzi wenzako. Jadilianeni kuhusu utaratibu wa mazishi ya kienyeji katika sehemu mtokako.

### iv) Kazi ya umuganda

*Umuganda* ni mkusanyiko wa watu kutoka vijiji mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa taifa. Mnamo siku ya Jumamosi ya mwisho kila mwezi, Wanyarwanda wote walio na miaka kati ya kumi na minane na sitini na mitano hukusanyika katika makundi mbalimbali kushiriki katika kazi za *umuganda*.

### Kazi ya wanafunzi wawili wawili

Jiunge na wanafunzi wenzako. Jadilianeni kuhusu shughuli mbalimbali ambazo hufanywa siku ya kazi ya *umuganda.*

***Tazama michoro hii kuhusu shughuli mbalimbali za umuganda na usome kifungu cha habari.***



Wanyarwanda hushiriki katika shughuli mbalimbali siku ya kazi ya *umuganda. Umuganda* huandaliwa kila Jumamosi ya mwisho ya mwezi. Kila kijiji huamua shughuli muhimu wanazostahili kufanya. Wao huchagua shughuli ambayo ina umuhimu kwao.

Baadhi ya wanakijiji huweka vizuizi vya mmomonyoko wa udongo kwa kuchimba mitaro. Wengine wanajaza mitaro hiyo kwa magunia yaliyojaa mchanga. Wengine wanafunika magunia hayo kwa mchanga. Mvua inaponyesha, maji tu ndiyo hupita lakini udongo hubakia kwenye mitaro na magunia yaliyowekwa. Hivyo, rutuba hubakia kwenye udongo nayo ardhi huweza kutumiwa tena katika shughuli za kilimo.



Wanyarwanda pia huja pamoja kusafisha maeneo wanamoishi. Watu hupewa majukumu mbalimbali wakati wa usafishaji. Baadhi ya watu huondoa taka kwenye mitaro ya maji machafu. Wengine hupewa jukumu la kuokota taka zilizotapakaa. Wengine huchoma taka hizo. Nao baadhi ya watu kufyeka nyasi zilizomea kando ya mitaro na maeneo mengineyo. Shughuli hizi hulenga kudumisha usafi katika miji na vijiji vyetu.

Wanyarwanda pia hupanda miti siku ya kazi ya *umuganda*. Wao hupanda miti hasa kwenye ardhi tambarare. Wengine hunyunyizia miche maji. Miti mingi hupandwa na wanakijiji mbalimbali kwa kuwa miti ni muhimu katika mazingira yetu.





Mbali na hayo, baadhi ya Wanyarwanda hulima na kupalilia mashamba yao. Wao huja pamoja kwa ajili ya kuwasaidia wenzao hasa wazee katika mashamba yao.

### Maswali

1. Eleza umuhimu wa kazi ya *umuganda* katika jamii zetu.
2. Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Kila mwanafunzi asimulie mambo muhimu yanayojitokeza katika shughuli ya kijamii aliyoshiriki zaidi.

### *Kazi ya kikundi*

Jiunge na wanafunzi wenzako. Jadilianeni kuhusu shughuli za kijamii mlizoshiriki kisha mziwasilishe mbele ya darasa.


## B Namna sahihi ya kuuliza maswali

Kufikia sasa, umejifunza mengi kuhusu shughuli mbalimbali za kijamii. Unaposhiriki katika mazungumzo kuhusu shughuli hizi za kijamii au mambo mengineyo, unaweza kuuliza maswali mbalimbali.

Katika Kiswahili, zipo namna mbalimbali za kuuliza swali. Maneno ambayo hutumiwa kuulizia maswali huitwa viulizi. Zipo aina mbalimbali za viulizi. Je, unakumbuka viulizi hivyo?

Viulizi huuliza maswali kuhusu jinsi kitendo kilivyotendeka (vipi), wakati kitendo kilipofanyika (lini), mahali kitendo kilipofanyika (wapi), aliyetenda kitendo (nani), kitendo chenyewe (nini), idadi (-ngapi) na namna ya kitendo au kifaa (gani). Hapa, maneno yaliyowekwa kwenye mabano ndiyo viulizi vinavyotumiwa kuulizia maswali.

***Soma kifungu hiki ili ujifunze mengi kuhusu namna sahihi ya kuuliza maswali.***



INEZA: Wenzangu, kwa nini hamkuhudhuria mkutano wa kijiji uliokuwepo Jumamosi iliyopita?

TONA: Shoga yangu, wewe unafahamu kuwa mamangu mzazi hajisikii vizuri. Sasa, siku hiyo ilibidi niondoke niende kumtazama.

NDOLI: Nami wenzangu sina sababu ya kutohudhuria bali nilisahau tu na kutanabahi mkutano umekwisha. Mambo gani yalijiri mkutanoni humo?

INEZA: Lo! Tulifanya shughuli mbalimbali...

TONA: Samahani kwa kukutatiza usemi. Shughuli hizo mlizifanya wapi?

INEZA: Tulikusanyika katika uwanja wa mkutano wa kijiji kisha tukajigawa katika vikundi mbalimbali. Kila kikundi kilishiriki kufanya kazi katika maeneo mbalimbali.

NDOLI: Kwa jumla, vikundi vilikuwa vingapi?

INEZA: Vikundi vyote vilikuwa tisa.

TONA: Nani aliongoza kikundi chenu?

INEZA: Kikundi chetu kiliongozwa na Bi. Kabatesi.

NDOLI: Nini alichowapa kabla ya kazi?

INEZA: Alitupa vifaa mbalimbali.
TONA: Mlipewa vifaa gani?
INEZA: Tulipewa mapanga na majembe.
NDOLI: Mlifanya kazi ipi katika kikundi chenu?
INEZA: Tulifyeka na kulima shamba la nyanyake Teta.
TONA: Mkutano ujao utakuwa lini?
INEZA: Mkutano ujao utakuwepo Jumamosi ya mwisho, mwezi ujao. Msikose kuhudhuria kikao.
NDOLI: Ni vifaa gani vitahitajika katika kazi hiyo ya umuganda?
INEZA: Vifaa vitakavyohitajika vitakuwa fagio, ndoo, majembe, mapanga na mafyekeo. Msikose kushiriki.
TONA na
NDOLI: Tukijaaliwa tutakuwepo. Asante.

## Kazi ya wanafunzi wawili wawili

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Tungeni maswali sahihi kuhusu shughuli mbalimbali za kijamii mkitumia viulizi vifuatavyo. Sahihishianeni majibu yenu.

a) vipi
b) lini
c) wapi
d) nani
e) nini
f) -ngapi
g) gani

## Kazi ya kikundi

Jiunge na wanafunzi wenzako katika kikundi. Rejeleeni vifungu vya habari mlivyosoma kuhusu shughuli mbalimbali za kijamii katika vipindi vilivyopita. Tumieni viulizi mbalimbali kuulizana maswali kwa zamu kutokana na yaliyomo kwenye vifungu hivyo. Anayeulizwa ajibu kila swali kwa usahihi. Anapopata jibu, naye amwulize mwenzake swali.

*Mifano*

1. Afisa wa afya kutoka wizara ya kilimo alisema nini kuhusu UKIMWI?
2. Nani alifanya harusi?

## C Aina saba za maneno

Lugha ya Kiswahili huwa na aina saba kuu za maneno. Maneno haya hutambuliwa kulingana na muundo na matumizi yake katika sentensi. Maneno hayo saba huwa nomino, vitenzi, vielezi, vivumishi, viwakilishi, viunganishi na vihisishi.

## Nomino

Kufikia sasa, umejifunza mengi kuhusu aina mbalimbali za nomino. Je, unazikumbuka?

Tunaweza kutumia nomino mbalimbali kutaja mtu au watu walioshiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii. Pia, tunaweza kutumia nomino kutaja vifaa mbalimbali vilivyotumika kutendea shughuli fulani za kijamii, mahali shughuli hizo zilipofanyika na kadhalika.

Tazama aina mbalimbali za nomino katika jedwali na usome mifano kando yake.

| | Aina za nomino | Matumizi |
|---|---|---|
| 1. | **Nomino za pekee**: Hutaja vitu au watu wenye sifa za kipekee. Zinapoandikwa, lazima zianze kwa herufi kubwa hata zikiwa katikati ya sentensi. | a) Tunamwomba Abatoni atufungulie mkutano kwa maombi.<br>b) Tutasafisha mitaa mbalimbali jijini Kigali wakati wa kazi ya *umuganda* siku ya Jumamosi.<br>c) "Mungu atuongoze tunapoanza kazi hii ya kusafisha kijiji," mhubiri alisema.<br>d) Tulisoma katika somo la Kilimo kwamba ikiwa wanakijiji watashirikiana katika kilimo, tutapata mavuno mengi. |
| 2. | **Nomino za kawaida**: Hizi hutaja vitu vya kawaida vinavyopatikana kwingi. | a) Kasisi hatakuwepo katika ibada ya leo.<br>b) Tuliongozwa na kiongozi wa kijiji kupanda miti uwanjani.<br>c) Nipe jembe hilo ning'oe magugu haya.<br>d) Nitaenda nyumbani kesho kushiriki katika harusi ya rafiki yangu. |
| 3. | **Nomino za jamii**: Hutaja jumla ya vitu vingi au vitu katika makundi ambapo jina katika umoja lina wingi. | a) Umati umekusanyika kufanya kazi ya *umuganda*.<br>b) Wanakijiji wameleta tita la kuni.<br>c) Tuliwapa kina mama korija ya leso walipotusaidia kulima shamba letu. |

| | | |
|---|---|---|
| 4. | **Nomino za wingi**: Hutaja vitu ambavyo haviwezi kugawika na kuwa kitu kimoja kimoja. | a) Wanakijiji walipewa sukari na chumvi kama shukrani ya kazi nzuri.<br>b) Mvua ilinyesha tulipokuwa tukienda msikitini.<br>c) Wanakijiji walipewa ng'ombe wa maziwa.<br>d) Tulichimba mitaro ya kupitisha maji machafu. |
| 5. | **Nomino za dhahania**: Hutaja vitu vinavyofikirika au visivyoweza kuguswa. | a) Umoja na ushirikiano wetu utatuletea manufaa mengi.<br>b) Ukarimu wa wanakijiji ulifanikisha harusi yetu. |

## Zoezi A

Soma kifungu kifuatacho cha habari. Bainisha na uainishe nomino mbalimbali katika kifungu.



Ama kwa kweli, ndoa ni jambo linalowafurahisha watu wengi. Kutajwa tu kwa neno hili hufanya roho za watu wengi kusisimka. Takriban watu wote husikia neno hili kwa upendo. Kwa nini upendo? Unapotajiwa neno hili, fikira ya kwanza kukujia ni raha. Watu husikia raha kwa sababu huwepo maakuli na vyakula vingi vya bwerere. Pia, harusi huleta heshima na umaarufu.

Kabla ya kufanya harusi, yapo mambo mengi ambayo hufanyika. Kwanza kabisa, ni sharti mchumba apatikane. Halafu ni sharti ujumbe wa posa upelekwe na mshenga

kwa kina mchumba. Ukikubalika, mahari huzungumziwa na kulipwa. Ni baada ya haya yote tu ambapo siku ya harusi huwekwa.

Nayo matayarisho ya harusi huwa mengi. Bi harusi pamoja na wapambe wake sharti wanunuliwe mavazi mbalimbali ya harusi. Mavazi haya huwa pamoja na nguo maalumu za Bi harusi na wapambe wake. Pia ni sharti pawepo jozi mpya za viatu, pete ya harusi, mashada ya maua na kadhalika. Matayarisho mengine ni usafiri, waendesha harusi, kwaya, na matayarisho mengine mbalimbali.

Hatimaye huja siku yenyewe ya harusi. Mfano mzuri wa siku hii ni harusi ya rafiki yangu Iliza iliyofanyika Ijumaa jijini Kigali. Umati wa watu ulihudhuria harusi hiyo. Baada ya ibada, tulienda katika Hoteli ya Serena ambapo sherehe kamili iliandaliwa.

**Zoezi B**

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Tungeni sentensi zinazohusu shughuli mbalimbali za kijamii kwa kutumia nomino mbalimbali mlizobainisha kifunguni.

## Vitenzi

Kitenzi ni neno lielezalo jambo la kutendwa au kufanywa.

Je, unakumbuka mifano mbalimbali ya vitenzi ulivyosoma?

Tunaposhiriki katika mazungumzo kuhusu shughuli mbalimbali za kijamii, ni sharti tutumie vitenzi mbalimbali.

***Tazama aina mbalimbali za vitenzi katika jedwali na usome matumizi yake.***

| | Aina ya vitenzi | Matumizi |
|---|---|---|
| 1. | **Vitenzi halisi:** Hivi ni vitenzi ambavyo vinajitosheleza kimaana. Vitenzi hivi hutoa habari kamili iliyokusudiwa. | a) Tunashirikiana kijijini mwetu.<br>b) Anaongoza mkutano.<br>c) Waombolezaji wanaimba.<br>d) Njoo msikitini Ijumaa. |
| 2. | **Vitenzi vikuu na vitenzi visaidizi**: Hutokea pamoja katika sentensi iwapo kuna mfuatano wa vitenzi katika sentensi hiyo. Kitenzi au vitenzi vinavyotokea mwanzoni huwa vitenzi visaidizi ilhali kitenzi cha mwisho huwa kitenzi kikuu. | a) Wanakijiji walikuwa wanafagia barabara.<br>walikuwa – kitenzi kisaidizi<br>wanafagia – kitenzi kikuu<br>b) Majembe yalikuwa yangali yanaletwa.<br>yalikuwa – kitenzi kisaidizi<br>yangali – kitenzi kisaidizi<br>yanaletwa – kitenzi kikuu |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | **Vitenzi vishirikishi**: Hivi ni vitenzi ambavyo hushirikisha vitu viwili kihali, kitabia au kimazingira katika sentensi. | a) Bibi harusi ndiye yule.<br>b) Wao si wavivu.<br>c) Watu wangali shambani.<br>d) Ibada ilikuwa jana.<br>e) Ufanisi wetu u mikononi mwetu. |

## Zoezi A

Soma kifungu kifuatacho cha habari. Bainisha na uainishe vitenzi mbalimbali vilivyomo kifunguni.



"Tuharakishe. Ujenzi wa choo umeanza," Ikirezi aliniambia. Alikuwa akihema.

"Mimi ni mgonjwa. Ningali ninaumwa na tumbo lakini nitajikaza," nilimjibu. Hatimaye tuliwasili penye mkutano. Watu walikuwa wamejigawa katika vikundi tayari kwa kazi mbalimbali.

"Tazama. Kila mtu ameanza kujenga choo isipokuwa sisi," nilimwambia Ikirezi. Kiongozi wa kijiji alinisikia.

"Msiwe na shaka. Nyinyi mtaokota taka zote zilizopo pale uwanjani. Baada ya hapo, mtafagia kando ya barabara. Kazi hiyo si ngumu," kiongozi wa kijiji alisema.

Mimi na Abatoni tulitafuta fagio. Tuliongezewa vijana watatu ili watusaidie kufanya kazi hiyo. Tulifurahia sana kushirikiana na wanakijiji.

## Zoezi B

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Tungeni sentensi zinazohusu shughuli mbalimbali za kijamii kwa kutumia vitenzi mbalimbali mlivyobainisha kifunguni.

## Vielezi

Vielezi pia huitwa viarifa nayo ni maneno yafafanuayo vitenzi, vivumishi au vielezi. Tunaweza kutumia vielezi kueleza jinsi shughuli mbalimbali za kijamii zilivyofanywa. Mathalan, ukisema: *Anafanya kazi haraka* neno *haraka* linaeleza jinsi kazi inavyofanywa.

Je, unakumbuka vielezi ulivyosoma?

***Tazama aina mbalimbali za vielezi katika jedwali na matumizi yavyo.***

| | Aina ya vielezi | Matumizi |
|---|---|---|
| 1. | **Vielezi vya namna au jinsi**: Haya ni maneno ambayo huarifu jinsi ya kutendeka mambo. | a) Wanakijiji hufanya kazi kwa bidii pamoja.<br>b) Usisumbuke bure! Tutakusaidia.<br>c) Tutaimba kwa furaha siku ya harusi yako.<br>d) Tembea haraka tumechelewa mkutanoni. |
| 2. | **Vielezi vya wakati**: Nayo haya ni maneno yanayofafanua ama kueleza wakati wa kutokea kitendo. | a) Mkutano ulianza mapema.<br>b) Tutaondoka hapa saa kumi jioni.<br>c) Wanakijiji hiki walianza kushirikiana zamani. |
| 3. | **Vielezi vya kiasi/idadi**: Vielezi vya kiasi ni namna ya maneno ambayo hufafanua vitenzi kwa kujulisha tendo limetokea mara ngapi. | a) Kazi ya umuganda hufanywa mara moja kwa mwezi.<br>b) Nilipoenda harusini mara ya kwanza nilikula sana hadi nikaumwa na tumbo. |
| 4. | **Vielezi vya mahali**: Haya nayo ni maneno ama mafungu ya maneno yanayofafanua panapotokea kitendo. | a) Fyekeni nyasi zilizopo kando ya mitaro.<br>b) Nitawahutubia watu wote waliopo pembeni mwa uwanja.<br>c) Tutamfungia ng'ombe wake nyuma ya boma.<br>d) Twende uwanjani. |

## Zoezi A

Soma kifungu kifuatacho cha habari. Bainisha na uainishe vielezi mbalimbali kifunguni.

Ilikuwa siku ya Jumamosi. Ilikuwa siku ya kuwasaidia wazee kuandaa mashamba yao na kupanda mbegu. Wanakiji wote waliamka alfajiri. Mimi pia nilijiunga nao kwa hiari.  Wa kwanza kusaidiwa aliitwa Abera. Tulitembea upesi kuelekea shambani mwake ili tufike mapema. Tulipofika ndani ya shamba, kila mtu alipewa jukumu. Wengine walifyeka majani marefu yaliyomea pembeni mwa shamba.

Waliyafyeka majani kwa panga. Wengine walilima kwa jembe la mkono. Wengine waliondoa magugu hatari kutoka shambani na kuyachoma kwa moto. Sisi tulipanda mbegu. Kila mtu alipewa kazi ya kufanya mara kwa mara. Hakuna aliyekaa bure. Sote tulifanya kazi kijeshi.



## Zoezi B

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Tungeni sentensi zinazohusu shughuli mbalimbali za kijamii kwa kutumia vielezi mbalimbali mlivyobainisha kifunguni.

### Vivumishi

Kwa kawaida, kivumishi ni neno linaloongezea nomino maana. Vivumishi vinaweza kutumiwa kuelezea sifa za mtu au watu walioshiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii. Pia, tunaweza kutumia vivumishi kueleza sifa za vifaa vilivyotumika katika shughuli za kijamii na kadhalika.

Kumbuka kuwa vivumishi ni sharti vitumiwe pamoja na nomino.

Je, unakumbuka vivumishi gani ulivyosoma?

***Tazama aina mbalimbali zifuatazo za vivumishi huku ukisoma matumizi yaliyotolewa.***

| | Aina ya vivumishi | Matumizi |
|---|---|---|
| 4. | **Vivumishi vya sifa**: Haya ni maneno yatajayo tabia au sifa za kitu. | a) Mnyarwanda mwema hushiriki katika shughuli zote za kijamii.<br>b) Tutapanda nyasi nyingi katika ardhi tambarare siku ya kazi ya *umuganda*.<br>c) Wanakijiji hodari walikunywa maji safi baada ya kulima vizuri. |
| 5. | **Vivumishi vya pekee**: Hutoa habari kuhusu nomino kwa njia ya kipekee. | a) Watu wenye mioyo ya ushirikiano hufaulu wenyewe.<br>b) Tutaondoa taka kwenye mitaro, kujengea wazee nyumba na shughuli nyinginezo.<br>c) Harusi yoyote huleta watu wote pamoja kusherehekea kufungwa kwa ndoa.<br>d) Sihitaji fyekeo jingine.<br>e) Wanakijiji walishirikiana kutupa msaada wowote siku ya mazishi. |

| | | |
|---|---|---|
| 6. | **Vivumishi vionyeshi**: Hutumiwa kuonyesha alipo mtu au kitu, yaani kuonyesha ujirani. | a) Niliamua kuwa mtu mwema baada ya kushiriki ibada katika msikiti huo.<br>b) Nitafyeka nyasi hizi.<br>c) Wanakijiji wawa hawa wanapenda kusaidiana.<br>d) Mitaro ile ile itasafishwa kesho.<br>e) "Asanteni sana kwa umoja huo," mgeni wa heshima alisema. |
| 7. | **Vivumishi vya idadi**: Haya ni maneno yanayoonyesha idadi ya watu ama vitu. | a) Tuletee mapanga sita na maji kidogo.<br>b) Nilikuwa wa kwanza kufika mkutanoni.<br>c) Umoja wetu utatuletea manufaa tele.<br>d) Kidole kimoja hakivunji chawa. |
| 8. | **Vivumishi viulizi**: Hili ni kundi la vivumishi ambavyo hutumia viulizi kuulizia swali. | a) Ni kiongozi yupi anatusimamia?<br>b) Miche ipi inapandwa hapa?<br>c) Watu wangapi wamealikwa harusini?<br>d) Tunapaka nyumba gani rangi? |
| 9. | **Vivumishi vimilikishi:** Vivumishi katika kundi hili hujibu swali mtu, kitu au jambo ni la nani? | a) Ushirikiano wenu unaleta maendeleo katika nchi yetu.<br>b) Azimio langu ni kuwasaidia wasiojiweza katika jamii.<br>c) Miti yao inanyunyiziwa maji. |

## Zoezi A


Soma kifungu kifuatacho cha habari. Bainisha na uainishe vivumishi mbalimbali katika kifungu.

Ni taifa gani ambalo halipendi maendeleo? Ama ni watu wepi ambao hawapendi kuendelea? Sisi Wanyarwanda tunapenda maendeleo ili taifa letu likue hata zaidi. Nchi yenye watu wanaopenda maendeleo hukua haraka. Ili jambo hili liwezekane, ni sharti tufanye mambo kadhaa.

Kwanza kabisa, nchi yetu haiwezi kukua bila masomo. Lazima watoto wote waliofika umri wa kuenda shule waende shuleni. Nasi wanafunzi wenyewe tulenge kufikia elimu ya chuo kikuu. Ili kufaulu masomoni, ni sharti tushirikiane na jamii. Ujuzi huu tunaopata shuleni ni sharti tuutumie kusaidia jamii. Tusingoje hadi tumalize chuo kikuu ndipo tuanze kujenga taifa hili letu.

Pili, usafi ni jambo muhimu sana. Jamii haiwezi kujenga taifa lake kama haina afya nzuri. Je, kina nani wanafaa kudumisha usafi huu? Watu hao si watu wengine bali ni mimi na wewe. Kila mmoja wetu ahakikishe kuwa anaishi katika mazingira safi kila siku.

Tatu, kuna shughuli ya mikutano tofauti tofauti ya kutangaza na kuhimiza maendeleo. Jamii inapokutana na kuelezwa maendeleo yaliyopatikana, hupata motisha ya kufanya mengi zaidi. Hali hii basi huwa ni msukumo muhimu katika kazi zao. Vilevile, vijiji hushindana katika maendeleo. Mashindano ya dhati kati ya vijiji huwa ni motisha nzuri ya ujenzi wa taifa. Kumbuka kuwa vijiji vikipiga hatua mbele nalo taifa hufanya vivyo hivyo.



Jambo jingine linalohitajika katika huu ujenzi wa taifa ni kuwa na mikakati kabambe ya kushughulikia mikasa. Mathalan, tumejitayarisha vipi kukabiliana na mkurupuko wa magonjwa hatari na njaa? Ni sharti tushirikiane ili kuibuka na mikakati kabambe ya kukabiliana na mikasa kama hii.

Ili haya yote na mengine mengi yafaulu, umoja na ushirikiano wetu lazima uwepo. Kumbuka kuwa kidole kimoja hakivunji chawa nalo jiwe moja haliinjiki chungu.

**Zoezi B**

Jiunge na mwanafunzi mwenzako. Tungeni sentensi zinazohusu shughuli mbalimbali za kijamii kwa kutumia vivumishi mbalimbali mlivyobainisha kifunguni.

## Viwakilishi

Viwakilishi ama vibadala ni maneno kamili ama viambata (sehemu za maneno) vinavyosimama badala ya majina. Je, unakumbuka viwakilishi ulivyosoma?

Tazama aina mbalimbali hizi za viwakilishi katika jedwali lifuatalo huku ukisoma matumizi yake.


| | Aina ya viwakilishi | Matumizi |
|---|---|---|
| 1 | **Viwakilishi nafsi**: Husimamia nafsi za nomino inayozungumziwa katika umoja au wingi. | a) Mimi ninapenda kufanya kazi na wenzangu.<br>b) Yeye anaongoza mkutano wa leo.<br>c) Wao wanachanga pesa zitakazotumiwa katika mazishi.<br>d) Tutapanda miti siku ya *umuganda*.<br>e) Wewe utatuletea fyekeo.<br>f) Mnafunga ndoa lini? |

| | | |
|---|---|---|
| | | g) Kitasafishwa kwa maji.<br>h) Imepandwa na wanakijiji.<br>i) Anakuja kanisani kuomba. |
| 2 | **Viwakilishi vitokanavyo na vivumishi**: Endapo kivumishi husika kimetumika badala ya nomino, kivumishi hicho kinakuwa kiwakilishi. Nacho kiwakilishi hicho huchukua jina la kivumishi hicho. | a) Huyo huyo atatuongoza katika ibada.<br>b) Hivi vinasafishwa.<br>c) Gani inatengenezwa?<br>d) Wangu nimewapa waliofiwa.<br>e) Wote wanakuja. |

**Zoezi**

Soma kifungu kifuatacho cha habari. Bainisha na uainishe viwakilishi mbalimbali katika kifungu.

Waliosema kuwa umoja ni nguvu hawakukosea bali waligonga ndipo. Mimi ninaamini sana katika msemo huu. Ninaamini kwa sababu ya mambo niliyoshuhudia nilipompoteza mama mzazi. Mama alikuwa mtu wa watu. Aliwapenda wanakijiji nao wanakijiji wa mbali na wa karibu wakampenda. Kifo chake kiliwashtua wengi. Kilifanya kijiji kizima kiomboleze. Watu walifurika nyumbani kwetu kutupa pole. Kuwepo kwao kulituliwaza. Licha ya machungu, tulihisi kuwa hatupo peke yetu. Nani angekosa kupata nguvu katika hali kama hii? Msiba huleta unyonge. Wetu ulileta nguvu kutokana na ushirikiano huo.



Mbali na kutupa moyo, wanakijiji waligharamia mazishi. Wao walisimamia kila kitu. Sisi tulishuhudia tu mambo yakitendeka. Hawakutaka tushiriki katika shughuli zozote kutokana na huzuni. Waliopika walipika. Waliotengeneza jeneza walifanya hivyo tena kwa ustadi. Waliochimba kaburi hawakusita kumaliza mapema. Kila kitu kilifanywa kwa haraka na ustadi. Mama akalazwa na kupewa heshima zake za mwisho kwa ushirikiano wa wanakijiji. Wao hao wakatuchangia pesa za matumizi ya baadaye. Tulikosa maneno ya kuelezea furaha na shukrani zetu kwao. Kweli, umoja ni nguvu.

## Viunganishi

Haya ni maneno yanayotumika kuunganisha maneno, vikundi vya maneno au sentensi ili kupitisha ujumbe fulani.

*Tazama mifano hii ya viunganishi.*

1. Tulikuja pamoja ili kuwafariji waliofiwa.
2. Mkutano uliahirishwa kwa sababu mvua kubwa ilinyesha.
3. Mbali na kufagia, wanakijiji hupanda miti na kujenga vizuizi vya kukinga mmomonyoko wa udongo.
4. Tulisameheana maadamu tulishiriki kazi pamoja.

**Zoezi**

Soma kifungu kifuatacho. Bainisha aina mbalimbali ya viunganishi vilivyotumika.

Kila jamii huwa na ngoma yao waipendayo. Aghalabu wao huipenda kwa sababu wameirithi kutoka kwa mababu zao. Mathalan, Waswahili hupenda sana msondo. Je, nyinyi mnapenda ngoma gani katika jamii yenu?



Kwa kawaida, ngoma kama hiyo huchezwa na wale waliopo sasa. Baadaye hupitishwa kwa vizazi vijavyo. Kwa namna hiyo, ngoma husika huja ikawa sehemu kuu ya utamaduni wao japo baadhi ya mambo ya kisasa huongezwa. Mambo hayo ya kisasa huongezwa pasipo kubadilisha asilia ya ngoma hizo.

Sisi Wanyarwanda pia tunapenda ngoma zetu za kiasili. Itokeapo shughuli muhimu, sisi hushiriki katika kuimba na kucheza ngoma zetu za kitamaduni.

Hivyo basi, ngoma huchezwa kama njia mojawapo ya kujiburudisha. Shughuli hii huambatana sana sana na sherehe fulani kama vile siku za kitaifa, harusi, kusherehekea mavuno, siku ya kutoka jandoni au kuvunja ungo na kadhalika. Mbali na hayo, ngoma ni njia moja kuu ya kutuleta pamoja ili kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo.

Aidha, tunapocheza ngoma fulani siku ya taifa, tunapata kumbukumbu muhimu katika historia yetu. Kwa mfano, tunakumbuka jinsi tulivyokuja pamoja kujikomboa kutoka kwa minyororo ya wakoloni. Ikiwa umoja wetu ulifukuza wakoloni sembuse umaskini?

Ngoma vilevile hutukumbusha umuhimu wa kuwepo kwa amani. Pia, ngoma hutuonya dhidi ya kuchukiana. Hutukumbusha kuwa amani, upendo na umoja ni mambo muhimu katika ujenzi wa nchi yetu.

Iwapo tutapenda ngoma zetu za kienyeji na kutunga nyimbo za kisasa zenye kukuza ushirikiano, basi tutapiga hatua kubwa katika maendeleo yetu.

**Kazi ya kikundi**

Jiunge na wanafunzi wenzako. Jadilianeni kuhusu aina na mifano mbalimbali ya viunganishi katika Kiswahili. Tungeni sentensi sahihi mkitumia viunganishi hivyo.

## Vihisishi

Vihisishi ni maneno ambayo huonyesha hisia mbalimbali za mzungumzaji. Unaweza kuelezea hisia zako kuhusu shughuli mbalimbali za kijamii kwa kutumia vihisishi. Vihisishi hutumika pamoja na alama ya hisi (!).

*Tazama mifano iliyotolewa hapa chini.*

a) Huree! Tumemaliza kujenga nyumba.
b) Alaa! Mbona harusi haijaanza?
c) Ole wangu! Kumbe nilikosa mengi katika mkutano wenu!
d) Inshallah! Tukutane kesho twendelee na kazi yetu.

**Zoezi**

Soma kifungu kifuatacho. Bainisha aina mbalimbali za vihisishi vilivyotumika.



Sote tulifunga safari ya kumtembelea Gatete kijijini mwao. Lo! Hatukuamini macho yetu tulipofika huko. Kumbe kijiji hicho kilikuwa safi na tulivu mno!

Gatete alipokuja kutulaki, tulimpa pongezi.

"Hongera! Mnafanya kazi nzuri kweli," Ndoli alisema.

Gatete alimtazama Ndoli kwa mshangao. Hakuelewa sababu za hongera zake.

"Jamani! Mbona kijiji hiki chenu ni safi namna hii?" nilimwuliza Gatete.

"Ahaa! Sisi hutupa taka zote katika majaa. Pia, tunachimba mitaro ili tusiwe na vidimbwi vya maji. Yeyote, awe mdogo au mkubwa, huokota majani makavu au taka zozote popote," Gatete alisema akitabasamu.

"Maskini sisi! Hatufanyi hivyo hata!" Ndoli alisema.

"Alaa! Mnafaa mwanze kufanya hivyo moja kwa moja. Usafi ni jambo muhimu sana katika maisha yetu."
"Naam! Kuanzia leo, nitahimiza wanakijiji wenzangu ili kwa pamoja tudumishe usafi."

### Kazi ya kikundi

Jiunge na wanafunzi wenzako. Fanyeni utafiti kuhusu aina mbalimbali za vihisishi katika Kiswahili. Tungeni sentensi sahihi mkitumia vihisishi hivyo.

### Zoezi la ziada

Soma kifungu hiki. Bainisha na uanishe aina saba za maneno ya Kiswahili (nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi, viwakilishi, viunganishi na vihisishi)

**Kukoga mwaka**



Hapo zamani, watu tofauti walikuwa na itikadi mbalimbali kuhusu kuanza kwa mwaka. Baadhi yao walisherehekea siku hiyo kwa kuchinja na kuandaa karamu murua! Nao wengine waliwatambikia wazee wao waliofuata njia ya marahaba. Zaidi ya haya, baadhi ya watu waliamini kuwa ni lazima mwaka mpya uanze kwa usafi. Hii ndiyo ilikuwa sababu ya kukoga mwaka.

Kukoga mwaka kulikuwa na utaratibu wake. Kazi hizo zote zilitegemea mwanzo wa mwaka wa kiasili bali si ule wa kizungu. Mwaka huo wa kiasili ulikuwa ukianza saa thenashara hivi za asubuhi. Hivyo basi, kabla ya wakati huo, wenyeji walirauka saa kumi. Madhumuni ya kuamka wakati huo yalikuwa kusafisha kila kitu kabla ya mapambazuko. Basi wanawake waliamka na kukusanya vitu vyote ambavyo viliweza kuoshwa na kuvipeleka mtoni. Wengine walibaki nyumbani kusafisha vile vitu ambavyo havikuweza kuchukuliwa mtoni lakini ambavyo vilihitaji kuoshwa au kusafishwa.

Baadhi ya vitu vilivyooshwa mtoni vilikuwa nguo zilizomea koga, vyungu, sahani, sufuria na vyombo vinginevyo. Baadhi ya watu walisafisha vyombo hivyo kwa sabuni lakini wengine walivisafisha kwa majani maalum.

Jambo lililokuwa la mwisho kufanywa huko mtoni ni kuwaosha watoto. Baadaye watu wazima wangeoga wao wenyewe. Wakati mwingine, watu wangeosheana miguu kama ishara ya upendo.

Nao wanawake wale waliobaki nyumbani walikuwa na kazi kubwa ya kusafisha nyumba mbalimbali za msonge. Baadhi yao walipaka sakafu kwa samadi mbichi iliyochanganywa na udongo na maji. Nao wanawake wengine waliondoa masizi yaliyokuwa yakining'inia kwenye mapaa.

Vijana nao walisomba maji kutoka mtoni. Maji hayo yangetumiwa na wanaume kuogea. Wao pia wangeoga baadaye.

Wanaume nao hawakukaa bure. Ilikuwa kazi yao kufyeka na kusafisha uani, mbele na pande zote za nyumba. Pia ilikuwa kazi yao kufyeka nyasi zo zote zilizokuwepo pale kiamboni pamoja na kukata matagaa yasiyohitajika ili kwamba jua la mwaka mpya lichomozapo liangaze boma zima.
Je, ni kwa nini kazi hizo zote zilifanyika? Hata wakati huo, wenyeji waliamini kuwa Mungu hakupenda uchafu. Isitoshe, waliamini kuwa mtu akianza jambo fulani kwa nuksi basi hatafanikiwa katika mambo mengi. Hivyo basi, imani yao ilikuwa kwamba mwaka ukianza kwa uchafu basi shughuli zao zote mnamo mwaka huo zingekumbwa na nuksi. Hapana hata mmoja aliyetaka kutofanikiwa. Naam! Mwaka mpya ungeanza kwa usafi kweli.

### Kazi ya kikundi

Jiunge na wanafunzi mwenzako. Someni vifungu mbalimbali vya habari vilivyopo katika sura hii ya nne. Bainisheni na kuainisha aina saba za maneno ya Kiswahili katika vifungu hivyo.

## D Matumizi ya wakati uliopita -li- hali yakinishi na hali kanushi

Tunaweza kuzungumzia shughuli mbalimbali za kijamii tulizoshiriki muda au wakati uliopita. Wakati huu huwasilishwa na -li-.

Vitendo katika wakati uliopita vinaweza kuwa katika hali yakinishi au katika hali kanushi. Hali yakinishi ni ya kukubali na hali kanushi ni kukataa.

***Tazama mifano ya matumizi ya wakati huu iliyotolewa kwenye jedwali lifuatalo.***

| | Hali yakinishi | Hali kanushi |
|---|---|---|
| i) | Watu wengi walihudhuria mazishi ya mjomba. | Watu wengi hawakuhudhuria mazishi ya mjomba. |

| | | |
|---|---|---|
| ii) | Mimi nilienda mkutanoni. | Mimi sikuenda mkutanoni. |
| iii) | Ibada ilianza saa tano kamili. | Ibada haikuanza saa tano kamili. |

Je, unaona mabadiliko gani katika hali kanushi ya vitenzi hivyo?
Katika jedwali lililopo hapo juu, vitenzi walihudhuria, nilienda na ilianza vipo katika hali yakinishi au kukubali kwa wakati uliopita.
Vitenzi hawakuhudhuria, sikuenda na haikuanza vimo katika hali ya kukataa yaani hali kanushi kwa wakati uliopita.
Kiambishi 'li-' hakitumiki katika hali kanushi. Huondolewa.

**Kazi ya wanafunzi wawili wawili**

Jiunge na mwenzako. Tungeni sentensi sahihi kuhusu shughuli za kijamii mkitumia wakati uliopita katika hali yakinishi na kanushi.

## E Matumizi ya wakati ujao -ta- katika hali yakinishi na hali kanushi

Wakati ujao hutumiwa kuelezea mawazo au vitendo vitakavyofanyika baadaye. Kiambishi -ta- hutumika pamoja na kitenzi husika kuonyesha kuwa kitendo kitafanyika baadaye.

Tunaweza kuzungumzia shughuli mbalimbali za kijamii ambazo zitafanyika baadaye. Mfano: unapoandika ratiba ya shughuli au kutoa maelekezo ya mambo yanayofaa au ambayo hayafai kufanywa, unatumia wakati ujao.

Vitendo katika wakati ujao vinaweza kuwa katika hali yakinishi au kanushi. Hali yakinishi ni ya kukubali na hali kanushi ni kukataa.

***Tazama mifano iliyotolewa kwenye jedwali lifuatalo.***

| | Hali yakinishi | Hali kanushi |
|---|---|---|
| i) | Mkutano ujao utaandaliwa hapa. | Mkutano ujao hautaandaliwa hapa. |
| ii) | Jembe hilo litatufaa sana. | Jembe hilo halitatufaa sana. |
| iii) | Nyinyi mtafyeka shamba lote. | Nyinyi hamtafyeka shamba lote. |

Vitenzi vilivyopo katika jedwali viko katika wakati ujao.

Je, unaona mabadiliko gani katika hali kanushi ya vitenzi hivyo?

Katika jedwali lililopo hapo juu, vitenzi utaandaliwa, litatufaa na mtafyeka vipo katika hali yakinishi au kukubali kwa wakati ujao.

Vitenzi hautaandaliwa, halitatufaa na hamtafyeka vimo katika hali ya kukataa yaani hali kanushi kwa wakati ujao.

## Kazi ya wanafunzi wawili wawili

Jiunge na mwenzako. Tungeni sentensi sahihi kuhusu shughuli za kijamii mkitumia wakati ujao. Mzingatie hali yakinishi na kanushi.

### *Mifano*

ABATONI: Vijana watafyeka barabara.
NDOLI: Vijana hawatafyeka barabara. Watasomba maji ya kujengea nyumba.
ABATONI: Wazee hawatasomba maji ya kujengea nyumba. Watatoa maelekezo.

### Maswali ya marudio

1. Eleza mambo muhimu ambayo hutendeka katika shughuli za *ubudehe*.
2. Linganisha na utofautishe shughuli za mazishi na harusi katika jamii.
3. a) Bainisha wahusika wakuu katika shughuli hizi za kijamii:
    - i) Mazishi
    - ii) Harusi
    - iii) Ibada msikitini au kanisani

   b) Eleza tofauti za kimawasiliano katika shughuli zilizotajwa hapo juu.
4. Tunga sentensi ukitumia msamiati ufuatao:
   a) kuchimba mitaro
   b) kusomba maji
   c) kula kiapo
   d) peleka mahari
5. Taja sherehe nne muhimu za jamii katika eneo utokako huku ukiielezea kila moja umuhimu wayo.
6. Wewe ni kiongozi wa kikundi kinachoshiriki katika shughuli fulani ya kijamii. Chagua shughuli upendayo kisha utoe maelekezo kwa wanachama wa kikundi chako.
7. Eleza manufaa ya kazi ya *umuganda* kwa jamii ya Wanyarwanda.
8. Taja mambo mawili yanayoweza kukuonyesha kuwa tungo ni swali.
9. Tunga maswali matano ukitumia viulizi mwafaka.
10. Zipo aina ngapi za maneno ya Kiswahili? Zitaje.
11. Yataje maneno kumi ya Kinyarwanda ambayo ni sawa na yale ya vihisishi vya Kiswahili.
12. a) Nomino ni nini na huweza kuitwaje pia?
    b) Tunga sentensi tano sahihi ukitumia aina mbalimbali za nomino.
13. Tambulisha vitenzi katika maneno yafuatayo:
    msamaha samehe hisi kihisishi rehema kurehemu rehemu fikira fikiri kilio lia
14. Zieleze aina zote za vivumishi ambazo umejifunza hadi sasa. Tunga sentensi ukitumia kila mojawapo.

15. Eleza tofauti iliyopo kati ya viunganishi na vihisishi.
16. Andika aya moja kuhusu shughuli fulani ya kijamii. Tumia maneno yote saba ya Kiswahili katika aya hiyo kwa usahihi.
17. Pigia kistari sentensi zilizopo katika wakati ujao na useme ikiwa ni hali yakinishi au kanushi.
    i) Siendi Kigali.
    ii) Wanaenda harusini.
    iii) Nitashiriki katika kazi zote kijijini.
    iv) Aliniita sikusikia.
    v) Hawatachelewa leo.
18. Eleza umuhimu wa ushirikiano katika jamii.
19. Taja mambo yote muhimu uliyojifunza katika sura hii.

# Faharasa

**adimika** – kosa kupatikana kwa urahisi
**ambukiza** – enezea ugonjwa
**andaa** - tayarisha
**ankra** – orodha ya vitu vilivyouzwa pamoja na bei ya kila bidhaa
**anuani** – maelezo ya mahali mtu anapoishi ambayo huandikwa katika barua
**asali** – namna ya kitu kioevu na kitamu sana kitengenezwacho na nyuki
**azma** – lengo au shabaha
**bainisha** – tambua jambo
**bao** – mpira kuingia katika lango katika mchezo wa kandanda (goli)
**baridi kali** – hali isiyokuwa na joto na isisimuayo sana mwili
**bei** – kiasi cha pesa kinachotumiwa kununulia ama kuuzia bidhaa fulani
**burudani** - starehe
**burudisha** – sababishia raha
**chai** – zao la mchai
**dumisha** – endeleza
**faranga** – pesa, fedha, dirhamu, senti, fulusi
**filisika** – ishiwa na mali
**fyeka** – kata nyasi
**gharamia** – lipia gharama
**harage/haragwe** – nafaka ya jamii ya kunde
**haramu** – -siyoruhusiwa, -siyokuwa halali
**Hisabati** – sayansi ya tarakimu ijumuishayo aljebra
**hitaji** – kuwa na haja ya kitu
**huzuni** – hisia za majonzi
**ibuka** – tokeza
**idadi** – hesabu au jumla ya vitu
**ilani** – tangazo la kuonya watu wasifanye jambo fulani hasa lenye kuleta madhara
**ingawa** – hata ikiwa
**jadhba/jazba** – hisia isababishayo kujisahau
**jamii** – watu wanaoishi pamoja
**jangili** – mwindaji haramu
**jedwali** – orodha ya maelezo kuhusu mambo fulani kwa namna yatakavyofuatana

**jibini** – chakula kinachotengezwa kwa kuyagandisha maziwa na kuyatoa maji
**jukumu** – wajibu
**jumuiya** – mkusanyiko wa watu
**kabuti** – koti zito la kuzuia baridi
**kagua** – chunguza kwa makini
**kahawa** – zao la mkahawa ama mbuni
**kandanda** – mchezo wa miguu
**kauli** – usemi
**kiasili** – kienyeji
**kifaa** – chombo
**kikao** – mkutano
**kipindi** – muda
**kipusa** – pembe ndogo ya kifalu
**kivuna nafaka** – mashine kama trekta ambayo huvuna ngano huku ikiitoa wishwa
**kiwanda** – mahali panapotengenezwa bidhaa
**kodi ya mapato** – fedha zinazolipwa serikali kama ushuru wa mapato ya mtu
**kupanda** – tia mbegu mchangani ili ziote
**limbikiza** – weka vitu kidogo kidogo ili viwe vingi
**lishe bora** – chakula kinachohitajika kwa afya nzuri ya mwili
**maabara** – mahali mnamofanyiwa majaribio ya kisayansi
**maalumu** – -enye sifa ya kipekee
**mada** – kiini cha jambo linalozungumziwa
**majira** – wakati au kipindi
**majira ya kiangazi** – kipindi cha kiangazi
**majira ya kipupwe** – kipindi cha baridi
**majira ya mvua** – kipindi cha mvua
**majira ya vuli** – kipindi cha mvua chache
**majivuno** – hali ya kujiona
**manufaa** – faida
**mapato** – kitu kinachopatikana kama vile baada ya kufanya kilimo ama kufanya biashara.
**masuala mtambuka** – mambo muhimu yanayoiathiri jamii katika kipindi cha sasa
**matini** – kifungu cha habari iliyoandikwa

**mazingira** – mambo yanayotuzunguka mahali tunapoishi
**maziwa** – kitu kioevu kitokacho ndani ya titi la mnyama
**mbatata** – namna ya viazi vilivyo mviringo na visivyo na ladha
**mbinu** – njia au namna ya kufanyia jambo
**mbuga** – eneo lililotengewa wanyama wa porini
**mchele** – mpunga uliokobolewa,yaani kuondolewa mashuke
**mfawidhi** – mtu aliyepewa wajibu wa kuendesha shughuli fulani, kama vile mkutano au sherehe fulani
**mfugaji tajiri** – mfugaji ambaye ana mali nyingi
**mifugo** – wanyama wanaotunzwa nyumbani
**mikahawa** – mimea izaayo kahawa
**mkulima tajiri** – mkulima ambaye ana mali nyingi
**mmomonyoko** – kuchukuliwa kwa udongo wenye rutuba
**mori** – hasira kali
**mshinde** – aliyeshindwa
**mshindi** – aliyeshinda
**msimu** – majira
**mtama** – zao la mtama
**muhogo** – mzizi wa muhogo unapokuwa umekomaa tayari kwa kuliwa
**ndama** – mtoto wa ng'ombe
**ndizi** – tunda la mgomba linalomea kwenye mkungu.
**ngeli** – kikundi cha majina au nomino zinazofuata kanuni sawa za kisarufi
**njugu** – mbegu zitengenezewazo mafuta ya karanga
**nyama** – sehemu laini ya mwili ambayo ikikatwa hutoka damu
**pandwa** – ingiwa na
**pekee** – pweke; bila ya -ingine
**pesa** – noti na sarafu zinazotolewa na kuidhinishwa na serikali kuwa ni fedha rasmi za kubadilishana na bidhaa.
**pori** – mahali palipo na miti mingi, nyasi na vichaka
**ratiba** – mpango wa mfululizo wa shughuli fulani
**refa** – mwamuzi katika mchezo wa mpira
**rejesta** – lugha inayotumiwa katika mahali maalum, kama vile hospitalini, hotelini, msikitini na kwingineko
**rutuba** – mbolea ya kukuzia mimea ardhini
**sajili** – rejesta
**shabiki** – apendaye sana timu

**sheria** – kanuni za kuongoza watu
**shime** – neno la kuhimizia mtu
**shiriki** – husika au kuungana na watu katika kufanya shughuli fulani
**soseji** – namna ya chakula kinachotengenezwa kutoka kwa nyama ya nguruwe au ya ng'ombe
**suala** – jambo au hoja
**sufu** – manyoya ya kondoo
**takwimu** – nambari zinazoeleza ukweli kuhusu matukio ya mambo, kwa mfano idadi ya watu katika eneo fulani
**tambua** – fahamu au maizi
**tanbihi** – maelezo yanayotoa habari muhimu
**tathmini** – pima
**tegemea** – weka matumaini kupata kitu
**tia mdomoni** – kumsema ama kumsengenya mtu
**ulinzi** – ulindaji, hali ya kulinda
**upanzi** – upandaji (uwekaji mbegu ardhini)
**utafiti** – uchunguzi wa kisayansi
**vanila** – kiungo kiyafanyayo maziwa yaliyoganda kuwa na ladha ya kupendeza
**viazi vitamu** – namna ya viazi vikubwa na vilivyo vitamu
**wadau** – mtu mwenye maslahi katika shughuli fulani
**wadhifa** – madaraka au cheo fulani
**waligonga ndipo** – walisema ukweli
**wasifukazi** – maandishi yanayoeleza kuhitimu kwa mtu katika kutekeleza kazi fulani, aghalabu, kimasomo, tajiriba ya kazi na ujuzi wake
**wishwa** – takataka za nafaka kama vile mtama au ngano
**yakinishi** – hali ya kukubali
**zao** – kile kinachozaliwa na mmea
**zaraa** – kilimo

## Vitabu vya rejea

Kagwa, F.M. na Waihiga, G. (2007) *Kamusi Changanuzi ya Methali*. Nairobi: Moran (E.A.) Publishers.

Kipande, M. (2013) *Sarufi.* Nairobi: Moran (E.A.) Publishers.

Massamba D.P.B. (2004) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Dar es Salaam. TUKI.

Mogambi Hezron (2007) *Premier Golden Tips; Kiswahili kwa Shule za Upili*. Nairobi: Moran (E.A.) Publishers.

Mutali Chesebe (2010) *Premier Golden Tips; Stadi za Uandishi wa Insha*. Nairobi: Moran (E.A.) Publishers.

Oxford University Press (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Toleo la tatu.
Oxford University Press.

Rwanda Education Board. (2015) *Kiswahili Sylabus for Ordinary Level. S1-S3*. Kigali: Rwanda Education Board.

TUKI (1990) *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam. TUKI.